Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

## Kikao cha Arobaini na Nane – Tarehe 15 Agosti, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo ni Kikao cha Arobaini na Nane cha Mkutano wetu wa Nane.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA M. SALUM):**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MHE. DUSTAN L. KITANDULA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA FEDHA):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Juu ya Wizara ya Fedha Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 380

### Mikakati ya Kupambana na UKIMWI Nchini

**MHE. MOZA A. SAIDY** aliuliza:-

Kwa mujibu wa takwimu za Mashirika ya Kimataifa, Tanzania ni nchi ya sita (6) Duniani kwa kuwa na waathirika wengi waishio na virusi vya UKIMWI (VVU):-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo?

(b) Je, Serikali kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa ina mikakati gani ya kupambana na kuzuia maambukizo mapya ya VVU/UKIMWI?

(c) Je, walengwa (Watanzania) wana ufahamu wa kutosha juu ya mikakati hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Utafiti wa viashiria vya UKIMWI unaonyesha kuwa maambukizi ya UKIMWI nchini yameshuka kutoka asilimia saba (7%) kwa mwaka 2003/2004 hadi asilimia Tano nukta saba (5.7%) mwaka 2007/08. Tanzania ni kati ya Nchi 32 Duniani ambazo maambukizi mapya yamepungua kwa asilimia 25 (25%).

Pamoja na mafanikio hayo, bado idadi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI nchini inaonekana kuwa kubwa kutokana na kuanzishwa kwa matibabu kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI (VVU) na UKIMWI mwaka 2004. Hatua hii imesaidia kuwafanya waendelee kuishi maisha marefu na ya afya na hivyo takwimu kuonyesha kuwepo kwa waathirika wengi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa imeandaa Mwongozo unaoainisha huduma muhimu za kudhibiti UKIMWI na Halmashauri zote zinafundishwa na kuelekezwa kuzingatia mwongozo huo. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inatafuta rasilimali fedha za kusaidia udhibiti UKIMWI ngazi ya Halmashauri. Mkakati wa kinga wa mwaka 2009-2012 pia umeandaliwa na mikoa yote imeelekezwa na kuwezeshwa kuandaa mipango yao ya kudhibiti maambukizi mapya, kuitekeleza na kufuatilia utekelezaji.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi za kutoa elimu kuhusu mikakati ya kujikinga na maambukizi mapya na umuhimu wa kujua hali zao za afya zinaendelea. Hivi sasa unyanyapaa na uelewa wa wananchi ni kati ya asilimia 50 mpaka 60. Mkakati wa kupunguza unyanyapaa na ubaguzi wa mwaka 2012 hadi 2017 umeandaliwa na mpango wa kuelimisha wananchi unaendelea. *(Makofi)*

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na elimu hiyo kutolewa. Je, ni jinsi gani elimu hiyo inawafikia maeneo hatarishi kama vile vilabu vya pombe za kienyeji, *guest* bubu, ngoma za asili na kadhalika?

Pili, kuna tetesi dawa za kurefusha maisha zinazotumiwa na waathirika ni *fake.*

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na tetesi hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa mkakati wa muda mrefu kama ifuatavyo. Serikali

imeandaa mkakati wa kutoa elimu kwa jamii nzima ya Watanzania na mkakati huo unaongozwa na mbinu mbalimbali. Mbinu moja muhimu ni vyombo vya habari.

Uelimishaji kupitia vyombo vya habari unapenya kila mahali, huko kwenye ngoma, *Guest Houses* na kila mahali ambao unaleta hatarishi. Vyombo vya habari vimekuwa mstari wa mbele katika kuelimisha Umma juu ya mapambano dhidi ya UKIMWI. Lakini sasa kama nilivyosema tumefikisha mkakati huu mpaka kwenye Serikali za Mitaa ambako kuna uongozi mpaka kwenye Serikali za Mtaa. Kwa hiyo, huko nako kwenye Halmashauri wanao mkakati wa kufikisha elimu hii mpaka kwa kaya zote za Watanzania.

Kwa hiyo, nataka kuamini kwamba hata wewe Mheshimiwa unafahamu kwamba elimu hii sasa angalau kama nilivyosema si chini ya asilimia 60 angalau wananchi wanajua mambo mbalimbali yahusuyo UKIMWI. Huko kwenye *Guest Houses* fulani fulani unazolala utakuta hata elimu iko humo humo na hata silaha ziko humo humo tayari. Wenye *Guest Houses* na wenye hoteli za kulala wameshajua namna ya kuwaweka salama wateja wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, dawa *fake,* kwa sababu anasema ni tetesi sina majibu. Labda kama kuna ushahidi tungeweza tukasema. Lakini binadamu ni binadamu inawezekana kwamba kuna watu ambao wameigiza hizi dawa na kuingiza kwa namna nyingine, tushirikiane tu popote pale ambapo mtu ana taarifa kwamba zinauzwa au zinapatikana dawa zisizostahili atoe taarifa ili tuchukue hatua. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa inasemekana nchi ya Amerika ilipata chanjo ya ugonjwa huu na sasa inasema imeshapata dawa za ugonjwa huu.

Je, nchi yetu ina habari hiyo na kama ina habari itakuwa tayari kuagiza dawa hizo sasa kwa ajili ya kusaidia watu wetu ili waweze kupona kabisa na sio kurefusha maisha?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi uchunguzi wa tafiti ndio unaonyesha kwamba kuna matumaini ya kuwepo kwa dawa. Lakini mpaka sasa hatuwezi kusema kwamba sasa tunayo dawa ya kutibu *HIV.* Kwa hiyo, tunaendelea na matibabu yaliyopo ya kupunguza makali ya virusi vile kwenye mwili, lakini mpaka pale tiba hiyo itakapokuwa imethibitika na kukubalika na *WHO* ndipo sasa maamuzi ya kuanza kutumika yanaweza yakafuata.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge anachosema Mheshimiwa Waziri dawa bado. Kwa hiyo, kufungulia mbwa hapana ni marufuku. Bado tuko Singida.

Na. 381

**Halmashauri Kutorejesha Mishahara na Maduhuli**

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Agizo Namba 370 la Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1997 linaagiza kuwa, mishahara isiyolipwa inatakiwa ipelekwe Benki ndani ya siku 10 za kazi:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani za kinidhamu kwa Watendaji wa Halmashauri zilizokiuka agizo hilo na kushindwa kurudisha fedha za mishahara isiyolipwa kama vile Halmashauri ya Manispaa ya Singida 929,905,200/=), Iramba (17,504,172/=), Manyoni (15,450,394/=)?

(b) Je, hatua gani zimechukuliwa kwa Mawakala wa kukusanya mapato wa Manispaa ya Singida ambao hawakurejesha maduhuli yenye thamani ya shilingi 46,940,900.00 kama taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG)* na 2010 inavyoeleza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo;-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa Hesabu za Serikali mwaka 2009/2010, Halmashauri za Wilaya za Manyoni, Iramba na Manispaa ya Singida zilikuwa na hoja zilizotokana na mishahara ambayo haikurejeshwa Hazina.

Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ilirejesha shilingi 15,450,399/= kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida kwa *Payment Voucher* Na. 15 ya mwaka 2010 na kupatiwa risiti Na. 16336232 na hoja hii imefungwa baada ya kuhakikiwa. Halmashauri ya Wilaya ya Iramba imewasilisha kwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida shillingi 16,578,740/= na shilingi

926,172/= zililipwa kwa mtumishi aliyekuwa hajalipwa fedha hizo.

Aidha, Halmashauri ya Manispaa ya Singida tarehe 27 Machi, 2010 ilirejesha shilingi 29,905,200/= kwa Katibu Tawala Mkoa ambazo zilikuwa ni mishahara ya walimu wa Sekondari waliopangiwa vituo katika Manispaa hiyo lakini hawakuripoti.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Halmashauri ya Manispaa ya Singida katika mwaka 2009/2010 iliingia mkataba na Kampuni inayoitwa Costantino Kebero kwa ajili ya ukusanyaji wa ushuru wa soko la Mjini Singida kwa thamani ya shilingi milioni 90.0 na *Volcano Cooperative Society* iliyopewa kazi ya kukusanya ushuru katika soko la Ukombozi kwa thamani ya shilingi milioni 28.9. Wakati ukaguzi unafanyika Mawakala wote walikuwa wanadaiwa shilingi 46,940,900/=. Baraza la Madiwani katika kikao chake cha tarehe 20 Julai, 2010 liliazimia na kuwataka Mawakala hao kurejesha fedha zote ambazo zilikusanywa na hazikurejeshwa katika Halmashauri.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza katika swali langu la msingi niliuliza kwamba agizo Na. 370 na Memoranda ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 iliagiza kwamba mishahara isiyolipwa itatakiwa kurudishwa Wizara ya Fedha ndani ya siku 10 na Naibu Waziri amenijibu kwamba fedha hizi zilirudishwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa Singida na hizi fedha zimerudishwa zaidi ya mwaka mmoja baada ya ripoti ya CAG kutoka na si ndani ya siku 10. Swali langu je, Naibu Waziri anaweza kuliambia Bunge lako Tukufu ni lini agizo hili Na. 370

lilitenguliwa na kuagiza kwamba fedha za mishahara isiyolipwa zirudishwe kwa Katibu Tawala wa Mkoa badala ya kurudishwa Wizara ya Fedha?

Swali la pili, kwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Singida iliingia mikataba halali na Mawakala wa Kukusanya Mapato au Ushuru katika masoko na Waziri amekiri kwamba fedha hizi bado hazijarudishwa na Baraza la Madiwani lililokaa liliagiza fedha hizi zirudishwe na mimi nina uhakika kwa sababu naingia kwenye vikao vya *RCC* hizi fedha ni kweli bado hazijarudishwa mpaka sasa hivi.

Je, kutoa agizo tu kwamba fedha zirudishwe wakati Halmashauri ya Manispaa ya Singida iliingia mkataba halali na hao Mawakala bila ya kuchukua taratibu za kisheria ni sawasawa na si kuipotezea Halmashauri ya Manispaa mapato yake? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi namwelewa Mheshimiwa Christowaja anachozungumza hapa. Tunapozungumza habari za Halmashauri usije ukafikiri *sales* tu zinajiendea zenyewe zinakwenda tu hivi. Katika hizo Ofisi za Mikoa kwanza tumeanzisha hiyo *Sub Office* iko hapo mkoani tunayozungumza.

Mimi hapa ninachoeleza hapa naeleza ili wewe ujue mahali pa kwenda kuulizia kwamba ni kweli *payment voucher* anayoitaja hapa iko hapa. Yaani mimi hapa *there is no problem* unachosema wewe ndicho tunachosema sisi. Hakuna mtu katika Ofisi ya Waziri Mkuu ambaye anaona raha fedha zinavyopotea anafurahi hizi fedha zinapopotea.

Mimi nimeonyesha hii ili ujue, ili ukitafuta fedha hizi kwamba Halmashauri hizi ninazozitaja hapa zililipa au hazikulipa pitia katika mkondo huu ninaokwambia. Ukienda kule Hazina watakwambia zipi fedha hizi zinakusanywa zote kimkoa na zikishakusanywa kimkoa zinachukuliwa zinaingiwa katika Hazina. Hazina yenyewe iko hapa hapa Ofisini. Kwa hiyo, hakuna kitu kingine ambacho kimekiukwa hapa. Nenda kaangalie vizuri uje utuambie, mimi nitashirikiana na wewe tutasaidiana na mimi nina uchungu na fedha hizi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, amezungumzia hii Halmashauri niliyoi-*quote.* Ni kweli na nataka niseme hapa anachosema Mheshimiwa Christowaja ukienda kwenye *CAG's report* hii yote anayosema iko pale. Kwa hiyo siwezi kusimama hapa nikabishana naye nikakataa nikasema siyo kweli. Tumemwita Mkurugenzi Mtendaji alikuwa Morogoro tumemwambia arudi Singida kwamba anatuambia tu fedha hizi hazijaenda zimepitia kwenye Baraza *is not enough* na tumeandika barua tumemwambia tunataka utueleze akishindwa atuambie anatumia hatua gani za kisheria kuhusu hizi shilingi milioni 40 ambazo hazikulipwa hapa ambazo na-*propose* hapa na mimi nataka nikuthibitishie kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, sisi TAMISEMI tuta-*trace* hizi fedha kuhakikisha kama zimekwenda na zimerejeshwa.

Tunachosema hapa hao Mawakala ambao si waaminifu ambao wanataka kuingia katika hatua hiyo kwa sababu wanataka kuchukua hiyo kazi halafu mbele ya safari anashindwa msiwape kazi hizo tena. Unamkuta mtu ana rekodi hapa mwaka jana hakulipa na mwaka wa juzi hakulipa mwaka huu mnampa Wakala huyo huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sauti hii Mheshimiwa inapanda sio kwamba mimi nataka kumgombeza ni msisitizo tu kuhusu jambo hili ninalozungumza hapa. (*Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Msisitizo wa Mheshimiwa Christowaja ni kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwa nini msifuate utaratibu ule wa Mheshimiwa Kagasheki wa kushughulikia watumishi wa Serikali wakorofi?

Na. 382

**Dhamira ya Ujenzi wa Zahanati Kwa Kila Kijiji Nchini**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Serikali imedhamiria kujenga zahanati kwa kila kijiji na Kituo cha Afya kwa kila Kata nchini:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa zahanati katika vijiji vya Vikonge, Bungwe, Ngomalusambo, Igalala, Igalula, Kasinde na Bujombe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya kujenga Kituo cha Afya katika kila Kata na Zahanati kila Kijiji inatokana na matakwa ya Sera ya Afya ya Mwaka 2007 ikiwa na lengo la kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Sera hii inatekelezwa chini ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi ambayo imejielekeza katika kuongeza, kurekebisha, kuimarisha vituo vya kutolea huduma za afya na Ustawi wa Jamii na kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali watu, vifaa, vifaatiba na dawa katika vituo vyote vya afya na kwa ubora unaotakiwa.

Vijiji vya Vikonge na Bungwe ni vijiji vipya vilivyotangazwa kwa Tangazo la Serikali Na. 392 la tarehe 15 Oktoba, 2010 kabla ya hapo vijiji hivyo vilikuwa ni Vitongoji katika Kijiji cha Majalila hivyo havikuwepo katika mpango wa Halmashauri wa kujengewa zahanati. Aidha, Bujombe sio kijiji bali ni Kitongoji katika kijiji cha Luega ambacho tayari kuna Kituo cha Afya cha Mwese kinachotoa huduma za afya kwa wakazi wa kijiji hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda katika mwaka 2012/2013 imetenga shilingi milioni 176.7 kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Halmashauri imeweka kipaumbele cha kutumia fedha hizi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi katika zahanati za Kapalamsenga, Sibwesa, Milala, Kasekese, Kabungu na ukarabati wa Zahanati ya Msimbo, ukarabati wa kituo cha afya cha Usevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vya Ngomalusambo, Igalala, Igalula na Kasinde vitawekwa katika mpango wa

kujengewa Zahanati kwa awamu kadiri upatikanaji fedha utakavyoruhusu. *(Makofi)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa vijiji vya Igalula, Mchakamchaka, Mpembe na Isengule ni vijiji ambavyo toka *operation* ya vijiji vimekuwepo.

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma hiyo ya Zahanati katika vijiji hivyo?

Swali la Pili, Kata ya Mpanda Ndogo Kata ya Katuma, Kata ya Sigwesa na Kata ya Kabungu ni Kata ambazo ni kubwa sana na zimekuwa zikipokea wageni siku hadi siku. Zina idadi kubwa ya watu wanaoishi katika maeneo hayo.

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma ya vituo vya afya katika Kata hizo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso Mbunge wa Mpanda Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, anachosema Mheshimiwa Kakoso ni sahihi kuwa tuliamua kuwa kila kijiji kiwe na Zahanati yake na utaratibu tuliopanga tuufanye ni ile *oppotunity and obstacles to Development O and O.D.* kwamba mtakuwa mnaonyesha vipaumbele vyenu. Na anasema vijiji hivi vimekuwepo toka uhuru lakini vijiji hivi tunatakiwa tuvi-*check* tena katika vipaumbele vya

Halmashauri kuona kuwa wao wamepanga kuwa vijiji hivi viwe na zahanati?

Kwa kuwa tunavijenga kama tunavyojenga zile shule za sekondari na kama tunavyojenga shule za msingi. Jitihada zilezile za kushirikiana na Halmashauri napenda nichuke hivi vijiji anavyovitaja Mheshimiwa Kakoso lakini akumbuke kuwa *the bottom line is* kwamba tuta -*check* pia kama wao wanaona kuwa hili ni kipaumbele kwa sababu kama hawatachoma matofali, kama hawatafyatua matofali, kama hawataenda kubeba mchanga wapeleke Halmashauri na sisi TAMISEMI tutafanya nini katika hali ya namna hii.

La pili, ambalo ninataka kusisitiza hapa ni kwamba vijiji hivi hatukusema kuwa ni *compulsory* kuwa kijiji kikishatokea kuna kijiji kiko hapa na kingine kiko pale. Pale ambapo itaonekana vijiji viko karibu, karibu wanaweza kuunganisha nguvu za wananchi kwa pamoja wakaweka nguvu katika kituo kile. Vinginevyo tutakuwa na matatizo ya watumishi kuwapeleka huku na kule sina maana ya kutengua torati nina maana tusije tukapoteza nguvu katika vile vijiji tutakwenda ku- *study* hili la Kata anazozisema hapa kwamba kuna Kata nyingi Mpanda nimekwenda na ninaifahamu tutakwenda wote na tutaangalia na Mkurugenzi tuone kuwa nini kinachotakiwa kufanyika lakini *formular* yake bado inabakia ni ileile niliyosema ya vijiji.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Vijiji vingi ambavyo wananchi walishajitolea sana kwa kujenga vituo vya Afya na Zahanati wamefikisha ngazi ya lenta na Serikali ilikuwa inategemewa imalizie kama ambavyo imeainisha kwenye Sera yake.

Tatizo la ukosefu wa huduma hiyo unatofautiana na eneo lenye barabara na lile lisilo na barabara.

Je, Serikali itakuwa tayari kuzikamilisha Zahanati ambazo ziko kwenye vijiji ambavyo havina barabara ili akina mama wajawazito wasipate taabu ya kubebwa kwenye vitanda wakati wa kwenda kujifungua?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninapata vitu viwili kwanza anazungumzia wale ambao wamefika katika *level* ya renta, ni kweli kuwa tulichokubaliana ni kuwa Halmashauri baada ya hapo na yenyewe isaidie zile jitihada za wananchi na sisi na Mbunge tunatakiwa tushirikiane katika jambo hili kuhakikisha kuwa tunasukuma Halmashauri na mapato yale ya *own source* yaani mapato ya ndani ndiyo yanatakiwa kutumika katika kazi hiyo.

Wakati mwingine tumepeleka katika *Constituence Development Catalysty Fund* Mbunge anaweza kuchukua hela zake na kupeleka hela yake kwa ajili ya kusaidia nguvu za wananchi kupitia ile *O and O.D.* ambayo nilikuwa nimezungumzia, lakini pia ameuliza swali hapa kuhusu barabara ni kweli kabisa kuwa ukijenga Zahanati na barabara hakuna na hizi *ambulance* au Bajaji tunazosema ziende kule ni kazi bure tutapoteza maisha ya watu ninajua kuwa katika nchi yetu tumepoteza akina mama na watoto wamezaliwa wamepotea kwa sababu ya barabara.

Ninakubaliana na wewe Mheshimiwa Mchemba na nikupongeze kwa kazi nzuri unayofanya katika Jimbo lako la Uchaguzi tutasaidiana na wewe katika hizo barabara

ambazo kama kuna Zahanati tulizojenga na vituo vya afya ili tuweze kukusaidia kukuondoa katika hali hiyo. *(Makofi)*

Na. 383

**Kupandisha Hadhi Mji Mdogo Mafinga**

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA** aliuliza:-

Mji mdogo wa Mafinga umekidhi vigezo vyote vya kuwa Halmashauri kamili ya Mji na vikao vyote vya Kisheria vimefanyika kuomba kupandisha hadhi mji huu, lakini Serikali haijajibu:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ombi hili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa mwaka 2011 Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) ilipokea maombi ya kupandisha hadhi Mamlaka ya Mji mdogo wa Mafinga kuwa Halmashauri ya Mji. Maombi haya yalikuwa na mapungufu kadhaa yakiwemo kutopata ridhaa ya vikao halali ya Kamati ya ushauri ya Wilaya *(DCC)* na Kamati ya Ushauri ya Mkoa *(RCC)* ambavyo ni vikao halali kwa mujibu wa Sheria.

Aidha, maombi hayakuwa na maelezo ya kina kuhusu hali halisi ya vigezo vya kupandisha hadhi Mamlaka hiyo. Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ilichukua hatua ya kuiandikia barua Mamlaka husika yenye kumb. Na CHB.215/358/10/60 ya 19 Julai, 2011 kumpatia maelekezo ya kukamilisha taratibu na vigezo vinavyotakiwa kuzingatiwa ili kuwezesha kushughulikia maombi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya majibu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilipokelewa Wizarani Julai, 2012 ikiwa ni takribani mwaka mmoja tangu maelekezo yatolewe. Pamoja na majibu ya barua hiyo kuthibitisha kuwa vikao vya *DCC* na *RCC* vimeridhia pendekezo la kupandisha hadhi Mamlaka hii kupitia muhtasari ya vikao hivyo, muhtasari wa *RCC* haukusainiwa na Mwenyekiti.

Aidha, mapungufu ya vigezo hayakurekebishwa hususan taarifa ya hali halisi kuhusu mapato ya ndani na matumizi, hadhi ya maeneo ya Mamlaka iwapo ni Makao Makuu ya Kata au Tarafa, idadi ya maduka ya rejareja yenye leseni yaliyopo na ukubwa wa eneo la Mamlaka hiyo. Mamlaka husika imeelekezwa kurekebisha mapungufu yaliyobainishwa kwenye muhtasari wa *RCC* na katika taarifa za hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya kupandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mafinga yatashughulikiwa kwa kuzingatia taratibu zilizopo kwa kuanzia na uhakiki wa vigezo mara baada ya mapungufu yaliyobainishwa yatakaporekebishwa na Mamlaka husika.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ninamheshimu Kaka yangu Naibu Waziri lakini kwa mujibu wa Kanuni Namba 45 naomba swali langu lipatiwe majibu upya. Kwa sababu Halmashauri ya Wilaya Mufindi haipaswi kupeleka maombi TAMISEMI na anaposema Mwenyekiti ni kitu cha ku- *sign* ina maana ni viongozi wote wa TAMISEMI ninaomba Mwongozo wako.

Na. 384

**Maslahi ya Walimu**

**MHE. MCHUNGAJI JACKSON N. MWANJALE (K.n.y. MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA)** aliuliza:-

(a) Je, ni kwa nini mishahara ya walimu haipandi licha ya kuwa wao ni zao la kila mtu?

(b) Je, ni tathimini gani imefanyika kuona madhara ya jambo hilo?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Machuche Mwanjelwa, lenye sehemu (a) na ( b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara kwa kada ya ualimu imekuwa ikiongezwa kila mwaka sambamba na nyongeza za mishahara zinazotolewa kwa watumishi wengine Serikalini. Takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha miaka nane kuanzia 2004/2005 hadi kufikia mwaka

2012/2013 wastani wa kianzia mshahara kwa walimu imekuwa ikiongezeka kwa 13% kama ifuatavyo:-

Kianzia mshahara kwa walimu wa Cheti kutoka shilingi 87,090 kwa mwaka 2004/2005 hadi shilingi 277,000 kwa mwaka 2012/2013.Walimu wenye Stashahada kutoka shilingi 108,800 hadi 370,000 na walimu wenye Shahada ya kwanza kutoka shilingi 140,000 hadi shilingi 532,000 kwa mwezi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mishahara ya walimu imekuwa ikipandishwa kila mwaka sambamba na ile ya Watumishi wengine Wizara imeona, hakuna umuhimu wa kufanya tathimini ya madhara ya kutopandisha mishahara ya Walimu peke yake.

**MHE. MCHUNGAJI JACKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ambayo Waziri amejibu nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza kwa kuwa migogoro hii ya mishahra ya walimu imekuwa ikiendelea mwaka hadi mwaka na inaonekana kuwa ufumbuzi bado haupatikani. Je, ni lini au Serikali inatamka nini kukomesha hali hiyo ambayo inajitokeza mara nyingi?

La pili, je migomo hii ya walimu ambayo imejitokeza siku za hivi karibuni haijaleta madhara yoyote kwa wanafunzi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, mimi ningependa kutoa taarifa kuwa tunaangalia mishahara na motisha kwa wafanyakazi wote bila kubagua

mfanyakazi yoyote kwa sababu kila mfanyakazi ana umuhimu wake.

Ninaomba Waheshimiwa Wabunge wawe na subira tunaiangalia mishahara ya Watumishi wote kwa ujumla baada ya kuanzisha Bodi ya Mishahara kwa hiyo tutaangalia motisha, mazingira magumu na mishahara ya wafanyakazi wote kwa ujumla.

Kuhusu athari za migomo kukiwa na mgomo wowote lazima kutakuwa athari. Kwa hiyo, athari zipo lakini niwaombe Waheshimiwa Wabunge kuwa wafanyakazi wote wanastahili posho, motisha na mishahara.

Wafanyakazi wa kada fulani wanapogoma siyo vyema na siyo busara ni vizuri tukaenda kwenye meza ya mazungumzo, tukazungumza na tukakubaliana na hata katika mgomo huu wa walimu katika mazungumzo tulizungumza nao, tulikaa nao na tulikubaliana kima cha chini. Lakini baada ya hapo wenzetu waligoma mimi ningependelea zaidi tuwe kwenye meza ya mazungumzo ili tuangalie mishahara ya wafanyakazi wote kwa ujumla bila kubagua kada ya aina fulani.

**MHE. PAULINe P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kufahamu pamoja na jitihada nzuri za Serikali kulipa madai ya walimu ikiwemo malimbikizo ambayo siyo mshahara bilioni 22 na Serikali imelipa bilioni 17 lakini yale malimbikizo ambayo yanahusu mishahara bilioni 29 Serikali hadi sasa imelipa bilioni 23 bado takribani bilioni 6. Ninapenda kufahamu ni lini Serikali itamalizia kulipa hayo malimbikizo ya walimu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimetoa taarifa hapa Bungeni ya malipo hayo na nikasema kuwa malipo haya ya mishahara yanalipwa moja kwa moja na Hazina.

Hazina iko mbioni kuyakamilisha, tulitegemea Hazina wangekamilisha tarehe 30 Juni, 2012 lakini kutokana na matatizo mbalimbali hicho kima kidogo kilichobaki wanahangaika kuweza kukimalizia kulipa tutegemee kuwa siyo muda mrefu kuanzia sasa malipo haya yatakuwa yamekamilika.

**MHE. DKT. PUDENSIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kufahamu kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amejibu kuwa Bodi ya Mishahara tayari imekwisha undwa. Nilitaka kufahamu ni lini Bodi hiyo itaanza kufanya kazi ili watumishi wote waweze kurekebishiwa mishahara kama walivyofanyiwa madaktari?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi hii imeshaundwa toka tarehe 1 Julai, 2012 na imeshaanza kazi.

Na. 385

**Mradi wa Umeme Segese - Msalala**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Tangu mwaka 2006 Serikali iliahidi kupeleka umeme vijiji vya Lunguya, Shilela na Segese, Jimboni Msalala kama

utekelezaji wa mradi wa kupeleka umeme Wilaya ya Bukombe:-

Je, ni lini mradi huo utaanza kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELLE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige Mbunge, wa Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya Serikali ya kupeleka umeme vijiji vya Lunguya, Shilela na Segese ipo palepale. Vijiji hivi vinatarajiwa kupatiwa umeme kupiti mradi wa *Electricity V* unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB).* Zabuni kwa ajili ya kupata wakandarasi wa ujenzi wa mradi imetangazwa tangu tarehe 7 Mei, 2012 na mwisho wa kurudisha kabrasha za zabuni ilikuwa tarehe 9 Julai, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, zabuni zinafanyiwa uchambuzi na hatimaye kupata wakandarasi wa ujenzi wa mradi huu. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza Desemba, 2012 na utagharimu kiasi cha dola za Marekani 10,328,228.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine yatakayo faidika na mradi huu ni pamoja na Ushirombo, Ikinda, Mlale, Bwelwa (Mbogwe) Nanda, Itunga *Primary School* Itrug, Bukombe, Lubeho, Masumbwe, Mzambaraoni, *Cagry Ginnery,* Kagwe, *Nipha Ginnery,* Bintubili A, Bintubili B, Lugunga, Kakumbi na Lunzewe.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri anayofanya na majibu mazuri aliyonipatia kwa niaba ya wananchi wa eneo hilo. Nilikuwa nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza kwa kuwa mradi huu umechelewa sana kwa sababu ni ahadi ilibidi kuwa umetekelezwa kwenye awamu ya 3 ambapo kulikuwa na mpango wa kupeleka umeme kwenye Wilaya zote mpya na Bukombe ilikuwa ni moja wapo na hivi sasa ni karibia miaka 7 toka ahadi hiyo imetolewa.

Je, Serikali inaonaje ikiwa na wakandarasi angalau wawili au watatu ili *scope* ya utekelezaji iwe fupi yaani badala ya kutumia miezi 18 kwa eneo lote kwa mkandarasi mmoja angalau kukawa na wakandarasi wawili.

Swali la pili, kwa kuwa utekelezaji wa miradi hii ya umeme mara nyingi imekuwa haifiki kwenye maeneo ya taasisi na kwenye eneo hilo kuna kama vile shule za Sekondari za Lunguya, shule ya Sekondari ya Nyikoboko, shule ya Sekondari ya Mwalimu Nyerere.

Lakini pia kuna kituo cha afya cha Lunguya pamoja na Zahanati kadhaa, mara kadhaa katika utekelezaji wa miradi taasisi hizi zimekuwa hazipatiwi umeme.

Je, Serikali inaweza ikatuhakikishia kuwa katika utekelezaji wa mradi huu itazingatiwa taasisi hizi kupatiwa umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunapokea pongezi tunashukuru. Pili, amesema mradi umechelewa ameshauri kwamba tuangalie uwezekano wa kutumia wakandarasi wawili kwa kuwa zabuni ilipokuwa imetangazwa mara ya kwanza ilikuwa inahitaji mkandarasi mmoja, basi tutaangalia kiufundi na masharti ya zabuni ili kuona kama tunaweza tukaongeza mtu mwingine katika kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili amezungumzia taasisi, tulielekeza mwanzoni kwamba ramani ya mradi ule kwanza mradi ule tunautolea eneo la Bulyankhulu karibu na mgodi wa Barick, tulielekeza laini za mradi huu zipite kwenye vijiji au *centers* ili ziweze kupatiwa huduma ya umeme. Kwa kuwa, tumepokea ushauri wa Wabunge wengi wakilalamika kwamba miradi mingi ya umeme inapita kwenye vijiji au *centres* na vinaachwa bila umeme na nguzo zile zinapita.

Kwa hiyo, Wizara tumeelekeza *TANESCO* kuangalia miradi yote inayopita katika vijiji ili tuangalie uwezekano wa kuweka umeme katika maeneo yenye *centres* ambazo zinahitaji kupewa huduma ya umeme. Kwa kufanya hivyo pia kama Wizara tumeagiza *transfoma* kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa miradi kama hiyo ya kuunganisha umeme katika *centers* au shule na sehemu ambazo zinahitaji umeme ambako miradi inapita.

Na. 386

**Kupanuliwa kwa Uwanja wa Ndege wa Mwanza.**

**MHE. RICHARD M. NDASSA** aliuliza:-

Uwanja wa Ndege wa Mwanza *(Mwanza Airport)* ni lango la kuingilia na kutokea kwa nchi za Rwanda, Burundi, *DRC,* Kenya, Uganda na Zinginezo:-

Je, ni lini hasa uwanja huo utaanza kupanuliwa?

**WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa maelezo mafupi kabla ya kujibu swlai la Mheshimiwa Rchard Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* imekuwa na mpango wa kuendeleza viwanja vya Ndege katika maeneo mbalimbali ya nchi kulingana na uhitaji uliopo na pia upatikanaji wa fedha. *TAA* inaendelea na mipango ya kupanua miundombinu na vitendea kazi ili kukidhi mahitaji ya abiria na ndege yanayoongezeka kila siku katika Kiwanja cha Mwanza.

Mfano katika mwaka wa Fedha 2007/2008 *TAA* ilifanya ukarabati na upanuzi wa eneo la kuegesha ndege za abiria kwa kiwango cha lami. Eneo hilo sasa linaweza kuegesha ndege tano kubwa aina ya *Boeing 737.*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kulifahamisha pia Bunge lako Tukufu kuwa, kuanzia mwezi Julai mwaka jana 2011, kiwanja cha ndege cha Mwanza kinatoa huduma za usafiri wa anga kwa masaa 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi napenda sasa kumjibu Mheshimiwa Ndassa kuwa mipango iliyopo sasa kwa kiwanja cha ndege cha Mwanza ni pamoja na kujenga jengo la abiria lenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni moja kwa mwaka, kurefusha urefu wa barabara ya kuruka na kutua ndege kwa mita mia tano, ujenzi wa jengo la kuongozea ndege, ujenzi wa jengo la mizigo na maegesho ya ndege na magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TAA* imeshampata mkandarasi wa kufanyakazi hizo za upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mwanza ambaye ni kampuni ya *Beijing Construction Engineering Group* kutoka China, kwa gharama ya Shilingi 105,943,140,184.20. Mkataba wa kazi hizo ulisainiwa Juni, 2012 na kazi zinaanza rasmi mwezi Oktoba, 2012 na zinatarajiwa kukamilika Septemba, 2014.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Kwanza naomba niipongeze sana Serikali kwa angalau kuanza na kutenga kiasi hiki. Lakini swali langu ninataka kujua kwamba pesa za ndani ni shilingi ngapi na pesa za nje ni shilingi ngapi na je, zitapatikana kwa wakati?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimshukuru kwa pongezi alizotoa kwa Serikali kwa kuanza upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Mwanza. Lakini pia nataka kumhakikishia kwamba katika

hizo shilingi bilioni 105. Serikali inatoa kiasi kikubwa zaidi kuliko *Development Partners* ambao watagharamia kiasi cha bilioni 20 tu. Kwa hiyo sehemu yote hii italipwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyokumbuka katika Bajeti yetu nilieleza kwamba kwa kweli tumetenga na ninyi wenyewe mmepitisha safari hii kiasi cha shilingi bilioni kumi na nane kuanzia hiyo kazi.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika uwanja wa ndege wa Mwanza ni muhimu sana kwa ajili ya ukuzaji wa utalii na tunafahamu kwamba sasa hivi tunahitaji watalii wengi zaidi ili tuweze kupata mapato mengi ya kigeni. Kuna juhudi ambazo zinafanywa ili uwanja wa ndege wa Mwanza utangazwe kuwa uwanja ndege wa kimataifa wa *Serengeti International Airport* Mwanza.

Je, Serikali iko tayari kushirikiana na wadau wa sekta ya Utalii na wananchi wa Mwanza ikiwemo Wabunge wa Mwanza na wananchi wa Kanda ya Magharibi na Kanda ya Ziwa, kuhakikisha kwamba uwanja wa ndege wa Mwanza unatangazwa kuwa uwanja wa ndege wa Kimataifa wa *Serengeti International Airport* ili kukuza utalii?

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa uwanja wa ndege wa Mwanza unatambuliwa kabisa na Serikali na ndiyo maana hata baada ya kukosa pesa ya kutosha kutoka kwa *Development Partners* Serikali ikasema ngoja sisi wenyewe tujibane tuweze kuujenga huo uwanja wa ndege na ndiyo maana sehemu kubwa ya pesa itatoka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uwanja wa ndege wa Mwanza kuwa uwanja wa kimataifa hilo ni suala rahisi sana, inategemea na sisi wenyewe ukamalishaji wa upanuzi wa uwanja huo, ili ukidhi viwango vya kimataifa, na mimi nitakuwa mtu kwanza kuunga mkono hilo suala kwa sababu uwanja wa ndege wa Mwanza kuwa uwanja wa kimataifa ni suala ambalo ni kuvutia watalii katika nchi yetu.

Na. 387

**Kujenga Maeneo Rasmi ya Kufanya Biashara Maeneo ya Mipakani.**

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA** aliuliza:-

Serikali inafanya jitihada kubwa kujenga barabara kwa lami nchini ikiwemo barabara ya Tanga – Horohoro:-

(a) Je, sanjari na ujenzi huo, Serikali ina mpango gani wa kujenga maeneo rasmi ya kufanyia biashara kwa wananchi walioko maeneo ya mipakani kama Horohoro ili kuepusha hatari ya kugongwa na magari kwa kufanyia biashara barabarani?

(b) Je, Serikali iko tayari kuharakisha ujenzi wa maeneo hayo ii kuondokana na aibu ya wananchi walioko mipakani ambao ndiyo kioo cha taswira ya nchi kufanya biashara barabarani?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dustan Luka Kitandula, Mbunge wa Jimbo la Mkinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika eneo la mpaka wa Horohoro, hufanyika biashara mbalimbali ambazo huwahusisha wadau kutoka Tanzania na wengine kutoka nchi jirani ya Kenya. Ili kuendeleza miundombinu ya masoko katika eneo la mpakani, Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, imechukua hatua kwa kuwatengea wananchi wa eneo hilo ekari 5.6 kwa ajili ya ujenzi wa soko la mazao na bidhaa mbalimbali karibu na mpaka wa Horohoro.Aidha, Halmashauri imeweza kutenga eneo la hekta 6.8 kwa ajili ya ujenzi wa mnada wa mifugo ambao kwa sasa umekamilika na unafanya kazi vizuri.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuharakisha ujenzi wa soko la mazao na bidhaa mbalimbali katika eneo hilo, Wizara itaendelea kushauri Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga kutenga fedha kwenye Bajeti kwa ajili ya ujenzi wa soko hili, ikiwa ni pamoja na kutafuta vyanzo vingine vya fedha kwa kushirikiana na sekta binafsi kupitia mpango wa *PPP.*

Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Halmashauri kwa kutoa ushauri wa kitaalam pale utakapohitajika.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Ujenzi wa masoko ya kimataifa ni gharama kubwa, Serikali kwa kulitambua hili imekuwa ikishirikiana na Halmashauri kadhaa kubeba mzigo wa ujenzi ili kufanikisha azma hii kama ilivyofanya kule Himo. Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Mkinga katika kufanikisha jambo hili?

(b) Wakati tunapofanya mchakato wa upembuzi yakinifu, miundombinu muhimu kama masoko, stendi na sehemu za wananchi kujisaidia yamekuwa yakiachwa kando na hivyo kuleta mzigo mkubwa na usumbufu kwa wananchi. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kujumuisha miundombinu hii muhimu katika upembuzi yakinifu wa barabara zetu?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ujenzi wa masoko haya ambayo tunayazungumzia ni kweli ni wa bei kubwa sana kama tulivyozungumza naye na kama ambavyo inafahamika katika maeneo ambayo masoko haya tayari yamejengwa.

Soko hili ambalo linatarajiwa kujengwa eneo la Horohoro litagharimu takribani shilingi milioni mia saba. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi tayari Serikali inashirikiana na Halmashauri ya Mkinga, inashirikiana na Mkoa wa Tanga na tayari andiko hilo limekamilika na litapelekwa kuombea fedha *IFAD* ili waweze kusaidiwa katika soko hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni dhahiri kwamba upembuzi yakinifu katika barabara zetu huko nyuma ulisahau hili suala la umuhimu katika safari za watu na mali zao. Serikali katika mipango mipya sasa tumelichukua na tutahakikisha kwamba kwa kadri itakavyowezekana mahali ambapo wananchi watasimama, watajisaidia na mambo mengine vitapewa kipaumbele katika mipango endelevu ya barabara zetu.

Na. 388

**Hali ya Uchumi wa Taifa baada ya Miaka 50 ya Uhuru.**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Mwaka 2011 Serikali ya Jamhuri ya Tanzania, ilitimiza miaka 50 tangu kupata Uhuru. Je, Serikali inawaambia nini Watanzania juu ya kuyumba kwa uchumi wa nchi, ongezeko la bei na kuongezeka kwa umasikini kwa watu wa hali ya chini?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka 50 iliyopita Tanzania kama Taifa imekuwa katika harakati za kutekeza mipango mbalimbali ya kimkakati ili kuinua maisha ya wananchi hususani kiuchumi na kijamii. Katika utekelezaji wa mipango hiyo, Taifa limepata mafanikio makubwa na pia limekumbana na chanmgamoto mbalimbali.

Mheshimiwa naibu Spika, baadhi ya mafanikio tuliyoyapata katika kipindi cha miaka kumi ya mwanzo baada ya uhuru yalidumazwa na changamoto na majanga mbalimbali yaliyoikumba Taifa na Dunia kwa ujumla.

Baadhi ya majanga haya ni pamoja na kupanda kwa ghafla bei ya mafuta katika soko la Dunia kati ya mwaka 1973 na 1979, kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977, Vita kati ya Tanzania na Uganda mwaka 1978/1979. Ukame wa mara kwa mara, mdororo wa uchumi duniani katika vipindi tofauti na changamoto za kuingia kwenye mfumo wa soko na uchumi huria uliotokea miaka ya 1980s na 1990s.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari za mdororo wa uchumi zilizotokea Duniani zimeiathiri nchi katika Nyanja mbalimbali zikiwemo za uzalishaji na upatikanaji mdogo wa chakula na kuongezeka kwa bei ya mafuta katika soko la Dunia. Madhara haya yamesababisha mfumuko wa bei na umasikini kupungua kwa kiasi kidogo hususani katika maeneo ya vijijini.

Chini ya malengo ya kimataifa ya kimaendeleo ya millennia ilitegemewa kwamba ili Tanzania iweze kupunguza umaskini kwa asilimia 50 ifikapo mwaka 2015, ilitakiwa uchumiwa nchi yetu ukue kwa kiwango kisichopungua asilimia nane kwa muda wa miaka ishirini mfululizo. Ukuaji wa pato la Taifa kwa wastani wa asilimia saba kwa kipindi kifupi hautaweza kupunguza umaskini kama ilivyoainishwa kwenye malengo ya millennia.

Sekta ya kilimo ambayo inaajiri watu wengi inakua kwa wastani wa asilimia 4 tu, kiwango hiki ni kidogo ukilinganisha na malengo ya kimataifa ya maendeleo ya Milenia. Mikakati na mipango inayotekelezwa na Serikali kama vile MKUKUTA na MKUZA, mpango wa maendeleo wa miaka mitano, Kilimo Kwanza, *SACGOT* ni baadhi ya hatua na mikakati stahiki zinazolenga kuinua uchumi hususani Kilimo na kupunguza umaskini nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nabu Spika, ningependa kuongeza kusema kuwa, Serikali ya Tanzania kwa kipindi chote cha miaka 50 imekuwa ikifanya juhudi kuhakikisha kuwa, wananchi wake wanaboreshewa maisha yao kwa kutumia mikakati mbalimbali na kila mara kujifanyia tathmini ambazo zimewawezesha kuangalia ni jinsi gani wataendelea kuboresha maisha ya wananchi, kijamii, kiuchumi hata kisiasa ili kuhakikisha kuwa maendeleo yanapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hiyo ndiyo jibu ambalo naweza kuwapa wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Naibu Waziri wa Fedha kwa majibu yake. Aidha naishukuru sana Serikali kwa kuwa kwa mara ya kwanza imekiri kwenye majibu yake kwamba kwa pato la Taifa haiwezi kupunguza umaskini kama ilivyoainishwa katika malengo ya millenia.

(a) Je, kwa nini wanaendelea kuwahadaa Watanzania kwa kuwaambia kwamba ifikapo mwaka 2015 asilimia 50 ya Watanzania watakuwa wamevuka katika kiwango cha umaskini?

(b) Kwa kuwa, wamekiri wenyewe kwanini haioni sasa ni wakati muafaka wa Chama cha Mapinduzi (CCM) kuwapisha Chama kingine ili wananchi tunaoweza kufanyakazi tuweze kuwaondolea umaskini Watanzania? (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kuwa tumetambua kwamba kwa jinsi tunavyoendelea sasa hatutaweza kufikia malengo ina maana kuwa tumeanza kuyafanyia kazi mapungufu hayo.

Sasa hivi tuna mikakati ya maendeleo ambayo tumeipanga na ambayo itahakikisha kuwa tuna harakisha ukuaji wa maendeleo yetu kufuatana na jinsi ambavyo tumejiwekea malengo. Tuna mikakati mbalimbali ambayo sasa hivi kila Wizara itahakikisha kuwa inaongeza ufanisi wake kwa kujiwekea vipaumbele vichache na kuhakikisha kuwa tunavizingatia hivyo katika kuweka Bajeti katika kuweka mipango ya maendeleo katika ufanisi na uadilifu wa kuhakikisha tuna-*deliver* kufuatana na malengo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapojikuta umefanya kitu na hakikuenda vile ulivyotegemea suala siyo kukimbia, suala ni kukaa na kulikabili tatizo ambalo liko mbele yako. Hivyo ndivyo Chama cha Mapinduzi kimedhamiria kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kubadilisha hilo litakuwa ni jukumu la wananchi wakati muafaka utakapofika. (*Makofi*)

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Kwa kuwa, sababu moja kubwa ambayo imewafanya wananchi wetu waendelee kuwa na umaskini mkubwa ni mfumuko wa bei ambao sehemu kubwa inatokana na chakula. Lakini vile vile ni asilimia 20 tu ya Watanzania wanaotumia mifumo ya kuweka fedha benki, asilimia 80 ya fedha zipo ndani ya mifuko ya watu.

Je, Serikali haioni kwamba kwa kutumia utaratibu wa kutumia Benki Kuu kuratibu mfumuko wa bei kwa kutumia fedha ambapo ni asilimia 20 tu ya watu wanaoweka fedha benki na asilimia 80 hawaweki haiwezi kusaidia kupunguza mfumuko wa bei, badala yake waweze kutumia utaratibu wa kuzalisha chakula zaidi kuwaongezea watu uwezo wa kuzalisha zaidi badala ya kutumia *currency* na kuongeza umaskini zaidi? (Makofi)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na Mheshimiwa Hamad Rashid. Anataka kujua kwa nini mfumuko wa bei uko namna hii na kwa nini tusichukue hatua za kuteremsha kwa kutumia utaratibu wa Sera yaani za *physical policy* badala ya Sera za Fedha yaani *monetary policy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumuko wa bei una sababu zake na lazima tutumie sababu zinazosababisha mfumuko wa bei kutokea kabla hatujasema tutumie aina hii ya Sera ni lazima tunachambua kwanza.

Sasa baada ya kuchambua, tumeona kweli katika kundi la chakula ndilo linalosababisha asilimia kubwa kusababisha mfumuko wa bei ambao umechangia kwa

asilimia 24.7 na ndiyo maana tumekuja na maamuzi ya Kisera kukabiliana na mfumuko wa bei unaosababishwa na kundi la chakula. Kwa hivi hapa tuko katika upande wa *physical policy*. Anayoipendekeza yeye sio Sera ya Fedha yaani *monitory policy* kwa hivyo tuko pamoja, analolipendekeza yeye ndilo hatua tulilochukua.

Lakini la pili, anasema kwa nini tusieneze huduma za fedha mpaka huko Vijijini ndiyo Sera ambayo tutakuja nayo na katika hotuba yangu ya baadae tutaeleza kwa kirefu tunataka kufanya nini ili huduma ya fedha ifike mpaka Vijijini ambako italeta *impact* kwa ajili ya msukumo wa maendeleo ya wananchi.

Na. 389

**Ujenzi wa Chuo cha Wauguzi- Rungwe**

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE** aliuliza:-

Uongozi wa KKKT Rungwe umedhamiria kujengea Chuo cha Wauguzi katika hospitali ya Itete ili kupunguza uhaba wa wauguzi katika hospitali na vituo vya afya mbalimbali nchini.

Je, Serikali itasaidiaje ili dhamira hiyo itekelezeke?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru na kupongeza Uongozi wa KKKT Rungwe kwa dhamira yao nzuri ya kujenga Chuo cha Wauguzi ili kupunguza uhaba wa wauguzi katika hospitali na vituo vya afya mbalimbali hapa nchini.

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inakitaka chuo kufuata miongozo inayohusu taratibu za kuanzisha vyuo vya Uuguzi na Mitaala ya kufundishia iliyoainishwa. Aidha, pale itakapowezekana Wizara itaweza kuwapatia walimu kwa mfumo wa kuazimwa na kutoa ruzuku kwa chuo kwa kila mwanafunzi atakayedahiliwa chuoni hadi kuhitimu. Wizara pia husaidia uendeshaji na usimamizi wa mitihani ya kuhitimu.

Walimu na wafanyakazi katika vyuo binafsi hupewa fursa za mafunzo ya kujiendeleza na kushiriki kwenye warsha na mikutano ya kitaaluma na uendeshaji wa vyuo inayoendeshwa na Wizara ya Afya na Ustawii wa Jamii. Hivi ndivyo itakavyokuwa kwa chuo hicho kinachokusudia kujengwa.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika,ahsante sana. Nina swali moja tu la nyongeza:-

Kwa kuwa hospitali ya misheni Itete iko umbali wa zaidi ya kilomita 50 kutoka hospitali ya wilaya ya Rungwe. Je, Serikali itakuwa tayari kuisaidia hospitali hii ili iweze kupata wataalamu wa kutosha kuiandaa hospitali hii kuwa hospitali teule kuwasaidia wananchi wa Halmashauri mpya ya Busokero ambayo itaanzishwa hivi karibuni?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hilda Ngoye, kama ifuatavyo:-

Suala la kupeleka wataalamu, hili ni suala la Kitaifa katika vituo vyote vya kutolea huduma hapa nchini. Lakini kama nilivyosema kutokana na ukweli kwamba kituo hiki bado ni mali ya KKKT- Rungwe na kusudio ni kwamba kwenye Halmashauri mpya kukifanya kituo hicho kiwe *DDH* au hospitali teule.

Mimi nimwombe Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Waheshimiwa kwenye Baraza hilo la Madiwani kule kukamilisha taratibu za kuitaka na kufanya makubaliano na hospitali hiyo ili hospitali hiyo iwe teule na kuwasilisha maombi hayo kwenye Serikali na baadaye Serikali itafanya maamuzi.

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya amesema kutambua vyuo binafsi ambavyo vinachangia katika kuzalisha wataalamu.

Je, Wizara inao mpango gani wa kuangalia vyuo binafsi vinavyoanzishwa chini ya mwanvuli wa vitu vingine lakini haviendeshi mafunzo kwa kufuata mitala ya Wizara ya Afya. Mfano Chuo cha Wauguzi Wasaidizi KOMASWA, Magu. Anayo hiyo taarifa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na

Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa, kama ifuatavyo:-

Kwanza vyuo vinakubalika na Wizara ya Afya pale ambapo itakuwa imekamilisha kufuata mwongozo wa uendeshaji wa vyuo na kupata ithibati kutoka *NACTE.* Pale itakapo kuwa inathibitisha chuo hicho kutofuata miongozo ya Wizara ya Afya iliyoainishwa na kutokuwa na ithibati ya *NACTE,* chuo hicho kinakuwa hakina stahili ya kutoa taaluma inayokusudia au inayotoa.

Sasa kwa hakika siwezi kujibu kwamba nina taarifa kwa sababu sina taarifa ya hicho chuo unachokizungumzia cha wauguzi wasaidizi, kimsingi naweza nikafuatilia ili pale nitakapokuwa nimethibitisha kwamba chuo hicho kinaendeshwa kinyume na miongozo ya Wizara ya Afya na vile vile hakijapata ithibati ya NACTE, basi hatua stahili tunaweza tukazichukua. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umeisha kabisa na maswali yameisha. Leo tuna wageni wengi sana kwenye gallery kwa hiyo tuvumiliane Waheshimiwa Wabunge. Niwatambue kama ifuatavyo; wageni kutoka Wizara ya Fedha ni Katibu Mkuu Hazina, Ndugu Ramadhani Kija, naomba usimame, ahsante sana Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Hazina, Dkt. Selvasias Likwelile, karibu sana, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Elizabeth Nyambibo, *Governor* wa *BOT,* Beno Ndulu, karibu sana Governor, Mkuu wa *TRA*, Ndugu Harry Kitilya ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, wako pia Makamishina, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, Vitengo, Taasisi zilizopo chini

ya Wizara ya Fedha, lakini vile vile wako wageni wanane wa Mheshimiwa Janeth Mbene, Naibu Waziri wa Fedha ambao ni watoto wake, wameandika vibaya haiwezekani, hawa vijana wangu wa Bunge wawe wanaandika vizuri haya matangazo. Ni wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha, Mheshimiwa Janeth Mbene ambao ni watoto wake Ndugu Steven na mke wake, Modesta na rafiki yake, Brenda na mume wake, Francis na mkewe, karibuni sana, ndiyo watoto wake kwa sababu ni watoto wake na wake zao nao ni watoto wake pia.

Waheshimiwa Wabunge wako wageni saba kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali wakiongozwa na Ndugu Pius Athanas, Mkaguzi Mkuu Msaidizi, ahsanteni sana, hawa wanatoka Ofisi ya CAG, karibuni sana. Wageni walioko kwa ajili ya mafunzo ni watoto 110 wa Utoto Mtakatifu wa Yesu kutoka Jimbo Katoliki la Tanga, wameambatana na Masista 3 na Mapadri 2 Dodoma kwa ajili ya kongamano la Kitaifa la Utoto Mtakatifu wa Yesu Kanisa Katoliki Tanzania, msimame pale mlipo, ahsante sana watoto, karibuni sana Dodoma, karibuni sana Bungeni.

Wako watoto 20 kutoka shule ya Msingi Kaloleni, Morogoro, walimu wa Kaloleni, ahsanteni sana pale mlipo, karibuni sana walimu kutoka shule ya msingi Kaloreni. Wanafunzi 16 kutoka shule ya msingi Chinangali, Manyoni ambao ni Wabunge wa Bunge la toto wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Majiri, Mheshimiwa Sakawa. Pia wameambatana na Mwalimu Mkuu, Ndugu Shomi na Spika wa Bunge la watoto Ndugu Amina Masimba. Watoto kutoka Manyoni wako wapi? Ahsanteni sana. Haya asimame Spika, Amina Masimba kutoka Manyoni, Spika

yuko wapi? Hongera sana. Asimame Naibu Spika, yuko wapi Naibu Spika? Ninyi watoto, aaah! Ahsante sana. (*Makofi/Kicheko*)

Wasimame wanafunzi 72 pamoja na walimu wao kutoka Shule ya Msingi ya Martin Luther, Dodoma. Karibuni sana watoto na walimu wa Martin Luther Bungeni kwenu hapa, Waheshimiwa Wabunge hii ni moja ya shule bora kabisa katika Mkoa wa Dodoma na ni katika shule bora Tanzania. Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 4 wa Mheshimiwa Israel Yohana Natse, mbunge wa Karatu wakiongozwa na mke wake, Mama Wilshermina Natse, pale walipo, wako pale karibuni sana Wageni wa Mchungaji Natse. Wako pia wageni 4 wa Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa na Mheshimiwa Hilda Ngoye ambao ni wajukuu wao wakiongozwa na Mkunde Ngodo, wako wapi? Karibuni sana pale mlipo. Wageni 22 wa Mheshimiwa Angellah Kairuki, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria ambao ni washiriki na wawezeshaji wa programu ya mafunzo ya siasa na uwongozi kwa wanawake Kanda ya Dodoma kutoka Hans Seidel Foundation, ahsante sana wageni wetu kutoka *Hans Foundation,* karibuni sana.

Wageni wa Mheshimiwa Devota Likokola ni waratibu 17 wa Vikoba Mikoa ya Njombe, Iringa, Mbeya na Ruvuma na viongozi 2 wa TAMFI ambao ni Bwana Atemias Milinga na Obadia Kahaya, wageni wa Vikoba karibuni sana. Wageni wa Mheshimiwa Goodluck Ole- Medeye, Naibu Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi ni Ndugu Christopher Kilaya, Katibu wa CCM Uchumi na Fedha Wilaya ya Muleba, Kilaja karibu sana Katibu wa Uchumi na Fedha CCM Wilaya ya Muleba, sijui vyama vingine vina Makatibu wa aina hii? Hiki chama kweli imara hiki. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa nawaletea Waheshimiwa Wabunge tusikilizane naona kelele zinazidi, tusikilazane vizuri. Sasa nawaletea wageni wa Mheshimiwa Mwigulu Lameck Mchemba ambao ni Ma-*Sheikh* na Ma- *Imam* kutoka Wilaya ya Iramba na hasa Jimbo la Iramba Magharibi wakiongozwa na *Sheikh* Omar Hassan Rukubwe, wale Ma- *Sheikh* naomba wasimame pale walipo, wako hapa, Ma- *Sheikh* hawa ni 69. Sitini na tisa (69) haijapata kutokea, karibuni sana Ma-*Sheikh*, Mbunge wenu anafanya kazi nzuri sana hapa Bungeni.

**MBUNGE FULANI:** *Takbirih*!!!

**MA-SHEIKH:** *Allwah Akbar!!!!*

**NAIBU SPIKA:** Kuna watu wanamwonea kijicho, tunaomba muendelee kumuwekea Dua. (*Makofi/Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** *Takbirih*!!!

**MA- SHEIKH:** *Allwah Akbar!!!*

**NAIBU SPIKA**: Kuna mgeni wa Mheshimiwa Mbunge Selemani Nchambis, Ndugu Taison kutoka Manispaa ya Shinyanga pale alipo karibu sana. Kuna wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Nishati na Madini, Mheshimiwa Masele, Mkurugenzi wa Manispaa ya Shinyanga Festo King'ombe, David Kyando na Hassan Ibrahim pale walipo karibuni sana.

Baada ya matangazo haya ya wageni sasa niwaletee matangazo ya vikao vya kazi. Ndugu Vita Kawawa, Katibu

Mkuu *APNAC* anaomba Kamati ya Utendaji ya *APNAC* ikutane saa saba mchana leo katika moja ya kumbi za ukumbi wa Msekwa pale mkutane pale Kamati ya Utendaji. Mheshimiwa Silinde, katibu wa Wabunge wa CHADEMA anawaomba Wabunge wa Kambi hiyo wakutane saa saba na robo Ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. CHADEMA saa saba na robo kwenye Ofisi ya Bosi wenu kule. Mahamud Mgimwa, Mwenyekiti Kamati ya Viwanda na Biashara anawaomba Wajumbe wa Kamati ya Viwanda na Biashara sasa saba na robo ukumbi mmoja wapo wa Pius Msekwa, mtajipanga huko maana yake matangazo mengi yanaonyesha kuna Kamati mbalimbali zinakutana Msekwa.

Mheshimiwa Edward Lowassa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama anaomba Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama saa saba na robo kikao cha Kamati Ukumbi 219 gorofa ya pili jengo la utawala. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo ya Hesabu za Serikali za Mitaa *LAAC* kwamba mkutano saa saba na robo, ukumbi namba 227.

Mheshimiwa Missanga na hili tangazo limetoka kwa Mheshimiwa Selemani Jafo, anawatangazia Waislamu wote waliofunga kwamba kile kikao kilichokuwa kifanyike jana ambacho hakikufanyika kutokana na kuingiliana kwa ratiba sasa kitafanyika leo saa saba na robo mchana baada ya kipindi cha Bunge katika Ukumbi wa Msekwa.

Waislamu waliofunga Waheshimiwa Wabunge saa saba na robo Ukumbi wa Msekwa.Tangazo hili limeletwa na

Mheshimiwa Selemani Jafo nadhani ni Katibu na Mheshimiwa Misanga ambaye nadhani ni Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kuna wageni, nadhani watakuwa ni wa Mheshimiwa Zambi, Ndugu Malick Nzowa, Mjumbe wa Halmashauri Kuu *CCM* Mkoa na ndugu Thadeo Zambi, kutoka Kata ya *CCM* Vwawa. Karibuni sana pale mlipo, karibuni sana sana sana.

Mheshimiwa Missanga, pia anawaomba Waheshimiwa Wabunge, waliofunga na wasiofunga, pamoja na Watumishi wa Bunge, waliofunga kuwa, wanaalikwa Futari leo siku ya Jumatano tarehe 15 Agosti, 2012 Saa 12.30 jioni, katika Ukumbi wa *Basement,* kwa hisani ya Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – *TAMISEMI.* Leo saa 12.30 Waheshimiwa waliofunga na wasiofunga, pamoja na Watumishi wa Ofisi ya Bunge waliofunga, *Basement.* Futari hiyo, imeandaliwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – *TAMISEMI.* Mheshimiwa Hawa Ghasia, kuna Waheshimiwa Wabunge, wameniandikia hapa wanaomba na mgao wa kanzu. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna tangazo limetoka kwa Mheshimiwa Magdalena Sakaya na vile vile Kaimu *DAP,* Mama Kipa, anatufahamisha kwamba, niwatangazie Waheshimiwa Wabunge, kwamba, Mheshimiwa Riziki Omar, ambaye huwa anakaa hapa kushoto kwangu, wa Kambi ya *CUF,* amefiwa na mtoto wake usiku wa kuamkia leo tarehe 15 Agosti, 2012 huko Pemba. Ni mtoto wake wa kiume, ambaye alikuwa akiitwa Masoud Hamad Abdallah. Kwa hiyo, Mheshimiwa, ameondoka alfajiri ya leo, ili aweze kuwahi mazishi kule Pemba. Mwenyezi Mungu, aiweke

roho ya Marehemu Mahali Pema Peponi. Mimi kwa niaba ya Wabunge wote, natoa pole sana, tunaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu Mahali Pema Peponi, Amin.

Matangazo yaliyo mengi yameisha, tangazo la mwisho Waheshimiwa Wabunge, hili ni la kwangu; kuna Wakuu wa Mikoa ambao kwa kweli, wanajituma sana na wanapaswa kupongezwa kipekee. Kuna Mkuu wa Mkoa wa Tabora, nadhani ni Fatma Mwasu, nadhani. Huyu mama ameweka utaratibu mzuri sana katika Mkoa wake; natumaini wengine nao wanaweza wakaiga. Ametoa maelekezo ya Mkoa wa Tabora kwamba wanaume wote kule Nzega na Bukene, wanatakiwa kuhudhuria katika Kliniki maalum, katika Hospitali ya Nzega, katika Hospitali ya Ndala, Zahanati ya Nata na Zahanati ya Mambali, wanaume wote wenye umri wa miaka 18 na kuendelea. Wanaume wa miaka 18 kurudi nyuma mpaka sifuri wanatakiwa waende na wazazi wao kwenye hiyo Kiliniki na katika Kliniki hiyo, hakuna malipo. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa kweli, huyu mama anafanya mambo makubwa sana, yanahitaji kuigwa. Kwa hiyo, natoa wito kwa wanaume wanaotakiwa kwenda huko, hebu wafanye hivyo haraka sana, katika Wilaya ya Nzega, waitikie wito wa Serikali ya Mkoa wa Tabora. Wanaitiwa nini? Watajua huko huko. *(Makofi/Kicheko)*

Matangazo yameisha, Katibu tuendelee na ratiba.

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Hatua Zilizochukuliwa Dhidi ya Wanafunzi na Walimu Waliohusika na Udanganyifu Katika Mitihani

**NAIBU SPIKA:** Naomba kumwita Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa Kauli za Mawaziri. *(Makofi)*

## MWONGOZO WA SPIKA

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Baada ya Kauli.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Naomba vijana wangu, muanze kugawa Kauli ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Waziri, endelea.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni 49 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, naomba kutoa Kauli ya Serikali, Kuhusu hatua zilizochukuliwa dhidi ya wanafunzi na Walimu, waliohusika na udanganyifu katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi na Mtihani wa Kidato cha IV, mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, udanganyifu katika mitihani ni vitendo vinavyofanywa na Watahiniwa, kwa lengo la

kupata alama za juu kuliko uwezo wao halisi. Vitendo hivyo, hufanywa ama na watahiniwa wenyewe binafsi au kwa kushirikiana na Walimu na Wasimamizi wa Mitihani.

Tatizo la udanganyifu wa mitihani linarudisha nyuma juhudi za Serikali, za kutoa elimu bora kwa wote na hivyo, Wizara yangu, imejipanga kukabiliana na tatizo hili, ili kuhakikisha matokeo ya mitihani yanatoa picha halisi ya uwezo wa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba nitoe taarifa kuhusu matukio ya udanganyifu, yaliyojitokeza katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi na Kidato cha Nne, mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi, ulifanyika mwezi Septemba, 2011. Jumla ya Watahiniwa walikuwa 983,545 walifanya mtihani na waliofaulu walikuwa 567,567 ambayo ni 58.3%. Katika mtihani huo, jumla ya Watahiniwa 9,736 ambao ni 0.98% walibainika kushiriki katika udanganyifu.

Baada ya Baraza la Mitihani la Tanzania, kugundua kuwa, kuna baadhi ya wanafunzi wamefanya udanganyifu katika mtihani huo, Serikali ilifanya uchunguzi uliolenga kubaini Walimu na Watumishi waliohusika katika udanganyifu, ili wachukuliwe hatua stahiki. Uchunguzi huo ulibaini kuwa, walioshiriki ni Walimu Wakuu 422, Walimu na Wasimamizi wa Mitihani 250 na pia Wamiliki na Mameneja wa Shule.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa dhidi ya waliohusika na udanganyifu katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi, ni pamoja na hatua zifuatazo:-

1. Kufuta matokeo ya Mitihani ya Watahiniwa 9,736 waliobainika kufanya udanyanyifu katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi.

2. Kuwavua madaraka Walimu Wakuu wa Shule 176.

3. Kuwapa onyo kali Walimu Wakuu 246 na Wasimamizi 213 wa Vyumba vya Mitihani, vilivyobainika kufanya udanganyifu na kutowahusisha tena na masuala ya mitihani ya kitaifa kwa miaka kati ya mitatu (3) hadi miaka mitano (5).

4. Kuwafikisha kwenye Vyombo vya Sheria, Wasimamizi wa Mitihani wanne (4).

5. Kutoa onyo kali kwa Wamiliki na Mameneja wa Shule Binafsi 33, ambao Shule zao zilihusika na udanganyifu katika mitihani.

6. Kuwafungulia mashitaka kwenye Tume ya Utumishi ya Walimu *(TSD)* Wasimamizi 33 wa Mitihani, waliotuhumiwa kushiriki katika udanganyifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtihani wa Kidato cha Nne ulifanyika Mwezi Oktoba, 2011 na matokeo yake yalitangazwa mwezi Februari, 2012. Matokeo hayo yalionesha kuwa, Watahiniwa 180,216 kati ya Watahiniwa 339,330 waliofanya mitihani, sawa na 53.6% walifaulu.

Watahiniwa 3,303 waliotoka katika shule 91 ambazo 75 ni shule za serikali na 16 zisizokuwa za Serikali, walibainika kujihusisha na udanganyifu. Aidha, Walimu 140 walibainika kujihusisha na udanganyifu huo, wakiwemo Wakuu wa Shule 48 na Wasimamizi wa Mitihani 92.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zilizochukuliwa dhidi ya waliofanya udanganyifu katika Mtihani wa Kidato cha IV, ni kama ifuatavyo:-

1. Jumla ya Watahiniwa 3,303 waliothibitika kushiriki katika udanganyifu wa Mtihani wa Kidato cha IV mwaka 2011, walifutiwa matokeo yao na Baraza la Mitihani la Tanzania.

2. Wanafunzi waliofutiwa matokeo ya mtihani mwaka 2011, walikuwa wamezuiliwa kufanya mtihani kwa kipindi cha miaka mitatu (3); hata hivyo kutokana na maombi ya wadau mbalimbali, adhabu hiyo ilipunguzwa na kuwa mwaka mmoja. Hivyo, wahusika wataruhusiwa kurudia Mtihani wa Kidato cha IV mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Shule za Sekondari za Serikali, hatua zilizochukuliwa dhidi ya Watendaji walioshiriki katika udanganyifu, ni hizi zifuatazo:-

1. Kuwashitaki *TSD,* Wakuu wa shule sita (6) ambao wawili kati yao wameshavuliwa madaraka.

2. Kuwapa onyo Wakuu wa Shule 11 na kuwafikisha Mahakamani Wasimamizi wa Mitihani 14.

3. Kuwapa onyo Wasimamizi wa Mitihani 68 na kusimamishwa kushiriki katika shughuli za Mitihani Wasimamizi wa Mitihani 10. Wasimamizi wa Mitihani 10, tayari wameshashitakiwa *TSD.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wamiliki wa Shule 13 za Sekondari zisizokuwa za Serikali na zilihusika na udanganyifu, wameandikiwa barua za kusudio la kuzuwia udahili wa Kidato cha I kwa kipindi cha mwaka 1 kuanzia mwaka 2013. Aidha Wamiliki hao, wameagizwa kuwachukulia hatua za kinidhamu Wakuu wa Shule na Walimu waliohusika katika udanganyifu huo, ikiwa ni pamoja na kuwavua madaraka Wakuu wa Shule na kuhakikisha kuwa hawashiriki katika shughuli za Mitihani ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuwachukulia hatua wahusika bado linaendelea kufanyika kwa mujibu wa Sheria na Taratibu za Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hatua za Kudhibiti Udanganyifu kwa Siku Zijazo. Baraza la Mitihani, liliunda Tume ya Uchunguzi ya Kufuatilia, Kuthibitisha na Kubaini mbinu zilizotumika kutekeleza udanganyifu katika Mtihani wa Kidato cha IV, mwaka 2011. Matokeo ya uchunguzi huo yamesaidia kupanga mikakati ya kudhibiti udanganyifu kwa siku zijazo. Mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:-

1. Kuzielekeza Kamati za Mitihani za Mikoa na Halmashauri, kuimarisha usimamizi wa Mitihani na kuhakikisha kuwa, mianya yote ya udanganyifu katika mitihani inaondolewa.

2. Kupunguza idadi ya wanafunzi katika Chumba cha Mtihani kutoka 30 hadi 25, kwa lengo la kupunguza msongamano unaoweza kusababisha wanafunzi kutazamiana majibu yao ya mitihani.

3. Kuimarisha usimamizi wa mtihani wa kumaliza elimu ya msingi kwa kuanzisha utaratibu wa kuwa na Msimamizi Mkuu, ambaye atakuwa ni Mwalimu Mkuu wa Sekondari.

4. Kuzielekeza Kamati za Mitihani za Mikoa na Halmashauri, kuteua mapema Walimu Waadilifu, kwa ajili ya usimamizi wa mitihani na majina yao yahakikiwe na vyombo vya usalama, kabla ya kuanza zoezi la kusimamia mitihani husika.

5. Kuzielekeza Kamati za Mikoa za Mitihani, kubaini shule zote ambazo zimekuwa zikijihusisha na udanganyifu katika mitihani na kuhakikisha wanaimarisha usimamizi na ufuatiliaji wakati wa mitihani.

6. Kuwaagiza Wamiliki wa Shule zisizo za Serikali, kuhakikisha wanazingatia taratibu za usimamizi na uendeshaji wa mitihani. Aidha, Wizara haitasita kuzifutia usajili shule zote zitakazobainika kujihusisha na vitendo vya udanganyifu katika mitihani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu, kuwa mtihani wa kumaliza elimu ya msingi utafanyika nchini kote tarehe 19 Septemba, 2012 hadi tarehe 20 Septemba, 2012. Hivyo, kupitia Bunge hili Tukufu, napenda kutoa wito kwa Maafisa Elimu wa Mikoa na wale wa Wilaya, kushirikiana na Kamati za Uendeshaji

Mitihani za Mikoa na Wilaya, kuhakikisha kuwa taratibu za uendeshaji mitihani zinazingatiwa ipasavyo.

Napenda pia kuwaasa Wasimamizi wote wa Mitihani, walimu Wakuu, Wakuu wa Shule, kuhakikisha kuwa, wanazingatia kikamilifu taratibu za usimamizi na uendeshaji wa mitihani, kwani Wizara yangu, haitasita kuchukua hatua kali kwa wote watakaobainika kufanya udanganyifu katika mitihani. Tumefanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo, mpaka tuiondoshe kadhia hii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa Kauli.

Nawaona Waheshimiwa Wawili. Tuanze na Mheshimiwa Kangi Lugola, halafu na jirani yako.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako chini ya Kanuni 68 (7). Wakati Swali Namba 382, la Mheshimiwa Moshi Kakoso, linajibiwa, linalohusu ujenzi wa Zahanati kote nchini kwenye Vijiji na ujenzi wa Vituo vya Afya kwenye Kata zote katika nchi hii, majibu ya Serikali yameendelea kuhusisha neno "Tumejipanga Vizuri."

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ahadi zilizotolewa na Mheshimiwa Rais, ambazo na zenyewe

zinahusisha maneno tumejipanga vizuri. Nilikuwa naomba Mwongozo wako, kujipanga vizuri maana yake ni nini?

Kujipanga vizuri, maana yake ni kuwepo *document* ambayo inaonesha namna ambavyo Zahanati zote kwenye Vijiji, zitakavyojengwa na Vituo Vya Afya na Utekelezaji wa Ahadi za Rais, kwa maana ya lini na wapi? Pamoja na kiwango cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninaomba Mwongozo wako, kama inaruhusiwa kuliambia Bunge, kwamba, tumejipanga vizuri, bila Bunge hilohilo, kulionesha mpango huo ambao mmejipanga vizuri. Kwa sababu, Watanzania wanaotusikiliza na kauli hizi zinazotolewa na Serikali, na hata kule kwangu Mwibara, wanaamini nikienda kule wataniuliza kwamba, Serikali, imejipanga vizuri, Kijijini Zahanati itajengwa lini? Au Kata yangu itapata Kituo cha Afya na Ahadi za Rais lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa ninaomba Mwongozo wako, kama inaruhusiwa Serikali kuliambia Bunge, tumejipanga vizuri, bila kulionesha Bunge, Mpango huo ambao wamejipanga vizuri.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi ninaomba Mwongozo wako kwa Kanuni hiyo ya 68 (7).

Mheshimiwa Naibu Spika, jana wakati Waziri wa Elimu, anatoa majumuisho ya Wizara yake, yeye alipewa dakika

40. Katika dakika 40 alizopewa, alitumia dakika 20 kutaja na kutambua majina ya watu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili limekuwa likitokea mara nyingi sana kwa Mawaziri, wanapokuja kujibu hoja za Wabunge hapa ndani, wanatumia zaidi ya nusu ya muda waliopewa ku-*acknowladge* na kutaja majina ya watu, huenda wana nia njema, lakini kwa hakika mimi ninaomba Mwongozo wako, ni kwanini tusifute utaratibu huu na tabia hii ikomeshwe kabisa Mawaziri, kutaja majina ya watu humu ndani au Kampeni Meneja au Mbunge kwa sababu, kama nilichangia watu wameniona au watu wamenisikia na mimi najua nimechangia. Dakika 40 wanazopewa Mawaziri, wazitumie kwenye kujibu hoja zenye manufaa kwa Watanzania na sisi Wabunge, badala ya kutaja majina humu ndani. Naomba tabia hii kwa Mawaziri wetu, isiendelee.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Miongozo hiyo nitaitoa baadaye.

Sasa naomba tuendelee, Katibu tuendelee.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa 2012/2013
### Wizara ya Fedha

**NAIBU SPIKA:** Naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa. *(Makofi)*

Karibu sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruksa yako naomba kuwakilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu ya Fedha, kwa Mwaka 2012/2013. Kufuatia Taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, wakati uliopita huko, naomba kutoa Hoja kwamba, Bunge lako Tukufu, likubali kupokea sasa na kujadili, kupitisha Makadirio ya Mapato na matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika na kwako wewe mwenyewe Naibu Spika, Mbunge wa Kongwa. Waheshimiwa Wenyeviti, Jenista Joachim Mhagama Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba, Mbunge wa Dole na Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mbunge wa Ilala, kwa kuongoza vema majadiliano ya Bunge la Bajeti hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kuwashukuru Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Janet Z. Mbene na Mheshimiwa Saada M. Salum pamoja na Katibu Mkuu, Ndugu Ramadhan M. Khijjah na Manaibu wake Ndugu Laston T. Msongole, Dkt. Servacius B. Likwelile na Ndugu Elizabeth J. Nyambibo kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Taasisi na Wakala wa Serikali, chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisome maelezo haya kwa muhtasari na hotuba nzima iingie katika kitabu cha *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara kwa mwaka 2011/2012. Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kupitia mafungu manne ya kibajeti. Mafungu hayo ni Fungu 50 - Wizara ya Fedha; Fungu 21 – HAZINA; Fungu 22 - Deni la Taifa; Fungu 23 - Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na - Fungu 45 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2011/2012, utekelezaji ulizingatia malengo kama yalivyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Wizara wa mwaka 2009/2010 - 2011/2012. Malengo hayo ni haya yafuatayo: kuboresha ukuaji wa uchumi wenye kuzingatia usawa; kuboresha usimamizi wa rasilimali fedha na uwajibikaji; kuboresha uratibu na upatikanaji wa rasilimali, ugawaji na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma; kusimamia mafao na pensheni ya wastaafu kwa waliokuwa watumishi wa Serikali na malipo ya mirathi; kuboresha mawasiliano na wadau kwa dhana ya ushirikishwaji na ushauri kwa umma; kujenga uwezo wa rasilimali watu na kuboresha mazingira ya kazi na kuboresha huduma kwa watumishi waishio na virusi vya ukimwi na kupunguza maambukizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa malengo haya yataiwezesha Wizara kuchangia katika kufikia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025; Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano 2011/2012 - 2015/2016; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania

(MKUKUTA); Malengo ya Maendeleo ya Milenia; Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA) pamoja na Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma *(Public Finance Management Reform Programme –PFMRP).* Aidha, Mpango na Bajeti ulizingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara kwa kuzingatia jukumu lake la msingi la kukusanya mapato na kusimamia matumizi ya fedha za umma, ilijikita katika kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla;

(ii) Kusimamia na kuratibu shughuli za Taasisi na mashirika ya umma;

(iii) Kukusanya mapato ya ndani yasiyopungua shilingi bilioni 6,435.28. Kati ya hizo shilingi bilioni 6,228.80 ni mapato ya kodi na shilingi bilioni 206.48 ni mapato yasiyo ya kodi;

(iv) Kujenga uwezo wa uandaaji na usimamizi wa Bajeti ya Muda wa Kati pamoja na utoaji wa taarifa za utekelezaji kwa wakati;

(v) Kufanya ukaguzi wa ndani na kuimarisha Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali;

(vi) Kusimamia utekelezaji wa bajeti ya serikali na uratibu wa utekelezaji wa MKUKUTA;

(vii) Kusimamia deni la taifa;

(viii) Kusimamia na kuhakiki malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali na Taasisi zake;

(ix) Kuendeleza kada za Uhasibu, Ukaguzi wa Ndani, Ununuzi na Ugavi, Uchumi, Uhakiki Mali, Mipango, Usimamizi wa Fedha, Watakwimu na Wataalamu wa Kompyuta;

(x) Kuendelea kuhuisha Daftari la Mali ya Serikali;

(xi) Kuendelea na ukaguzi wa miradi ya maendeleo na kusimamia utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la *Millennium Challenge Corporation (MCC);*

(xii) Kuboresha utoaji wa huduma za mafao ya wastaafu na mirathi;

(xiii) Kuimarisha Mtandao wa Malipo – *(Intergrated Financial Management System – IFMS)* katika ngazi zote za Serikali, na kusambaza matumizi ya mfumo wa malipo kwa njia ya elektroniki katika HAZINA ndogo na Sekretarieti za Mikoa;

(xiv) Kutoa mafunzo ya kuandaa hesabu za serikali katika viwango vya kimataifa;

(xv) Kuhamasisha ushiriki wa Sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya ubia; na

(xvi) Kutoa mikopo kwa asasi ndogo za fedha kupitia Mradi wa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo *(Small*

*Enterprise Loans Facility Project - SELF)* na kuongeza kasi ya ukusanyaji wa madeni ya mikopo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2011/2012 na malengo ya mwaka 2012/2013. Ukusanyaji wa mapato kwa mwaka2011/2012. Kuanzia Julai 2011 hadi Juni, 2012 mapato ya kodi yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yalifikia shilingi bilioni 6,511.2, sawa na asilimia 104.5 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 6,228.8. Aidha, Wizara ilikusanya mapato yasiyo ya kodi kiasi cha shilingi bilioni 214.62 sawa na asilimia 103.9 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 206.48. Kufikiwa kwa malengo ya makusanyo ya mapato ya kodi kumetokana na kuboresha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato na utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Tatu wa miaka mitano wa maboresho ya utendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, ukusanyaji wa mapato utaendelea kuimarika kwa kuchukua hatua za kisera na kiutawala kwa maeneo ya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi. Kwa kuzingatia hatua hizo, mapato ya kodi kwa mwaka 2012/2013 yatakayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania yamepangwa kufikia shilingi bilioni 8,070.09. Aidha, mapato yasiyokuwa ya kodi yamepangwa kufikia shilingi bilioni 124.42 kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, misaada na mikopo. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara ilipanga kukusanya mapato kutokana na misaada na mikopo kutoka nje ya nchi yenye thamani ya shilingi bilioni 3,923.55. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 869.41 ni misaada na mikopo ya kibajeti

na shilingi bilioni 2,366.14 ni misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo na shilingi bilioni 688 ni misaada na mikopo ya mifuko ya kisekta. Hadi kufikia mwishoni mwa Juni, 2012 misaada na mikopo iliyopokelewa ilikuwa shilingi bilioni 2,487.9 sawa na asilimia 63 ya makadirio ya mwaka. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 916 sawa na asilimia 105 ya makadirio ilikuwa misaada na mikopo ya kibajeti na shilingi bilioni 1,571.9 sawa na asilimia 51 ya makadirio ilikuwa misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo na mifuko ya kisekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imelenga kukusanya mapato ya shilingi bilioni 3,229.0 kutokana na misaada na mikopo kutoka nje. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 842.48 ni misaada na mikopo ya kibajeti, shilingi bilioni 1,971.40 ni misaada na mikopo ya miradi ya maendeleo ikijumuisha shilingi bilioni 72.3 marejesho ya fedha ya rada na shilingi bilioni 415.14 ni misaada na mikopo ya mifuko ya kisekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la shilingi bilioni 72.3 nitalieleza baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa Deni la Taifa. Wizara ya Fedha imeendelea kusimamia deni la taifa kwa kuzingatia Mkakati wa Kusimamia Deni la Taifa wa mwaka 2002 pamoja na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Na. 30 ya mwaka 1974 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2004. Hadi mwishoni mwa mwezi Juni 2012, Deni la Taifa *(debt stock)* lilikuwa shilingi bilioni 20,865.0 ikilinganishwa na deni la shilingi bilioni 18,617.0 mwezi Juni 2011 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 10.7. Kati ya hizo, shilingi bilioni 15,927.1 zilikuwa ni deni la nje na shilingi bilioni

4,937.9 ni deni la ndani yaani *domestic debt.* Kati ya kiasi cha deni la nje, shilingi bilioni 12,644.6 zilikuwa ni deni la umma na kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 3,282.5 ni deni la sekta binafsi. Aidha, hadi kufikia mwezi Juni 2012, deni la ndani yaani la Serikali lilifikia shilingi bilioni 4,937.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 4,729.0 mwezi Juni, 2011, sawa na ongezeko la asilimia 4.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera za Bajeti na Fedha *(Fiscal & Monetary Policies)* zinajumuisha mikopo ya ndani na nje. Kuongezeka kwa Deni la Taifa kumetokana na mikopo mipya ya ndani na nje inayokopwa ili kuziba nakisi ya bajeti ya maendeleo. Hadi kufikia Juni 2012, malimbikizo ya deni kwa nchi ambazo bado hazijatoa misamaha yalifikia Dola za Marekani milioni 907.24. Nchi hizo ni Brazil ambayo iko kwenye kundi la Klabu ya Paris ambayo malimbikizo ya deni kwa nchi hiyo ni Dola za Marekani milioni 239.6. Nchi nyingine ambazo zipo kwenye kundi lisilo la Klabu ya Paris ni Iran (Dola za Kimarekani milioni 372.03), Iraq (Dola za Kimarekani milioni 290.1) na Angola (Dola za Kimarekani milioni 5.51). Majadiliano ya msamaha wa madeni baina ya Serikali na nchi hizo yanaendelea na yamefikia katika hatua nzuri ya kufikia makubaliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo ya deni la Taifa hufanyika kupitia Fungu 22 - Deni la Taifa. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2011 hadi Juni, 2012, malipo ya deni la ndani yalikuwa shilingi bilioni 1,671.71 na malipo ya deni la nje yalikuwa shilingi bilioni 125.15. Aidha, madai na madeni mengine hulipwa kupitia mafungu ya Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuongeza ufanisi katika kuratibu na kusimamia Deni la Taifa katika mwaka wa fedha

2012/2013, Wizara imepanga kufanya marekebisho katika Muundo wake kwa kuanzisha Idara kamili ya usimamizi wa Deni la Taifa ambayo pia itakuwa na wataalam wenye weledi katika masuala ya mikopo ya kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uandaaji, usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2011/2012. Katika kutekeleza majukumu yake, Wizara iliandaa, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Aidha, Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ambao unatekeleza Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 - 2015/2016 uliandaliwa. Mwongozo huo ulisambazwa kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala za Serikali, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na umetumika katika kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2012/2013. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuboresha malengo, matokeo na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa bajeti ya Serikali, Wizara imeandaa taarifa mbalimbali zikiwemo: Vitabu vya bajeti; Taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2011/2012; Taarifa ya Uchambuzi wa Bajeti ya Serikali katika Kipindi cha Muda wa Kati *(Budget Background and Medium Term Expenditure Framework – 2011/12 - 2012/13);* Taarifa za madeni; Taarifa za mfumuko wa bei; Taarifa ya Hali ya Uchumi; Taarifa za kifedha kupitia Benki Kuu na Kitabu cha bajeti ya Serikali kwa lugha rahisi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara iliratibu tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali pamoja na Mkutano wa Taifa wa Mwaka wa

Mjadala wa Kisera *(National Annual Policy Dialogue)*. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, ilikuwa mwenyeji wa mkutano wa 20 wa Bodi ya Magavana wa *"The African Capacity Building Foundation",* Mkutano wa Bodi ya Magavana wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na Mkutano wa 16 wa Kamati ya Wataalam wa Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Masuala ya Uchumi ya Afrika Ukanda wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara inakusudia kuendelea kujenga uwezo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuandaa mipango na bajeti; kuandaa Mwongozo wa Mpango na Bajeti; kufuatilia matumizi ya fedha za Serikali; Kuandaa maelezo ya bajeti na kitabu cha bajeti ya Serikali kwa lugha rahisi *(Budget Background and Citizen Budget)* na kuendelea kuboresha uandaaji wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa fedha za umma. Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ilikamilisha utekelezaji wa awamu ya tatu ya programu hii ambapo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuimarisha mfumo wa malipo kwa njia ya elektroniki katika Wizara na Idara zinazofanya malipo kupitia Ofisi Kuu ya Malipo Hazina; kutoa mafunzo ya *"Cash Management"* na malipo kwa njia ya elektroniki kwa Wahasibu 304 kutoka Sekretarieti za Mikoa, HAZINA Ndogo, TAMISEMI, Ofisi ya Bunge na Tume ya Ushirika na Masoko; pamoja na kutoa mafunzo na kuandaa Mwongozo wa Kihasibu wa kutumia viwango vya kimataifa vya kuandaa hesabu *(IPSAS –Accrual)* kwa Wahasibu wa Wizara, Idara,

Mikoa na Balozi pamoja na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kusimamia uendeshaji wa mtandao wa malipo wa Serikali *IFMS* kwa kuziwezesha Wizara, Idara za Serikali na Mikoa kutumia mtandao huo kwa ufanisi. Aidha, maboresho ya mfumo wa kihasibu wa '*Epicor*' kutoka toleo namba 7.3.5 kwenda toleo namba 9.05 yamefanyika. Toleo hilo limeanza kutumika mwaka huu wa fedha wa 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika kama zilivyokusudiwa, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na TAMISEMI imefanya ukaguzi wa matumizi ya fedha katika Halmashauri saba ambazo ni: Muleba, Kiteto, Lindi, Geita, Bukombe, Musoma na Jiji la Mwanza. Aidha, Wizara ilifanya ukaguzi wa fedha zilizotumika kununua chakula cha hifadhi kwa Wakala wa Hifadhi ya Chakula katika hifadhi za Songea, Makambako, Sumbawanga, Shinyanga, Arusha, Dodoma na Kipawa. Taarifa za ukaguzi huo ziliandaliwa na kusambazwa kwa wahusika ili kufanyia kazi kasoro zilizojitokeza. Wizara inafuatilia utekelezaji wa hatua zilizochukuliwa kurekebisha kasoro hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudi za kuboresha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha na mali ya Serikali, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wa kiutendaji Watumishi wa Kada za Uhasibu, Ununuzi na Ugavi, Ukaguzi wa Ndani na Mifumo ya Kompyuta. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imedhamini mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 263 wa kada hizo kutoka Wizara,

Idara za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa katika vyuo mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara inakusudia kufanya yafuatayo: kudhamini watumishi wa Serikali katika vyuo mbalimbali vya Uhasibu na Kompyuta; kusimamia na kuimarisha uendeshaji na uunganishaji wa mtandao wa malipo wa Serikali; kutekeleza hatua za kuingia kwenye utaratibu wa kuandaa hesabu za Serikali kwa viwango vya kimataifa vya uhasibu; kuanza kutumia mfumo wa malipo wa elektroniki katika HAZINA ndogo na Mikoa yote; kuendelea kutoa miongozo ya kusimamia na kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali; kusimamia mfuko wa mikopo kwa watumishi wa umma; kutengeneza *VISA Stickers,* kufunga mitambo ya kutolea *VISA Stickers* na kurekebisha mfumo wa kutolea *VISA* kwenye Balozi zetu ili kudhibiti na kuongeza mapato ya Serikali; na kuimarisha usimamizi na utoaji wa taarifa mbalimbali za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukaguzi wa ndani. Ili kuimarisha uwazi na uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma, Wizara imeendelea kuimarisha Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imefanya yafuatayo: kuandaa Mpango Mkakati wa Ukaguzi wa Ndani; kutayarisha mwongozo wa kazi ya Ukaguzi wa Ndani na kutoa mafunzo ya mwongozo huo kwa wakaguzi wa ndani 500 kutoka Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Aidha, katika juhudi za kuwajengea uwezo wakaguzi wa ndani, Wizara imeendelea kudhamini mafunzo ya muda mfupi katika kozi za kitaaluma za ukaguzi wa ndani, ukaguzi wa kiuchunguzi na mafunzo yaliyolenga maeneo hatarishi. Vile vile, mafunzo yalitolewa kwa kamati

za ukaguzi za mamlaka za Serikali za Mitaa katika mikoa ya Dar es Salaam na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliendelea na ukaguzi wa kiufundi *(Technical Audit)* wa miradi inayotekelezwa na Wizara mbalimbali, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali. Katika kutekeleza hili, miradi mbalimbali ya majengo na barabara ilikaguliwa. Miradi hiyo ni pamoja na: Hospitali ya Rufaa – Singida; jengo la Mahakama Kuu - Shinyanga; Hospitali ya Mkoa - Shinyanga; makazi ya Spika - Dar-es-Salaam na maktaba ya Kisasa katika Chuo cha Usafirishaji. Kwa upande wa barabara zilizokaguliwa ni: barabara za Nzega - Puge – Tabora; Ndundu – Somanga; Mwenge – Tegeta, Dar-es-salaam na mradi wa mabasi yaendayo kasi Dar es salaam *(DART).* Aidha, Wizara ilikagua utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (*MMES*) katika Manispaa za Ilala, Temeke na Kinondoni katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kaguzi hizi, mambo yafuatayo yalibainika: kutozingatiwa kikamilifu kwa sheria na taratibu za ununuzi wa umma; viwango hafifu vya ubora wa kazi zilizofanywa na miradi mingi kutokamilika katika muda uliopangwa. Wizara ya Fedha imewasiliana na Wizara na Wakala zenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo na kutoa ushauri wa hatua za kuchukua ili kurekebisha kasoro zilizojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kupitia Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali inakusudia kutekeleza yafuatayo: kukamilisha kanuni za maadili ya Wakaguzi wa Ndani Serikalini; kukamilisha mkataba wa makubaliano kati ya Wakaguzi wa

Ndani na wateja wake; kuandaa mwongozo wa utekelezaji wa usimamizi wa vihatarishi *(Guideline on Implementation of Institutional Risk Management Framework);* kuhuisha Mwongozo wa Ukaguzi wa ndani wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa uendane na viwango vya kimataifa; kuandaa Mpango Mkakati wa Teknolojia ya Mifumo ya Fedha; kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa watekelezaji wa miradi hiyo; kuandaa mwongozo wa uhakiki wa ubora wa ukaguzi wa ndani na kuandaa Mwongozo wa Kamati za Ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa hesabu za Serikali. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilifanikiwa kutekeleza malengo yaliyopangwa. Ofisi iliweza kupanua wigo wa ukaguzi katika ngazi ya Halmashauri na kufika hadi vijijini kuhakiki utekelezaji wa miradi na matumizi ya fedha zinazotolewa kuendana na Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Serikali za Mitaa *(D-by-D).*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ofisi iliweza kutoa ripoti tano za ukaguzi wa thamani ya fedha yaani *value for money.* Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeendelea kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Kiutambuzi *(Forensic Audit Unit)* kwa kuwajengea uwezo Wakaguzi wa kitengo hicho kwa kuwaambatisha kwenye ofisi za ukaguzi za nchi za nje zinazofanya vizuri katika eneo hilo. Vilevile, ofisi imeweza kukamilisha ukaguzi kwa kutumia mifumo ya kompyuta *(System Audit)* katika kaguzi zote. Kadhalika, muundo mpya wa ofisi umeanza kutekelezwa kwa awamu ili kukidhi mahitaji ya Sheria ya Ukaguzi wa

Umma Na.11 ya mwaka 2008. Ujenzi wa ofisi katika Mikoa ya Kilimanjaro na Shinyanga pia umekamilika na ujenzi wa ofisi za Mikoa ya Dodoma na Rukwa umeanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, ofisi itakuwa inatekeleza kwa mwaka wa pili mpango mkakati wa mwaka 2011/1202 hadi 2015/2016. Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imelenga kutekeleza yafuatayo: kukagua mafungu 49 ya Wizara na Idara za Serikali, hesabu za Mikoa 21 ya Tanzania Bara, hesabu za Halmashauri 134 za Miji, Wilaya, Manispaa na Majiji, Mashirika ya Umma 170, Balozi zote zilizoko nje ya nchi na Wakala 33 za Serikali; kukamilisha ukaguzi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kwa kutumia *Audit Software - TeamMate* na kuzingatia viwango vya Kimataifa vya ukaguzi; kushiriki kikamilifu katika jukumu jipya la kukagua taasisi za Umoja wa Mataifa ambapo Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imechaguliwa kuwakilisha Bara la Afrika katika Bodi ya Ukaguzi ya Umoja wa Mataifa *(UN Board of Auditors)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi itaendelea na ujenzi wa majengo katika Mikoa ya Dodoma na Rukwa pamoja na kuanza ujenzi katika Mikoa ya Mara na Iringa ili kuondokana na kutegemea ofisi za wakaguliwa. Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi itaanza ujenzi wa kituo cha mafunzo cha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi *(NAO training centre*) katika eneo la Gezaulole – Kigamboni pale Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi itaendelea kufanya ukaguzi wa Mashirika ya Umma hasa uendeshaji wake *(Management Audit),* ukaguzi wa ufanisi pamoja na ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali

Kuu pamoja na Halmashauri. Aidha, ofisi itaweka mifumo ya kompyuta katika huduma mbalimbali zinazotolewa na ofisi hasa katika maeneo ya masijala, utumishi, bohari na kitengo cha kushughulikia ukaguzi wa majalada ya wastaafu, kuunganisha ofisi 10 za ukaguzi zilizoko Mikoani na Makao Makuu kwa kutumia *Wide Area Network* (*WAN*). Vilevile, ofisi itaendelea kufanya kaguzi za thamani ya fedha na kupanua wigo wa ukaguzi wa fedha (*Regularity Audit*) kwa kufanya uhakiki wa utekelezaji wa miradi na matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa malipo ya mishahara ya watumishi wa umma. Katika uhakiki wa watumishi uliofanyika mwezi Januari 2012, kwenye Halmashauri 133 na kwenye Taasisi na Wakala za Serikali 154 majina 9,949 ya watumishi wasiostahili kuwemo kwenye orodha ya mishahara yalibainika na hivyo kuyaondoa kwenye orodha hiyo. Taarifa ya ukaguzi imetayarishwa na kupelekwa kwa mamlaka husika kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki. Wizara inafuatilia kwa mamlaka husika kufahamu hatua zilizochukuliwa kwa watumishi husika. Aidha, Wizara imeanzisha kitengo cha ukaguzi wa mifumo ya *TEHAMA (IT and Systems Audit)* chini ya Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali ambacho kinashughulikia uandaaji wa miongozo kwa ajili ya kaguzi za mishahara na bajeti, pamoja na kufanya kaguzi katika mifumo ya mishahara na bajeti. Kitengo hiki kinatumia *Audit Payroll Analytics Software* ambayo itarahisisha ukaguzi wa mfumo wa malipo ya mishahara na kubaini dosari ili kuchukua hatua kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itaendelea kukamilisha uhakiki wa

watumishi wa Wizara, Idara zinazojitegemea na Mikoa pamoja na kuendelea kusimamia ulipaji wa mishahara ya watumishi wa Serikali na taasisi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa mali ya Serikali. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imehakiki utunzaji wa mali ya Serikali na kutoa ushauri. Katika kulitekeleza hilo uthamini wa mali umefanyika katika Wizara 20, Idara zinazojitegemea 12 na Mikoa minne na mwongozo wa usimamizi wa mali ya Serikali ulitayarishwa. Aidha, Wizara imehakiki mali katika bohari za Serikali 350 ambapo ushauri na taarifa zake zimetolewa kwa Maafisa Masuuli husika; mali chakavu Serikalini ziliondoshwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Fedha ambapo jumla ya magari 145, pikipiki sita, mitambo 74 na vifaa mbalimbali vilihusika. Katika zoezi hilo, jumla ya shilingi bilioni 1.73 zilipatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itaendelea na kazi ya kuingiza kwenye daftari mali ya Serikali iliyokwisha thaminiwa na kuondosha mali chakavu kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Fedha. Aidha, kazi ya kuhakiki mali ya Serikali katika Wizara, Idara zinazojitegemea na Balozi za Tanzania nchi za nje itaendelea ili kutoa ushauri na kuhakikisha kuwa mali ya Serikali inatunzwa na kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa. Vilevile, Wizara itaandaa Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mali ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa mashirika na taasisi za umma. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imeendelea kusimamia utendaji wa mashirika ya umma pamoja na taasisi za Serikali. Majukumu yaliyotekelezwa ni pamoja na: kuendesha zoezi la ukaguzi wa kimenejimenti

katika taasisi zifuatazo: Hospitali ya Rufaa (*KCMC*), Chuo cha Ubaharia cha Dar es Salaam (*DMI*), Tume ya Matumizi Bora ya Ardhi na Chuo Kikuu Kishiriki cha Stadi za Ushirika na Biashara (*MUCCoBS*).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, uhakiki wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*), Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu (*CDA*), Shirika la Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (*COASCO*), Taasisi ya Uhasibu Arusha (*IAA*), Taasisi ya Utafiti wa Madawa ya Wadudu Waharibifu katika Nchi za Tropiki *(TPRI),* Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (*NIT*), Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo (*TEMDO*) na Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (*CAMARTEC*) unaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uhakiki huo masuala ya msingi yaliyoangaliwa ni pamoja na uzingatiaji wa kanuni, sheria na miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali, uwajibikaji na utawala bora, matumizi ya fedha za mishahara, matumizi mengineyo na kuangalia jinsi taratibu za ajira zinavyozingatiwa katika taasisi na mashirika ya Umma. Zoezi hili ni endelevu na linalenga kuboresha uendeshaji wa mashirika na taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, Wizara ilichambua na kuidhinisha miundo ya utumishi kwa taasisi na Mashirika 20, kanuni za utumishi kwa taasisi na mashirika 15 na kanuni za fedha kwa taasisi na mashirika 25. Aidha, ikama na bajeti kwa taasisi za Serikali 132 zilichambuliwa na kuidhinishwa kwa ajili ya malipo ya mishahara, upandishwaji vyeo na ajira mpya. Vilevile, uchambuzi wa mikataba ya hiari kwa mashirika mawili (2) ulifanyika, mapendekezo kutolewa na hatimaye kuidhinishwa. Kadhalika, katika

kipindi hicho, jumla ya taasisi 15 zenye mishahara ya kipekee zimewasilisha maombi ya kuhuisha miundo ya utumishi na mifumo ya mishahara ambayo bado uchambuzi wake unaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itatekeleza yafuatayo: kuchambua bajeti za mashirika na kuainisha kiasi cha mapato kinachoweza kupatikana kutoka katika kila shirika ili yaweze kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali; kufanya ukaguzi wa kimenejimenti (*Management Audit*) kwa wakala, taasisi na mashirika ya umma; kuchambua na kuidhinisha miundo ya utumishi na mifumo ya mishahara, kanuni za utumishi pamoja na mikataba ya hiari kwa taasisi. Pia kuchambua na kuidhinisha makadirio ya ikama na bajeti kwa taasisi za Serikali kwa ajili ya malipo ya mishahara, upandishwaji vyeo na ajira mpya; kuhuisha nyaraka za mishahara ya taasisi kwa mujibu wa ongezeko la mishahara lililotolewa na Serikali, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeweka uwiano wa ongezeko la mishahara kwa kila kada na katika kila mfumo wa mishahara na kuandaa viwango sawa vya posho za madaraka kwa taasisi za elimu ili kuweka uwiano wa posho hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itasimamia na kuratibu zoezi la ubinafsishaji, urekebishaji na ufuatiliaji linaloendelea kwa mashirika na makampuni ya *UDA, TRL, TTCL, ATCL, General Tyre East Africa, URAFIKI (FTC)* na hisa za Serikali katika *TDFL*. Aidha, Wizara itaimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina ili iweze kusimamia kikamilifu mashirika ya umma ikiwa ni pamoja na kutunga sheria mpya ili kuipa nguvu zaidi za kusimamia mashirika na taasisi za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi – *Public Private Partnership (PPP).* Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara imetayarisha mwongozo wa uendeshaji wa miradi ya ubia (*PPP Operational Guidelines*). Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, imeandaa mkakati wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (*PPP Implementation Strategy*). Vilevile, Wizara imeendelea kuimarisha kitengo kinachoshughulikia ubia kwa kuwapatia mafunzo maafisa walioko katika kitengo hicho pamoja na kuongeza vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imelenga kutoa mafunzo kuhusu dhana ya ubia kwa watumishi wa vitengo na madawati ya ubia katika wizara mbalimbali; kufanya utafiti wa baadhi ya miradi ya *PPP* ambayo inaendelea na kuanza kutathmini miradi ya ubia kwa lengo la kuidhinisha na kukamilisha miongozo na taratibu za utekelezaji wa sera ya ubia pamoja na kuisambaza kwa wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, uratibu wa utekelezaji wa MKUKUTA. MKUKUTA ni Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini, unaojielekeza katika matokeo katika maeneo makuu matatu, ambayo ni kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato, kuboresha maisha na ustawi wa jamii na utawala bora na uwajibikaji. Lengo likiwa kupunguza umaskini wa kipato kufikia asilimia 20.4 ifikapo mwaka 2015 kutoka asilimia 33.6 mwaka 2007. Utekelezaji wa MKUKUTA huratibiwa na Wizara kupitia Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini *(MKUKUTA Monitoring Master Plan)* na taarifa mbalimbali za uchambuzi wa

utekelzaji hutolewa. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Wizara iliandaa na kusambaza taarifa ya mwaka ya utekelezaji ya MKUKUTA, taarifa ya hali ya umaskini na maendeleo ya watu na taarifa ya maendeleo ya malengo ya millenia. Taarifa hizi zimechambua mwenendo wa viashiria vya umaskini, mafanikio, changamoto na zimependeka hatua za kuchukua. Aidha, Wizara imekamilisha mkakati wa mawasiliano wa MKUKUTA na utafiti wa maoni ya watu kuhusu umaskini *(Views of the People Survey).* Taarifa ya matokeo ya utafiti huo inaandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada nyingine zilizofanyika ni pamoja na kuhamasisha na kuelimisha umma kuhusu kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Shughuli hizi ni pamoja na kuendesha semina kwa makundi mbalimbali ya kijamii, kuchapisha na kusambaza taarifa na majarida mbalimbali yenye lengo la kuhamasisha shughuli za uzalishaji na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumze juu ya Mradi wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo *(Small Entrepreneurs Loan Facility –SELF)*. Katika mwaka 2011/2012, mfuko wa *SELF* ulitoa mikopo ya shilingi bilioni 8.77 kwa taasisi ndogo za fedha 111 na kuwafikia walengwa 7,729. Kwa wastani urejeshwaji wa mikopo ulifikia shilingi bilioni 8.31 ambazo ni sawa na asilimia 94.75. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa wajasiriamali 1,417, watendaji 317 ambao ni asilimia 99 ya walengwa (320), wakiwemo maafisa mikopo, wajumbe wa kamati za mikopo za asasi, watunza vitabu vya fedha na wajumbe wa bodi na watoa huduma za maendeleo ya biashara 39 ambao ni Maafisa Ushirika wa Wilaya. Vilevile, watumishi wa mradi wapatao 19 walipatiwa

mafunzo mbalimbali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za mradi. Mradi pia ulifanya uhamasishaji katika mikoa yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Programu ya Taifa ya Kuongeza Kipato *(National Income Generation Programme – NIGP).* Programu ya Taifa ya Kuongeza Kipato ilikuwa na miradi mingi ya masoko pamoja na baba na mama lishe ambayo baadae ilikabidhiwa kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa na kubakiza miradi michache ya ufugaji nyuki na kuzalisha chumvi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kusimamia *NIGP* kwa kufuatilia utekelezaji wa miradi hiyo. Wananchi walipatiwa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki na miradi inayoendelea iliimarishwa kwa kupatiwa vifaa vya kuzalisha na kuvuna asali. Aidha, *NIGP* iliendelea kusimamia miradi ya uzalishaji wa chumvi katika maeneo ya Chake Chake (Pemba) na Chukwani (Unguja).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imelenga kutekeleza yafuatayo: kufanya tathmini ya MKUKUTA II na kuandaa taarifa ya mwaka ya utekelezaji ambayo itabainisha mafanikio na changamoto zilizopo; kuandaa taarifa ya malengo ya milenia; kutambua na kuainisha juhudi mbalimbali za kinga ya jamii zinazofanyika nchini na kutangaza fursa zinazotolewa na mifuko ya wajasiriamali (*SELF* na *NIGP*) kwenye vyombo vya habari ili wananchi waweze kunufaika nazo. Aidha, Wizara itafanya tathmini ya miradi ya programu ya *NIGP* ili kubaini namna bora ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumze juu ya huduma kwa wastaafu na mirathi. Pamoja na kuanzishwa kwa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (*PSPF*),

Wizara ya Fedha inawalipa pensheni watumishi waliostaafu kabla ya Juni 2004, Wanajeshi, Usalama wa Taifa, Viongozi Wastaafu wa Kitaifa na watumishi wenye ajira katika mamlaka mbili. Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Juni 2012, Wizara imelipa mafao na stahili za wastaafu ya shilingi bilioni 120.03 sawa na asilimia 100 ya bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Wizara imeanza kuwalipa wastaafu pensheni kwa vipindi vya miezi mitatu mitatu badala ya miezi sita sita kuanzia Januari 2012. Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka hili lilikuwa ombi la Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika juhudi za kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa wastaafu ambao wapo kwenye daftari la pensheni la Hazina, Wizara inaendelea kuweka kumbukumbu zilizopo kwenye majalada binafsi ya wastaafu kwenye mfumo wa kompyuta ujulikanao kwa jina la *Saperion* kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa za mstaafu kila zinapohitajika. Hadi mwezi Juni 2012, jumla ya majalada 72,928 yameshaingizwa kwenye mfumo huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imechukua hatua mbali mbali zenye lengo la kuondoa ucheleweshaji wa malipo ya mirathi. Hatua zilizochukuliwa na Wizara ni pamoja na: kutoa elimu kwa umma kupitia vipeperushi, maonesho mbalimbali ya kitaifa; kutoa mafunzo kwa maafisa wa ofisi za Hazina Ndogo na Makarani na Wahasibu wa Mahakama zinazoshughulikia malipo ya mirathi ambayo yalifanyika katika kanda sita zenye Mikoa minne minne katika vituo vya Mwanza, Arusha, Dodoma, Morogoro, Mbeya na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itatoa mafunzo kama hayo kwa baadhi ya Mahakimu kutoka katika Mahakama zinazoshughulikia malipo ya mirathi ili kuwepo na uelewa sawa kwa maafisa wa Mahakama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze juu ya michango ya mwajiri katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Wizara imeendelea kuwasilisha michango ya mwajiri ya watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kwenye Mifuko mbalimbali ya Hifadhi ya Jamii *(PSPF, GEPF, LAPF, PPF na NSSF),* pamoja na Mfuko wa Bima ya Afya - *NHIF*. Kufikia mwezi Juni 2012, kiasi cha shilingi bilioni 534.0 kimewasilishwa kwenye mifuko hiyo. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itaendelea kulipa michango ya mwajiri kwa mujibu wa sheria kwa watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kila mwezi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria na Miswada ya Fedha. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara iliendelea kuzifanyia marekebisho sheria mbalimbali ili ziendane na wakati na mahitaji yaliyopo. Baadhi ya sheria zilizofanyiwa marekebisho ni Sheria ya Fedha Haramu Sura 423 *(The Anti-Money Laundering (Amendment) Act, 2012)* ambayo ilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Februari, 2012 pamoja na Sheria ya Fedha ya mwaka 2011 *(The Finance Act, 2011).* Aidha, Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 ilipitishwa na Bunge mwezi Novemba 2011. Vilevile, Sheria ya Bima ya mwaka 2009 ilifanyiwa marekebisho na Bunge mwezi Aprili, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha 2012/2013, Wizara itaendelea kukamilisha maandalizi ya kuwezesha kutungwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Malipo ya Ki-elektroniki *(The National Electronic Payment System Act)* pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Taasisi zinazotoa Mikopo Midogo Midogo *(The National Microfinance Act)*. Sheria hii inalenga kuvitambua vikundi kama *VICOBA* na taasisi nyingine ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itakapokamilisha maandalizi ya sheria hizi itawasilisha Miswada ya sheria husika kwa ajili ya kujadiliwa hapa Bungeni. Aidha, Wizara itaendelea kuandaa Kanuni za Sheria mbalimbali za fedha pamoja na nyaraka za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi hizi zitasaidia sheria hii kurasimisha makundi hayo na hivyo kuleta msukumo wa kiuchumi katika jamii kwa kutumia huduma za fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya watumishi. Katika jitihada za kuongeza ufanisi, Wizara imefanya yafuatayo: imeajiri watumishi 57 wa kada mbalimbali; imebadilisha kada watumishi 17; imethibitisha kazini watumishi 229 wa kada mbalimbali na kupandisha vyeo watumishi 214. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha utendaji wa watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Vilevile, katika kutekeleza mkakati wa kupambana na Ukimwi, Wizara imehudumia watumishi wanaoishi na virusi vya Ukimwi. Wizara pia ilifanya vipimo kwa watumishi kwa magonjwa ya saratani na kisukari. Kadhalika, katika kujenga afya za watumishi Wizara

imekuwa ikitoa fursa kwa watumishi kushiriki katika michezo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: kuajiri watumishi 80 wa kada mbalimbali; kubadilisha kazi watumishi waliopata sifa mbalimbali za kitaaluma; kuthibitisha watumishi kazini waliomaliza muda wao wa majaribio na kupandisha vyeo watumishi 300. Aidha, Wizara itaendelea kuwapatia watumishi wake mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao na ya kuwaandaa kwa ajili ya kustaafu. Vilevile, Wizara itaendelea kutoa elimu kuhusu magonjwa sugu pamoja na kuwapatia lishe walioathirika na Ukimwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imesimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyo chini yake. Miradi hiyo ni pamoja na: Ujenzi wa Ofisi ya HAZINA na Upanuzi wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini – Dodoma; Ujenzi wa Maktaba – Chuo cha Uhasibu - Arusha; Ujenzi wa Kituo cha Taaluma ya Uhasibu - Dar es Salaam na Ukarabati wa majengo ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliratibu utekelezaji wa Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (*Public Finance Management Reform Programme- PFMRP),* ambayo utekelezaji wake umeingia katika awamu ya nne kuanzia mwezi Julai 2012. Maeneo yaliyolengwa katika awamu hiyo ni: Usimamizi wa Mapato ya Serikali; Mipango na Uandaaji wa bajeti ya Serikali; Utekelezaji wa Bajeti; Uwazi na Uwajibikaji; Udhibiti wa Bajeti ya Serikali na Ufuatiliaji na Tathmini na Usimamizi wa Programu na

Mabadiliko ya Utendaji. Aidha, Wizara pia imekamilisha uhuishaji wa Mpango Mkakati wake wa Miaka Mitano (2012/2013 – 2016/2017), pamoja na Mkataba wa Huduma kwa Mteja ambayo imeanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itaendelea kusimamia Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara pamoja na kutekeleza Mpango Mkakati wa Awamu ya Nne ya Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma *(PFMRP IV).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya *Millenium Challenge Corporation (MCC).* Wizara imesimamia utekelezaji wa miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia *MCC* ikijumuisha Miradi ya Barabara ya Tunduma-Sumbawanga, Songea-Namtumbo, Peramiho – Mbinga na Tanga - Horohoro; barabara za vijijini Pemba; na Kiwanja cha ndege cha Mafia. Mradi wa barabara ya Tanga - Horohoro upo katika hatua za mwisho za kukamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingine ni ya nishati na maji ambayo utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali. Miradi ya nishati inajumuisha kutandika waya wa umeme chini ya bahari kwenda Zanzibar; kukarabati vituo 24 vya umeme; upanuzi wa mtandao wa umeme katika mikoa ya Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya, Dodoma, Mwanza na Kigoma. Aidha, Miradi ya maji inayotekelezwa ni: upanuzi wa mtambo wa kuchuja maji wa Ruvu Chini; na ukarabati wa mifumo ya maji ya Manispaa ya Morogoro na Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itakamilisha miradi ya *MCC* na kukabidhi miradi iliyokamilika kwa taasisi husika pamoja na kutoa mafunzo kwa ajili ya kuhakikisha usimamizi endelevu wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Pamoja ya Fedha *(Joint Finance Commission – JFC)*. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Tume ya Pamoja ya Fedha imekamilisha Utafiti wa usimamizi wa deni la taifa linalohusu Serikali mbili na kufanya utafiti wa kubaini mfumo bora wa kodi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Matokeo ya tafiti hizo yatawasilishwa kwenye ngazi husika. Aidha, ili kuiwezesha Tume kufanya kazi kwa ufanisi, imepewa fungu lake la kibajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kupitia Tume ya Pamoja ya Fedha imepanga kukamilisha utafiti wa mfumo wa kodi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuanzisha Programu ya Kutekeleza Sera ya Taifa ya Mfumo wa Habari na Mawasiliano na kutoa ushauri kuhusu ushirikishwaji wa pande mbili za Muungano katika utafutaji wa misaada na mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi. Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu inazitaka benki na taasisi za fedha kutunza kumbukumbu sahihi kuhusu wateja wake. Katika kutekeleza jukumu hili, benki na taasisi za fedha zilitakiwa kuhuisha taarifa zote za wateja wake kufikia Machi 2012. Kwa kuwa kumbukumbu hizi zilihusu kipindi kirefu sana na idadi kubwa ya wateja,

benki ziliomba kuongezewa muda hadi Machi 2013 ili ziweze kukamilisha zoezi la kuhakiki taarifa za wateja wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imetoa mafunzo ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi kwa wafanyakazi wa Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi (*Financial Intelligence Unit - FIU)*. Mafunzo hayo yametolewa pia kwa Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Mapato, TAKUKURU na Kurugenzi ya Mashtaka. Aidha, mafunzo mengine ya kupiga vita fedha haramu yalitolewa kwa baadhi ya wafanyakazi wa benki, mashirika ya bima, kasino na biashara za michezo ya kubahatisha, kampuni za simu, masoko ya mitaji na hisa, Waandishi wa Habari, Mahakimu, Majaji na Wanasheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itafanya yafuatayo: kuboresha Mkakati wa kitaifa wa kupambana na fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; kutoa elimu ya kupiga vita fedha haramu na ufadhili wa ugaidi na kuandaa kanuni, miongozo na taratibu za kukagua watoa taarifa, kwa kushirikiana na wasimamizi wa watoa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, habari, elimu na mawasiliano kwa umma. Wizara ilisimamia na kuendelea kuboresha mawasiliano kati yake na wadau kwa kutoa taarifa kwa wakati. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, elimu kwa umma imetolewa kwa wananchi kuhusu majukumu, mafanikio na changamoto za Wizara kupitia machapisho na vyombo vya habari na njia mbalimbali yakiwemo magazeti, redio, tovuti, televisheni na vipeperushi. Aidha, Wizara imeendelea kuhamasisha umma

kuhusu umuhimu wa kushiriki katika zoezi la sensa ya watu na makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara itatoa elimu kuhusu utendaji wa Wizara, utaratibu wa malipo kwa wastaafu, sheria za kodi na taratibu za kukata rufani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa umma. Katika eneo la ununuzi wa umma, Wizara imetekeleza majukumu yafuatayo: kusimamia marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004; kuandaa Kanuni za Ununuzi wa Umma; kusimamia uandaaji wa Sera ya Taifa ya Ununuzi wa Umma na kusimamia na kuendeleza kada ya Ununuzi na Ugavi Serikalini. Vilevile, Wizara imeboresha daftari la Maafisa Ununuzi na Ugavi Serikalini kwa lengo la kuwatambua na sifa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara inalenga kutekeleza yafuatayo: kukamilisha uandaaji wa Sera ya Ununuzi wa Umma; kuhakikisha ununuzi wa umma unatekelezwa kwa kuzingatia sheria na kuendelea kuhuisha daftari la Maofisa Ununuzi na Ugavi Serikalini. Aidha, Wizara itafanya uchambuzi wa wataalamu wa ununuzi na ugavi ili kubaini mahitaji halisi na kuongeza udahili wa wanafunzi wa taaluma hii katika vyuo vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa ununuzi wa umma. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (*Public Procurement Regulatory Authority - PPRA)* ilitekeleza yafuatayo: kutoa mafunzo kwa taasisi za ununuzi 18

zikiwemo Halmashauri na kuhudhuriwa na watumishi 370 kwa lengo la kuboresha ununuzi kwenye Halmashauri na taasisi nyingine ambazo zilikuwa na hoja mbalimbali za ukaguzi; kuandaa warsha ya wakuu wa vitengo vya ununuzi nchini ambayo ilihudhuriwa na wakuu wa vitengo vya ununuzi 184; na kutoa mafunzo kwa wataalamu wa ununuzi 10 kutoka *PPRA* kuhusu mbinu za kugundua rushwa katika ununuzi wa umma na kufanya ukaguzi wa kiutambuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu mengine yaliyotekelezwa kupitia Mamlaka hiyo ni pamoja na: kufanya ukaguzi wa miradi 113 ya ujenzi iliyokamilishwa na inayoendelea kwenye Taasisi za Umma 30; kufanya ukaguzi wa ununuzi kwenye Taasisi za Umma 120; kufuatilia utekelezaji wa hoja zilizoibuliwa katika kaguzi za nyuma ambapo Maafisa Masuuli wa taasisi za umma 37 zilizofanya vibaya walihojiwa na Bodi ya Wakurugenzi ya *PPRA* na kushauriwa. Aidha, Mamlaka iliwaondoa kwenye shughuli za ununuzi baadhi ya watendaji, kuwachukulia hatua za kinidhamu au kuwajengea uwezo baadhi yao na kuwafungia kushiriki kwenye zabuni makandarasi wanane (8) ambao waligundulika kuhusika kwenye vitendo vya udanganyifu wa kupokea malipo hewa. Aidha, *PPRA* imezifungia kampuni nyingine 384 kutoshiriki kwenye zabuni zinazotolewa na Taasisi za Umma hapa nchini kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja na zaidi kulingana na makosa ya kuhusika na rushwa au vitendo vya udanganyifu na kushindwa kukamilisha mikataba waliyopewa na Taasisi za Umma. Kati ya kampuni hizo 27 ni kampuni za humu nchini na mbili ni za nje lakini zimesajiliwa hapa nchini na zilizobaki ni kampuni za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, *PPRA* imeendendelea kuelimisha umma na kutoa taarifa za zabuni mbalimbali za Taasisi za Umma kupitia jarida la ununuzi – *"Tanzania Procurement Journal"* litolewalo kila wiki na tovuti ya *PPRA (http://www.ppra.go.tz);* kuandaa program ya uelimishaji umma kuhusu masuala ya ununuzi na kutoa mafunzo kwa taasisi 46 kuhusu matumizi ya mfumo wa upokeaji na usimamizi wa taarifa za ununuzi nchini. Vilevile, *PPRA* imeanzisha utaratibu wa kutoa taarifa kuhusu zabuni zinazoitishwa na Taasisi za Umma kwa njia ya ujumbe mfupi kupitia simu za viganjani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imelenga kuongeza ufanisi wa usimamizi na udhibiti wa ununuzi wa umma kulingana na Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma kwa kufanya yafuatayo: kuanza maandalizi ya kujenga ofisi za kudumu za *PPRA* na kuajiri watumishi wa kutosha na kufungua ofisi za kanda ili kuiwezesha *PPRA* kupanua wigo wa usimamizi na ukaguzi kwenye taasisi zilizopo Mikoani hususan Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, rufaa za zabuni za umma. Katika mwaka fedha 2011/2012, jumla ya rufaa 12 zilipokelewa na Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma (*Public Procurement Appeals Authority – PPAA)* na kutolewa maamuzi. Aidha, Mamlaka iliendesha warsha saba za kuelimisha Wazabuni na watendaji wa Serikali na Taasisi za Umma juu ya Sheria ya Ununuzi wa Umma hususan, taratibu za uwasilishaji malalamiko pamoja na haki na wajibu wao katika kuimarisha usimamizi wa shughuli za ununuzi wa umma. Warsha hizo zilifanyika Singida, Shinyanga, Babati, Karatu na Arusha. Vilevile, watendaji 12 na Wajumbe wa Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma walihudhuria

mafunzo mbalimbali ya muda mfupi ili kuwajengea uwezo na kuboresha utendaji wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mamlaka itatekeleza majukumu yafuatayo: kuendelea kushughulikia migogoro inayojitokeza katika ununuzi wa umma; kutoa elimu kwa Wazabuni, Watendaji wa Serikali na Taasisi zake pamoja na umma kwa ujumla juu ya Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 na kujenga uwezo kwa watendaji na wajumbe wa Mamlaka juu ya utatuzi wa migogoro na ununuzi katika miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara kupitia Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (*Government Procurement Services Agency – GPSA)* ilitekeleza majukumu yafuatayo: kuanza utaratibu wa kusimika mfumo wa matumizi ya '*smart card'* kwa ajili ya ununuzi wa mafuta wenye tija kwa magari ya Serikali ambapo mkandarasi amepatikana; kuendesha mafunzo kuhusu mfumo wa ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka unavyofanya kazi kwa lengo la kuwajengea weledi watumishi wa umma na wafanyabiashara katika kituo cha Mwanza ambapo washiriki walitoka Mikoa ya Mwanza, Dar es Salaam, Dodoma, Shinyanga, Kigoma, Kagera, Mara na Tabora. Aidha, Wakala umekamilisha ukarabati na upanuzi wa kisima cha mafuta cha Dar es Salaam na ukarabati wa ofisi ya Tanga. Ukarabati na ujenzi wa ofisi na visima vya mafuta katika Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Lindi, Mtwara, Dodoma na Manyara unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo:

kufungua ofisi za kutoa huduma ya uuzaji wa mafuta na vifaa vya ofisi kwenye mikoa mipya ya Njombe, Katavi, Geita na Simiyu; kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma na wafanyabiashara kuhusu mfumo wa ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka; kukamilisha ujenzi na ukarabati wa ofisi, maghala na vituo vya mafuta katika mikoa ya Manyara, Dodoma, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Tabora, Mbeya, Morogoro, Shinyanga, Lindi, Mtwara, Rukwa na Mwanza na kusimika mitambo ya usimamizi wa usalama *(CCTV)* wa mali za Wakala na wateja wake katika kituo cha mafuta cha Kurasini, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, rufaa za kodi. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Bodi ya Rufaa za Kodi (*Tax Revenue Appeals Board - TRAB)* imepokea rufaa 107 na imesikiliza na kutolea maamuzi rufaa 79. Aidha, Bodi imechapisha taarifa kwa rufaa zote zilizoamuliwa kuanzia mwaka 2005 – 2008 - *Tanzania Tax Law Reports*. Vilevile, Wizara kupitia Baraza la Rufaa za Kodi (*Tax Revenue Appeals Tribunal - TRAT)* imepokea rufaa 44 ambapo rufani 31 zimesikilizwa na kutolewa maamuzi. Kadhalika, Baraza limetoa elimu kwa walipa kodi kuhusu taratibu za kukata rufaa ya kodi na sheria za kodi katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kupitia Bodi ya Rufaa za Kodi imepanga kufanya yafuatayo: kusikiliza na kutolea maamuzi rufaa 103; kutoa elimu kwa walipa kodi juu ya taratibu za kukata rufaa za kodi katika kanda ya kaskazini; kutoa mafunzo kwa wajumbe wapya wa Bodi juu ya taratibu za kutatua migogoro ya kodi itokanayo na sheria za kodi zinazosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na kuchapisha *Tanzania Tax Law Reports* za mwaka 2009-2010.

Aidha, Wizara kupitia Baraza la Rufaa za Kodi inategemea kupokea, kusikiliza na kutolea maamuzi rufaa 80; kutoa elimu kwa walipa kodi katika Mikoa ya Manyara, Dodoma, Singida na Mbeya juu ya taratibu za kukata rufaa za kodi na kutoa mafunzo kwa wajumbe wa Baraza la Rufaa juu ya taratibu za kutatua migogoro ya kodi itokanayo na sheria za kodi zinazosimamiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA).* Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mamlaka ya Mapato Tanzania, ambayo ni Wakala wa Serikali wa ukusanyaji wa mapato ya kodi imeendelea na jukumu hilo. Lengo la makusanyo kwa mwaka 2011/2012 lilikuwa ni shilingi bilioni 6,228.8. Hadi Juni, 2012 jumla ya shilingi bilioni 6,511.2 zilikusanywa ikiwa ni sawa na asilimia 104.5 ya lengo. Katika mwaka wa fedha 2012/2013 lengo ni kukusanya shilingi bilioni 8,070.09.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kufikia lengo hilo, Mamlaka ya Mapato Tanzania imepanga kuendelea kusimamia mikakati mbalimbali iliyoainishwa katika mpango wake wa Tatu unaolenga kuboresha makusanyo ya mapato yatokanayo na kodi. Maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na: Kuendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya ki-elektroniki katika utawala wa kodi ikiwa ni pamoja na kupanua wigo wa matumizi ya mashine za ki-elektroniki za kutoa stakabadhi za kodi (*Electronic Fiscal Device – EFD)* na mfumo wa kuwasilisha ritani *(returns)* za kodi kwa njia ya ki-elektroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Mamlaka ya Mapato Tanzania imepanga kuandaa Mkakati wa Muda wa kati na Muda Mrefu wa

Kuboresha Mapato ya Serikali (*Second Medium and Long Term Revenue Mobilization Strategy*); kuandaa Mpango Kazi wa Nne wa Maboresho wa miaka mitano ambao utaanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai, 2013 kufuatia kumalizika kwa muda wa Mpango Kazi wa Tatu; kukamilisha uanzishwaji wa Kitengo cha Kushughulikia Utozaji Kodi kwa Makampuni ya Kimataifa (*International Taxation Unit)* ili kuboresha ukusanyaji wa mapato kwa makampuni hayo; kuboresha uwezo na ukaguzi kwenye Sekta maalum (madini, mawasiliano, utalii, benki na taasisi nyinginezo za kifedha) na sekta ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Pensheni. Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma – *PSPF*. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mfuko umeendelea kusajili na kuhifadhi kumbukumbu za wanachama pamoja na kukusanya michango na kuiwekeza. Aidha, Mfuko ulikusanya jumla ya shilingi bilioni 527.22 ambapo kati ya makusanyo hayo, michango ya wanachama ni shilingi bilioni 449.99 na mapato yatokanayo na vitega uchumi ni shilingi bilioni 77.23. Kati ya hizo, shilingi bilioni 371.40 zilitumika kulipa mafao ikiwa ni pamoja na mafao ya kiinua mgongo na pensheni za kila mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mfuko unatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 718.30. Kati ya hizo, michango ya wanachama ni shilingi bilioni 590.19 na mapato yatokanayo na vitega uchumi ni shilingi bilioni 128.11. Mfuko unatarajia kulipa kiasi cha shilingi bilioni 452.93 kwa ajili ya mafao mbalimbali ikiwa ni pamoja na kiinua mgongo na pensheni za kila mwezi ambapo jumla ya wanachama 6,974 wanatarajia kustaafu kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 30 Juni 2012, Mfuko ulikuwa na thamani ya shilingi bilioni 1,071.19. Mfuko unatarajiwa kufikia thamani ya shilingi bilioni 1,438.29 ifikapo tarehe 30 Juni 2013. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 34.27.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini – *GEPF*. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini *(GEPF)* ulitekeleza majukumu yake kwa mafanikio makubwa. Thamani ya Mfuko imeongezeka kutoka shilingi bilioni 119.4 mwezi Juni, 2011 hadi kufikia shilingi bilioni 150 mwezi Juni 2012. Mapato yatokanayo na vitega uchumi yameongezeka kutoka shilingi bilioni 9.4 mwaka 2010/2011 hadi shilingi bilioni 10.9 kwa mwaka 2011/2012. Aidha, Mfuko umesajili wanachama wapya 10,401 kupitia mpango wa lazima na mpango wa hiari ambapo umeyafikia makundi mbalimbali ya wazalishaji mali wakiwemo wakulima, wafanyabiashara, wasafirishaji, wafugaji na waajiriwa. Mafanikio haya yametokana na juhudi za kuutangaza mfuko kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Aidha, hadi kufikia Juni 2012, Mfuko ulikua umelipa kiasi cha shilingi bilioni 4.09 kwa wanachama wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mfuko utaendelea kuboresha huduma kwa wanachama, kupanua wigo wa wanachama, kukuza mapato yatokanayo na uwekezaji na kusajili wanachama zaidi kupitia skimu zote mbili ambazo ni Teknolojia ya Habari na Mawasiliano pamoja na kuimarisha mpango wa hiari wa kujiwekea akiba ya uzeeni kwa kufungua ofisi tatu katika Manispaa za Dar es Salaam na kuimarisha ofisi zilizopo Mikoani. Lengo ni kusajili jumla ya wanachama 19,606 na

kukusanya michango inayofikia shilingi bilioni 35.21 ifikapo mwezi Juni, 2013. Vile vile, mapato yatokanayo na vitega uchumi yanatarajiwa kufikia shilingi bilioni 16 na thamani ya mfuko kufikia shilingi bilioni 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011, Mfuko wa Pensheni wa mashirika ya umma – *Parastatal Pension Fund (PPF),* Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma – *PPF* ulikusanya shilingi bilioni 188.1, ikiwa ni michango ya wanachama ambayo ni ongezeko la asilimia 27 ikilinganishwa na shilingi bilioni 147.65 zilizokusanywa mwaka 2010. Ongezeko hili lilitokana na waajiri kuzingatia sheria kwa kuleta michango kwa wakati na uandikishaji wa wanachama wapya. Katika kipindi cha Januari – Juni 2012, Mfuko ulikuwa umekusanya shilingi bilioni 112.3, ikiwa ni michango kutoka kwa wanachama. Kadhalika, mapato yatokanayo na uwekezaji yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 35.2 mwaka 2010 hadi shilingi bilioni 88.1 mwaka 2011, ikiwa ni ongezeko la asilimia 140. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa thamani ya Hisa za makampuni ambayo Mfuko umewekeza, kuongezeka kwa gawio kutoka makampuni mbalimbali, kuongezeka kwa mapato yatokanayo na vitega uchumi vya muda maalum pamoja na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na pango.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya wanachama wanaochangia katika Mfuko imeongezeka kutoka 160,068 mwaka 2010 hadi kufikia wanachama 180,049 mwaka 2011. Mfuko umelipa jumla ya shilingi bilioni 71.9 kwa mwaka 2011, ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.7 ikilinganishwa na shilingi bilioni 63.8 zilizolipwa mwaka 2010. Aidha, kufikia Desemba 2011, thamani ya Mfuko ilikuwa shilingi bilioni 896.1, ikiwa ni ongezeko la asilimia 24 ikilinganishwa na shilingi bilioni

722.47 mwezi Desemba 2010. Ongezeko hilo lilitokana na ziada ya shilingi bilioni 173.6 iliyopatikana kutokana na ukusanyaji wa michango pamoja na mapato yatokanayo na uwekezaji. Vilevile, thamani ya Mfuko hadi kufikia Juni, 2012 ilikuwa imefikia shilingi bilioni 989.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2013, Mfuko umejiwekea malengo ya kukusanya michango kutoka kwa wanachama ya kiasi cha shilingi bilioni 244 na mapato yatokanayo na uwekezaji ya shilingi bilioni 103.5 ili kuwezesha thamani ya mfuko kukua hadi kufikia shilingi bilioni 1,220.6 kutoka shilingi bilioni 1,058.7 mwaka 2012. Mfuko unatarajia kulipa mafao ya jumla ya shilingi bilioni 84.6 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2013. Aidha, Mfuko unategemea kuandikisha jumla ya wanachama 55,000 kutoka katika sekta ya umma na binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za kibenki. Benki Kuu ya Tanzania. Sekta ya benki imeendelea kuwa imara na benki nyingi zimekuwa na mitaji ya kutosha *(capital adequency*) pamoja na viwango vya juu vya ukwasi (*liquidity),* ikilinganishwa na viwango vinavyotakiwa kulingana na kanuni (*prudential guidelines).* Uwiano wa mtaji na mali iliyowekezwa (*core capital to total risk weighted assets and off-balance sheet exposures)* ulikuwa asilimia 17.5 mwezi Juni 2012 ikilinganishwa na kiwango cha chini kinachotakiwa kisheria cha asilimia 10.0. Uwiano kati ya mikopo na amana za wateja (*credit/deposit ratio*) ulikuwa asilimia 67.5, ikilinganishwa na kikomo cha asilimia 80.0. Vilevile, uwiano kati ya mikopo chechefu na jumla ya mikopo (*non performing loans/total loans*) yote katika mabenki ulipungua hadi kufikia asilimia 8.2 mwezi Juni 2012 kutoka asilimia 9.1 mwezi Juni 2011. Hali hii ni kithibitisho cha

uboreshaji wa urudishaji mzuri wa mikopo itolewayo na mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu imeimarisha na kuboresha mfumo wa malipo baina ya mabenki (*Tanzania Inter-bank Settlement System – TISS)* kwa kujumuisha malipo ya fedha za kigeni kupitia mfumo huu. Aidha, Bodi ya Mapato ya Zanzibar na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa upande wa Zanzibar zilianza kutumia mfumo huo. Hali hii ilisaidia kupunguza matumizi ya hundi za Serikali kutoka hundi 79,803 zenye thamani ya Shilingi bilioni 6,275.3 hadi hundi 55,838 zenye thamani ya shilingi bilioni 6,115.6. Vilevile, Benki Kuu imeanza kutumia mfumo wa malipo kwa njia ya elektroniki baada ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuidhinisha utaratibu utakaosimamia Mfumo wa Malipo kwa Nchi za Afrika Mashariki. Kadhalika, Kanuni za malipo kupitia simu za mkononi ziliboreshwa ili kuhakikisha malipo hayo yanafanyika kwa ufanisi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Benki Kuu imepanga kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la ukuaji wa wastani wa fedha ya msingi usiozidi asilimia 16.0 na wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) usiozidi asilimia 18.0, ili kutoa nafasi kwa mikopo kwa sekta binafsi kukua kwa asilimia 20.0. Aidha, Benki Kuu itatekeleza yafuatayo: kusimamia sekta ya fedha kwa lengo la kuhakikisha kuwa inaimarika kwa kuanzisha kiungo muhimu cha kuimarisha ushirikiano katika usimamizi na ufuatiliaji wa majanga mbalimbali katika mfumo wa kibenki; kutoa miongozo ya kuimarisha usimamizi wa huduma za kibenki kwa njia ya simu za mkononi nchini ili kuongeza ufanisi katika huduma

ya malipo na kuongeza biashara kati ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Mfumo wa Malipo wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Rasilimali Tanzania – *TIB*. Katika mwaka 2011/2012, Wizara imeendelea kuimarisha Benki ya Rasilimali kwa kutekeleza yafuatayo: kuanza utaratibu wa utekelezaji wa mfumo wa makampuni mawili yanayofanya kazi pamoja ambayo ni kampuni mama - Benki ya Maendeleo na kampuni tanzu - Benki ya Biashara; kufungua tawi la benki Mbeya ambalo limeanza kazi Mwezi Juni 2012 kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi. Aidha, katika kipindi kilichoishia Desemba 2011, Benki ya Rasilimali ilipata faida (kabla ya kodi) ya shilingi bilioni 5.8 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 2.2 ikilinganishwa na mwaka ulioishia Desemba 2010. Vilevile, waraka mizania wa benki ulikua kufikia shilingi bilioni 305.8 ikilinganishwa na shilingi bilioni 243.7 Desemba 2010; Mikopo iliongezeka kufikia shilingi bilioni 181.7 kutoka shilingi bilioni 106.1 Desemba 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia Julai 2011 hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 2012, Dirisha la Kilimo katika Benki ya Rasilimali lilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 14.23 na hivyo kufanya mikopo yote kufikia shilingi bilioni 33.71. Kati ya mikopo iliyoidhinishwa shilingi bilioni 6.88 zilienda kwa vikundi vya wakulima wadogo na *SACCOS* na hivyo kufanya jumla ya mikopo iliyotolewa kwa kundi hili kufikia shilingi bilioni 12.88, wakati shilingi bilioni 7.35 zilitolewa kwa makampuni na hivyo kufanya jumla ya mikopo iliyotolewa kwa kundi hili kufikia shilingi bilioni 15.35. Hadi mwezi Juni mwaka huu kiasi cha shilingi bilioni 2.76 ikijumuisha riba ya shilingi bilioni 0.79 kilikuwa kimerejeshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Benki ya Rasilimali itatekeleza mpango mkakati wake ambao umelenga kuwezesha uwekezaji katika shughuli mbalimbali zikiwemo za madini, uvuvi, mifugo, miundombinu, utalii, viwanda hususan usindikaji wa mazao ya kilimo. Aidha, Wizara itaendelea kuongeza mtaji wa *TIB* kadri hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya Posta Tanzania – *TPB*. Katika mwaka 2011, Benki ya Posta imeendelea kuboresha huduma ambapo amana za wateja ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 107.33 mwaka 2010 na kufikia shilingi bilioni 120.48 mwaka 2011, ikiwa ni ongezeko la asilimia 12.3. Aidha, idadi ya wateja iliongezeka kutoka 582,774 mwaka 2010 hadi kufikia 612,005 mwishoni mwa mwaka 2011. Thamani ya vitega uchumi vyote hadi Desemba 2011 iliongezeka na kufikia kiasi cha shilingi bilioni 121.0 kutoka shilingi bilioni 112.76 mwaka 2010, ikiwa ni ongezeko la asilimia 7.3. Vilevile, Benki iliendelea kutoa huduma za mikopo kwa wateja wake ambapo hadi kufikia Desemba 2011 uwekezaji kupitia mikopo ulikuwa na thamani ya jumla ya shilingi bilioni 66.75 kutoka shilingi bilioni 64.08 mwaka 2010, ikiwa ni ongezeko la asilimia 4.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho mapato yatokanayo na mikopo pamoja na riba katika dhamana za Serikali yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 24.28 ikilinganishwa na shilingi bilioni 20.29 zilizopatikana mwaka 2010. Hili ni ongezeko la asilimia 19.7 na hivyo kufanya faida ya Benki baada ya kodi kuongezeka kutoka shilingi bilioni 0.46 mwaka 2010 hadi shilingi bilioni 2.27 mwaka 2011. Aidha, benki ilipata mapato kutokana na kuingia katika

mkataba wa kukusanya kodi za ndani kwa niaba ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Benki inalenga kutekeleza yafuatayo: kuimarisha matumizi ya teknolojia ya *TPB* Popote kwa huduma ya benki kupitia simu za mkononi kwa lengo la kuwafikia Watanzania waishio vijijini; kuongeza idadi ya mikopo kwa kupanua wigo wa wateja ikiwa ni pamoja na kuingia mikataba na Halmashauri za Wilaya mbalimbali; na kuongeza mapato ya Benki kufikia shilingi bilioni 28.62. Lengo ni kupata faida baada ya kodi isiyopungua shilingi bilioni 3.56.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Twiga Bancorp Limited.* Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba 2011, *Twiga Bancorp Limited* iliendelea kutoa huduma mbalimbali na kuweza kukusanya mapato ya shilingi bilioni 10.0, ikilinganishwa na mapato ya shilingi bilioni 9.6 kwa mwaka uliotangulia, ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 0.4 sawa na asilimia 4.2. Aidha, amana za wateja ziliongezeka kufikia shilingi bilioni 54.2 kwa kipindi kilichoishia Desemba 2011 kutoka shilingi bilioni 48.2 kama ilivyokuwa Desemba 2010, ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 6.0 sawa na asilimia 12.4. Mpaka kufikia Desemba, 2011 mikopo iliyotolewa na *Twiga Bancorp Ltd* kwa wateja mbalimbali ilifikia shilingi bilioni 35.9, ikilinganishwa na shilingi bilioni 30.7 mwaka ulioishia Desemba 2010, ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 5.2 sawa na asilimia 16.9. Vilevile, hadi kufikia Desemba 2011, Taasisi ilikuwa imewekeza shilingi bilioni 19.0 kwenye Dhamana za Serikali na Amana katika Benki zingine ikilinganishwa na shilingi bilioni 20.5 mwaka ulioishia Desemba 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka utakaoishia Desemba 2012, Taasisi itatekeleza yafuatayo: kuimarisha huduma kwa kutumia Mashine za kutolea Pesa *'ATMs';* kuongeza matawi katika mji wa Dodoma na Jiji la Dar es Salaam; kuimarisha huduma mpya za kibiashara za kutoa mikopo kwa Sekta ya Viwanda na Biashara Ndogo na Kati pamoja na mikopo ya kulipia Bima za wateja na kubadilisha Muundo wa Taasisi kuwa Benki Kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi imejiwekea lengo la kukusanya na kukuza amana za wateja kufikia shilingi bilioni 69.9 kutoka shilingi bilioni 54.2 za Desemba 2011, hii ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 15.7 sawa na asilimia 28.9. Vilevile Taasisi imejiwekea lengo la kutoa mikopo kwa wateja mbalimbali kufikia shilingi bilioni 45.3 kutoka shilingi bilioni 35.9 Desemba 2011, hii ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 9.4 sawa na asilimia 26.2, kuwekeza fedha zenye thamani ya shilingi bilioni 17.8 katika Dhamana za Serikali na Amana za muda maalumu kwenye mabenki ikilinganishwa na Dhamana pamoja na Amana zenye thamani ya shilingi bilioni 7.1 mwaka 2011 ambalo ni ongezeko la shilingi bilioni 10.7 sawa na asilimia 150.7, na kupata faida kabla ya kodi ya shilingi billioni 0.82. Aidha, kutokana na shughuli za biashara kwa mwaka 2012 mtaji wa Benki unatarajiwa kukua kutoka shilingi bilioni 5.1 kama ilivyokuwa Desemba 2011 na kufikia shilingi bilioni 8.7 ifikapo Desemba 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Consolidated Holdings Corporation – CHC*. Katika kipindi kilichoishia Desemba 2011, *CHC* ilikusanya mapato yaliyofikia shillingi bilioni 6.3 sawa na asilimia 66 ya lengo. Upungufu huu wa mapato umetokana na kutopata gawio kutoka kwenye benki ya *NBC* ambapo shirika linasimamia asilimia 30 ya hisa kwa

niaba ya Serikali. Aidha, Shirika limesimamia kesi zilizoko Mahakamani pamoja na kufuatilia kwa karibu madeni yatokanayo na ubinafsishaji, madeni sugu ya iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara, shughuli za ufilisi wa mashirika ya umma na riba kutoka katika benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, shirika linatarajia kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 12.77 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na: uuzaji wa viwanja na majengo, ukusanyaji wa madeni chechefu, ukusanyaji wa madeni yanayotokana na ubinafsishaji, ufilisi wa makampuni na mapato yanayotokana na riba itakayotolewa na benki kwa amana zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za Bima. Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima – *TIRA*. Sekta ya Bima imeendelea kukua ambapo idadi ya makampuni, madalali na mawakala wa Bima imeongezeka kwa wastani wa asilimia 25. Mapato kutokana na ada ya bima yameongezeka kutoka shilingi bilioni 286.9 mwaka 2010 hadi shilingi bilioni 342.1 mwaka 2011 sawa na ongezeko la asilimia 19.2. Malipo ya madai ya bima nayo yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 136.4 mwaka 2010 hadi shilingi bilioni 137.4 mwaka 2011. Vitega uchumi vya bima viliongezeka kwa asilimia 16 kutoka shilingi bilioni 254.3 mwaka 2010 hadi shilingi bilioni 296.3 mwaka 2011. Aidha, Mamlaka imefungua ofisi mbili za kanda katika miji ya Arusha na Mwanza ili kusogeza huduma za usimamizi wa soko karibu na wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ikishirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, iko katika hatua za mwisho za

mchakato wa uanzishwaji rasmi wa mfumo wa uuzaji wa bima unaoshirikisha mabenki (*bancassurance*) kwa lengo la kuwafikia wateja wengi zaidi nchini. Ripoti ya Mtaalamu ya kuainisha njia bora zaidi ya uanzishwaji wa mfumo wa *'bancassurance'* hapa nchini imeshapokelewa na mamlaka husika na mapendekezo yaliyotolewa kufanyiwa kazi ili mapema iwezekanavyo mabenki yaweze kuruhusiwa kuuza bima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mamlaka itaandaa Kanuni zitakazosimamia utendaji wa Baraza la Usuluhishi la Bima. Aidha, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima itafungua ofisi katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, kwa lengo la kusogeza huduma za usimamizi wa soko karibu na wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Bima la Taifa *(NIC).* Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara iliendelea kulifanyia marekebisho Shirika la Bima la Taifa ili kuliwezesha kuongeza tija na hatimaye lianze kufanya biashara kwa faida. Katika kutekeleza malengo yake ya kuhakikisha kuwa madai halali yote ya bima yanalipwa kwa wakati, Shirika limesimamia ulipaji wa malimbikizo ya madai ya muda mrefu ya wateja wake ambapo jumla ya shilingi bilioni 25.32 zimelipwa katika mwaka wa 2011. Kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi bilioni 19.98 zilipatikana kutokana na kuuzwa kwa baadhi ya mali ya Shirika isiyoendana na biashara ya msingi (*non-core assets*) na shilingi bilioni 5.34 ni kutokana na mapato ya biashara (*premiums).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato ya Shirika la Taifa la Bima yatokanayo na vitega uchumi yameongezeka kutoka shilingi bilioni 6.0 mwaka 2010 hadi shilingi bilioni 16.47

mwaka 2011 ikiwa ni ongezeko la asilimia 174. Ongezeko hili lilitokana na mauzo ya nyumba na viwanja vya shirika visivyoendana na biashara ya msingi. Pato la Shirika kutokana na bima mtawanyo (*reinsurance Premium*) nalo liliongezeka kutoka shilingi bilioni 0.93 mwaka 2010 hadi shilingi bilioni 1.31 mwaka 2011 ikiwa ni ongezeko la asilimia 41. Kwa ujumla, mapato ya shirika kutoka vyanzo mbalimbali yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 32.91 mwaka 2010 hadi shilingi bilioni 44.38 mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara inalenga kuligawa Shirika katika makampuni mawili kwa mujibu wa Sheria ya Bima ya mwaka 2009 ambapo kampuni moja ni kwa ajili ya Bima za Maisha (*Life company*) na kampuni nyingine ni kwa ajili ya bima ya kawaida (*Non-life company*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Masoko ya Mitaji na Dhamana. Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana – *CMSA*. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ilitekeleza yafuatayo: kuanzisha mchakato wa kurekebisha Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania; kuratibu ushiriki wa wageni katika soko la mitaji; kutoa elimu kwa umma kupitia usambazaji wa vipeperushi na machapisho mbalimbali yenye elimu na ujumbe kuhusu soko la mitaji; kuweka taratibu za kuanzisha soko la Hatifungani za Serikali za Mitaa *(Municipal Bonds)* pamoja na Soko la Bidhaa (*Commodity Exchange*) nchini na; Soko la Kukuza Kampuni za Wajasiriamali; kushiriki katika kuboresha sheria za masoko ya mitaji ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na; kukamilisha maandalizi ya utekekezaji wa mapendekezo ya kuboresha biashara ya Hatifungani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana inatarajia kutekekeza yafuatayo: kuandaa Mpango Mkakati wa Mamlaka; kuendelea kutoa elimu kwa umma hususan kuwafikia wananchi walio vijijini; kuendelea kujenga masoko ya mitaji na dhamana kwa kuongeza bidhaa na washiriki; kuandaa sheria mpya ya masoko ya mitaji na dhamana; kuzindua soko la kampuni za ujasiriamali na soko la Hatifungani za Manispaa na Halmashauri za Serikali za Mitaa; kuendelea kuboresha biashara ya Hatifungani kwa kushirikiana na wadau wengine na kuweka mazingira yatakayowezesha uanzishwaji wa Soko la Bidhaa (*Commodity Exchange*) nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Soko la Hisa la Dar es Salaam – *DSE*. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 kampuni tatu ziliorodheshwa kwenye soko la hisa na kufanya soko hilo kufikisha jumla ya kampuni 18. Kampuni hizo mpya ni *National Media* Group *(NMG), African Barrick Gold (ABG)* na *Precion Air Services Ltd (PAL).* Aidha, kutokana na ongezeko la kampuni idadi ya wawekezaji iliongezeka kutoka 174,013 mwaka 2010/2011 hadi 180,882 mwaka 2011/2012. Fahirisi ya Soko la Hisa iliongezeka kutoka 1,264.49 mwezi Julai 2011 hadi 1,437.84 mwezi Juni 2012, sawa na ongezeko la asilimia nne (4%). Vilevile, thamani ya soko kwa ujumla (*Market capitalization*) iliongezeka kutoka shilingi bilioni 5,926.60 mwezi Julai 2011 hadi shilingi bilioni 12,772.79 mwezi Juni 2012, sawa na ongezeko la asilimia 116. Ongezeko hili kwa sehemu kubwa limechangiwa na Kampuni ya *African Barrick Gold* ambayo ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 5,396.73 wakati ikiorodheshwa

sokoni. Kwa upande wa hisa za makampuni, hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 44.4 ziliuzwa ikilinganishwa na lengo la kuuza hisa zenye thamani ya shilingi bilioni 54.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, *DSE* itaanza kutekekeza Mpango Mkakati wa Miaka Mitano kwa kufanya yafuatayo: kuanzisha hatifungani za akiba (*micro savings bond)* ambapo zitauzwa kwa viwango vya chini na kwa kupitia mtandao wa malipo kwa njia ya simu ili kuwafikia wananchi wengi haswa wa kipato cha chini (hadi vijijini); kueneza elimu ya masoko ya fedha kwa mapana zaidi (*financial inclusion and financial literacy strategy*); kukamilisha utafiti wa njia bora za kuwekeza mtaji; na kuboresha uongozi wa Soko la Hisa la Dar es Salaam ili kulifanya soko lijiendeshe kibiashara (*Demutualization)* na kuondokana na utegemezi kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania – *UTT*. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania ilitekeleza yafuatayo: kuhamasisha uwekaji wa akiba pamoja na dhana ya uwekezaji kupitia elimu kwa umma; kusimamia utendaji na ufanisi katika Ofisi zake za Kanda ili kuwafikia Watanzania wengi; na kuimarisha mafanikio yaliyofikiwa na mifuko minne ya uwekezaji wa pamoja iliyokwishaanzishwa yaani – Mfuko wa Umoja, Mfuko wa Wekeza Maisha, Mfuko wa Watoto na Mfuko wa Jikimu. Katika jitihada hizo, thamani ya vipande imeongezeka kiasi cha kuridhisha. Mfano, thamani ya kipande kimoja cha Mfuko wa Umoja kimepanda kutoka shilingi 180.53 mwezi Juni 2011 hadi shilingi 206.66 mwezi Juni 2012 sawa na ongezeko la asilimia 14.5 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Dhamana ya Uwekezaji Tanzania itatekeleza yafuatayo: kuanzisha Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja wa *Dollar Fund*; kuanzisha Kitengo cha uibuaji wa miradi na usimamizi wake; kuanzisha kitengo/dirisha la mikopo (*Microfinance division*) na kuhamasisha uelewa juu ya dhana ya uwekezaji kupitia elimu kwa umma kwa njia mbalimbali na kusimamia utendaji wa ufanisi katika Ofisi zake za Kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi za Kitaalam na Huduma Nyinginezo. Ofisi ya Taifa ya Takwimu - *NBS*. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilitekeleza majukumu yake ya kukusanya, kuchambua, kutunza na kusambaza takwimu zilizohitajika katika sekta mbalimbali nchini. Pamoja na majukumu hayo, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea na maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 kwa kukamilisha utengaji wa maeneo ya kuhesabia watu, kufanya Sensa ya Majaribio na kukamilisha nyaraka mbalimbali za Sensa yakiwemo madodoso na mwongozo wa namna ya kuwapata Makarani na wasimamizi wa Sensa katika Kamati za Sensa za Mikoa na Wilaya. Ofisi imeendelea na maandalizi ya eneo la kuingiza takwimu kwenye kompyuta, kufanya shughuli za uhamasishaji, kutoa mafunzo kwenye ngazi ya Taifa na kufanya vikao vya Sensa kwenye ngazi mbalimbali. Aidha, zoezi la ukamilishaji wa mapitio ya Takwimu za Pato la Taifa kwa bei ya mwaka 2007 linaendelea. Ofisi hii pia, inaendelea na utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi kwa mwaka 2011 ambayo pamoja na mambo mengine takwimu zake zitatumiwa na Serikali pamoja na

wadau wengine ili kujua kiwango cha umaskini wa kipato nchini tangu mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu imetekeleza Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu Tanzania uliopitishwa na Serikali mwezi Juni, 2010. Katika mpango huu, makundi ya kazi ya kisekta yameundwa ili kuboresha mfumo wa takwimu nchini. Aidha, marekebisho ya Sheria ya Takwimu, 2002 yanaendelea ili kuimarisha uratibu na usimamizi wa utoaji wa takwimu rasmi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Ofisi ya Taifa ya Takwimu itafanya Sensa ya Watu na Makazi tarehe 26 Agosti, 2012 pamoja na kufanya uchambuzi wa takwimu za sensa. Shughuli nyingine zitakazotekelezwa ni pamoja na: kukusanya, kuchambua, kutunza na kusambaza takwimu katika sekta mbalimbali nchini na kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Kuimarisha na Kuboresha Takwimu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sensa ya Watu na Makazi. Tarehe 26 Agosti, 2012 ni siku ya sensa ya watu na makazi. Sensa itafanyika nchini kote na ni ya tano tangu kuzaliwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1964. Kauli mbiu yake ni "SENSA KWA MAENDELEO, JIANDAE KUHESABIWA". Lengo kuu la Sensa ya mwaka 2012, ni kuchangia katika uboreshaji wa maisha ya Watanzania kwa kutoa takwimu sahihi na zinazoendana na wakati kwa ajili ya kutunga sera, kupanga mipango ya maendeleo na kuboresha utoaji wa huduma za jamii ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji na kutathmini utekelezaji wa programu na maendeleo ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sensa ya mwaka huu ina umuhimu wa kipekee kwa maendeleo ya nchi yetu kwa sababu takwimu zitakazokusanywa zitatumika kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Malengo ya Milenia ya mwaka 2015, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 kwa Tanzania Bara na mwaka 2020 kwa Tanzania Zanzibar pamoja na MKUKUTA kwa Tanzania Bara na MKUZA kwa Tanzania Zanzibar. Aidha, nitumie fursa hii kuwaomba viongozi wenzangu na wananchi kwa ujumla kushiriki na kuhakikisha kuwa tarehe 26 Agosti, 2012 tunahesabiwa bila kukosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi – *NBAA*. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu imetekeleza yafuatayo: kuendesha semina na kongamano 11 kuhusu matumizi ya viwango vya kimataifa vya utayarishaji na ukaguzi wa taarifa za hesabu; kuendelea kujenga uwezo wa *NBAA*; kuhariri mitaala pamoja na silabi ya taaluma ya uhasibu; kuendesha Programu ya Maendeleo Endelevu ya Kitaaluma ambapo jumla ya semina 11 ziliendeshwa; kusimamia ubora wa ukaguzi wa hesabu (*Audit Quality Review Scheme*) ambapo hadi Juni, 2012 makampuni 50 kati ya 156 yalikaguliwa katika awamu ya kwanza; na Kufanya usajili wa wahasibu na kutunza takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, *NBAA* imejipanga kutekeleza majukumu yake yakiwemo: kuendelea kufanya usajili wa watahiniwa, wanachama na makampuni ya uhasibu na ukaguzi; kufanya ukaguzi na kusimamia ubora wa kazi za ukaguzi;

kutoa miongozo ya viwango vya uhasibu na ukaguzi na kusimamia mradi wa maboresho ya Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu unaoendelea chini ya Mshauri Elekezi. Aidha, Bodi itaendelea na jukumu la kuendeleza taaluma ya uhasibu pamoja na awamu ya pili ya ujenzi wa Kituo cha Taaluma ya Uhasibu eneo la Bunju, Wilayani Kinondoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi – *PSPTB*. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (*Procurement and Supplies Professionals and Technicians Board*) ilitekeleza yafuatayo: kuboresha mazingira ya mafunzo kwa kutengeneza na kuzindua tovuti (www.psptb.go.tz) na kanzi data ya wataalam (*Professionals Management Information System - PMIS*); kusajili wataalamu 991 wa ngazi mbalimbali; kuendesha mafunzo ya kitaaluma ambapo warsha 18 ziliendeshwa katika mikoa 12. Aidha, Bodi imetahini jumla ya wanafunzi 4,532 ambapo 1,689 sawa na asilimia 37.3 walifaulu. Idadi ikijumuishwa na wale wahitimu wa iliyokuwa Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa *(NBMM)* inafanya wahitimu kufikia 19,629 kati ya watahiniwa 65,149.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Bodi itaendelea kutekeleza yafuatayo: kuendelea kuelimisha umma juu ya Sheria Namba 23 ya mwaka 2007 ya Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi na Kanuni zake; kuelimisha na kuhamasisha wataalamu wa ununuzi na ugavi wazingatie Sheria ya Ununuzi wa Umma (*PPA-2011*); kuongeza kiwango cha ufaulu wa wanachama toka kiwango cha sasa cha asilimia 37 hadi kufikia asilimia 45; kutafuta wabia watakaoweza kuipatia Bodi vitendea kazi, na kuboresha mazingira ya kazi; na kufanya upembuzi

yakinifu wa ujenzi kwenye kiwanja cha *PSPTB* kilichopo eneo la Luguruni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha iliendelea kutekeleza majukumu yafuatayo: kutoa leseni kwa waendeshaji wa michezo ya aina mbalimbali ya kubahatisha nchini; kusimamia taratibu za kisheria na kiufundi na ukaguzi wa mara kwa mara wa uendeshaji wa michezo ya kubahatisha ili kuhakikisha michezo hiyo inaendeshwa kwa mujibu wa sheria na kukamilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Na. 4 ya mwaka 2003 na Kanuni zake ili kuruhusu uanzishwaji wa michezo ya *"internet casino".* Aidha, Bodi imekusanya kodi inayofikia jumla ya shilingi bilioni 7.2 ikiwa ni asilimia 97 ya lengo la shilingi bilioni 7.4, ikiwa ni ongezeko la asilimia 16 ikilinganishwa na shilingi bilioni 6.2 zilizokusanywa mwaka 2010/2011. Hadi kufikia Juni, 2012, mapato ya Bodi yalifikia shilingi bilioni 5.43, ikiwa ni ongezeko la asilimia 42 ikilinganishwa na shilingi bilioni 3.8 zilizokusanywa kwa mwaka 2010/2011. Vilevile, Bodi imechangia kiasi cha shilingi milioni 382.6 katika Mfuko Mkuu wa Serikali, ikiwa ni ongezeko la asilimia 45 ikilinganishwa na mchango wa shilingi milioni 263.7 kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, Bodi inatarajia kukusanya kodi ya shilingi bilioni 13.5 ambayo ni ongezeko la asilimia 88 ikilinganishwa na shilingi bilioni 7.2 kwa mwaka 2011/2012. Ongezeko hili linatokana na ubunifu wa vyanzo vipya vya kodi pamoja na kuongezeka kwa vima vya tozo kwa michezo ya kasino. Vyanzo vipya vinavyotarajiwa kuchangia kuongezeka kwa kodi ni "*internet casino", sms lotteries na sports betting.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Asasi za Mafunzo -Taasisi ya Uhasibu Arusha – *IAA*. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Taasisi ya Uhasibu Arusha imetekeleza yafuatayo: kuanzisha Shahada ya Uzamili ya Fedha na Uwekezaji kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha *Coventry* cha Uingereza; kuandaa mitaala kwa ajili ya Stashahada tatu ambazo ni Stashahada ya Uzamili katika Benki na Fedha, Stashahada ya Uzamili katika Kompyuta na Stashahada ya Uzamili katika Ugavi na Usambazaji; kuweka Samani katika jengo jipya la maktaba; kuanzisha Kitengo cha Utafiti wa Teknolojia na kukamilisha Mfumo wa *Student Academic Register Information System (SARIS)* ambao utarahisisha upatikanaji wa taarifa zote za kitaaluma na fedha kwa wanachuo popote walipo kupitia mtandao. Aidha, Idadi ya wanachuo imeongezeka kutoka wanachuo 3,394 kwa mwaka 2010/2011 na kufikia 3,427 mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ushirikiano na Taasisi ya Teknolojia ya Birla kutoka India, Chuo kinatarajia kuanzisha Shahada tatu za Uzamili ambazo ni Shahada ya Uzamili katika Uhandisi wa Mifumo ya Kompyuta, Shahada ya Uzamili katika Matumizi ya Kompyuta na Shahada ya Uzamili katika Usalama wa Mifumo ya Kompyuta. Kwa sasa mitaala ya shahada hizo inahakikiwa na *NACTE*. Aidha, udahili wa wanafunzi katika stashahada tatu za uzamili ambazo mitaala yake imeshapitishwa na *NACTE* unatarajiwa kuanza katika mwaka wa masomo unaoanza Octoba 2012. Vilevile, Chuo kina mpango wa kuanzisha kituo cha elimu kwa masafa *(E-Learning Centre*). Idadi ya wanafunzi kwa mwaka 2012/2013 inatarajiwa kufikia 3,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Uhasibu Tanzania – *TIA*. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Taasisi iliendelea kuendesha kozi zake kuanzia ngazi ya Cheti, Diploma na Shahada katika fani za Uhasibu, Ununuzi na Ugavi, Rasilimali Watu na Uongozi wa Biashara. Katika kukidhi matakwa ya wadau wake, Taasisi imeendelea na mipango ya kuanzisha kozi ya Uhasibu wa Serikalini (*Public Sector Accounting)* na tayari zoezi la kuandaa mitaala limekamilika. Kuanzishwa kwa kozi hii kutatoa mchango mkubwa katika kutoa wahasibu wenye sifa za kufanya kazi Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Taasisi ya Uhasibu Tanzania imepanga kufungua tawi jipya katika Jiji la Mwanza. Kozi zitakazoendeshwa katika tawi hili ni katika fani za Uhasibu, Ununuzi na Ugavi, Rasilimali watu na Uongozi wa Biashara kwa ngazi ya cheti. Jumla ya wanachuo 600 wanatazamiwa kudahiliwa katika tawi hili. Aidha, Idadi ya wanachuo inatarajia kuongezeka kufikia 8,000 kutoka 6,500 ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Usimamizi wa Fedha – *IFM*. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, chuo kimelipa fidia kwa wanavijiji wa Msata na Kihangaiko Wilaya ya Bagamoyo kwa ajili ya kumiliki eneo la ekari 1,500 ambalo litatumika kuanzisha kampasi ya pili itakayoweza kudahili zaidi ya wanafunzi 15,000. Chuo pia, kimeendelea kutoa mafunzo ya uzamili kwa ushirikiano na Taasisi ya Biashara ya Kimataifa ya India, Chuo Kikuu cha Strathclyde (Scotland) pamoja na Chuo Kikuu cha Avinashilingam cha India. Aidha, udahili wa wanafunzi umeongezeka na kufikia 8,350 ikilinganishwa na wanafunzi 7,217 waliodahiliwa katika kipindi cha mwaka 2010/11. Vile vile, chuo kimeendelea na hatua za kupitia upya mitaala ili kukidhi mahitaji ya soko

katika ubora na viwango vya elimu ya juu ili kuwezesha kushindana na vyuo vikuu katika soko la ajira na wahitimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, chuo kinatarajia kutekeleza yafuatayo: kuanzisha shahada mpya za uzamili; kuanzisha kituo cha ufundishaji huko Mwanza; kuongeza na kuboresha mbinu za kukitangaza chuo na kuainisha maeneo ya utafiti na huduma kwa jamii ambayo chuo kinaweza kushirikiana na taasisi zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini – *IRDP*. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Chuo kimetekeleza yafuatayo; kutoa mafunzo ya muda mrefu katika program kumi za ngazi za Cheti, Stashahada, Shahada na Stashahada za Uzamili kwa wanafunzi wapatao 4,000; kuanzisha mafunzo ya cheti katika kituo cha Mwanza kwa wanafunzi 320; kujenga uwezo wa watumishi 166 na kuajiri watumishi wapya 14; kukamilisha maandalizi ya Taarifa za Kiuchumi na Kijamii kwa Wilaya za Kondoa, Kilosa na Gairo. Aidha, Chuo kimekamilisha maandalizi ya programu mbili za Shahada ya Uzamili katika Uchumi na Mipango ya Mazingira; kimetoa ushauri na uelekezi katika utayarishaji wa mipango mikakati kwa Halmashauri nne na kutekeleza mradi wa mfano wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi katika kijiji cha Chololo-Dodoma kwa ufadhili wa Jumuiya ya Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Chuo kitatoa mafunzo ya muda mrefu kwa kozi 12 katika ngazi ya Cheti, Stashahada, Shahada, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamili. Aidha, Chuo kitaanzisha kozi tatu mpya katika ngazi ya Shahada ya Uchumi wa Maendeleo, Mipango ya Rasilimali Watu na

Mipango Miji na Usimamizi wa Mazingira na kuendelea kutoa mafunzo ya programu ya Cheti na Stashahada katika kituo cha Mwanza. Vilevile, Chuo kitaendelea kukamilisha ujenzi wa jengo la pili la Taaluma, kuendelea kujenga uwezo wa watumishi wake na kuajiri watumishi wapya ili kuimarisha ubora wa mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika – *EASTC.* Chuo hiki kiliendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu ya Stashahada na Cheti cha takwimu kwa nchi zinazotumia huduma ya Chuo kwa mwaka 2011/2012. Wanafunzi 142 walisajiliwa kati ya hao 83 walisajiliwa kwa kozi ya cheti na 59 kwa Stashahada ya Takwimu ambapo wanawake ni asilimia 30 ya wanafunzi waliosajiliwa. Nchi zilizoleta wanafunzi na uwiano wa wanafunzi wote waliosajiliwa ni Afrika Kusini asilimia 23, Uganda asilimia nne (4%), Zambia asilimia tano (5%), Zimbabwe asilimia tatu (3%), Namibia asilimia moja (1%) na Tanzania asilimia 64. Aidha, Chuo kilianza maandalizi ya mtaala wa kutoa mafunzo ya awali (*Foundation Course)* kwa wanafunzi walioshindwa kupata alama za kutosha kuendelea na kidato cha tano na cha sita ili waweze kuendelea na masomo ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo kikiwa ni kituo cha Kanda cha Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)* katika kuhamasisha matumizi ya takwimu, kilitoa mafunzo yanayohusu uandaaji wa hesabu za mapato na matumizi ya Pato la Taifa kwa baadhi ya nchi za *SADC*. Mafunzo hayo yalilenga kujenga uwezo wa nchi hizo katika kuchambua vyanzo vya mapato kwa ajili ya kujumuishwa kwenye maandalizi ya hesabu za mapato na matumizi ya nchi hizo na kuwa na ulinganifu wa utendaji katika uandaaji

wa Pato la Taifa. Nchi zilizonufaika na mafunzo hayo ni Tanzania, Afrika Kusini, Botswana, Malawi, Mauritius, Lesotho, Swaziland, Zimbabwe, Angola na Msumbiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Chuo kitaongeza idadi ya kozi zinazotolewa kutoka mbili kufikia tano ambapo moja ya kozi hizo itafanywa kwa ushirikiano na Chuo cha takwimu cha Abidjan, Ivory Coast-ENSEA. Chuo kitaanza kutoa mafunzo kwa njia ya mtandao ili kuwezesha wahitaji wengi kusoma kwa gharama nafuu. Aidha, Chuo kitaendelea na kutekeleza Mpango Mkakati wake ikiwa ni pamoja na kuendelea kuimarisha rasilimali watu ili iendane na mahitaji ya ukuaji wa Chuo. Vilevile, Chuo kitaendelea na maandalizi ya mtaala wa Shahada ya Takwimu itakayoanza mwezi Oktoba, 2012. Sambamba na hilo, Mafunzo ya awali (*Foundation Course*) yataanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto na hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto ni kama ifuatavyo:-

(i) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa namba 9 ya mwaka 1982 (*Local Government Finances Act No. 9 of 1982)* haijaoanishwa na Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348;

(ii) Kudhibiti matumizi ya fedha za umma sambamba na kuongeza mapato ya Serikali;

(iii) Kuhuisha muundo wa utumishi wa kada ya Ukaguzi wa Ndani Serikalini ili ujumuishe taaluma nyingine mbali ya uhasibu;

(iv) Kuzingatia kanuni na taratibu zilizoainishwa kwenye Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania (MPAMITA);

(v) Kupunguza na kudhibiti mfumuko wa bei ambao umeongezeka kutoka asilimia 13 mwezi Julai 2011 hadi asilimia 17.4 mwezi Juni, 2012;

(vi) Kuwianisha uandaaji wa hesabu za majumuisho kutokana na Serikali Kuu kuandaa hesabu zake kwa utaratibu wa *"IPSAs Cash Basis"* wakati hesabu za Serikali za Mitaa zinaandaliwa kwa "*IPSAs Accrual Basis*";

(vii) Kuzingatiwa kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma;

(viii) Kuwa na watumishi wa kutosha na wenye weledi wa Ununuzi wa Umma na Ukaguzi wa Ndani;

(ix) Kupunguza hoja za ukaguzi;

(x) Kuondoa migongano ya Sheria ya Msajili wa Hazina na Mashirika anayoyasimamia; na

(xi) Kuwa na Sera ya Mali ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na changamoto nilizozitaja, hatua zifuatazo zimechukuliwa:-

(i) Kuoanisha Sheria ya Fedha ya Serikali Kuu na Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ili kuondoa ukinzani uliopo;

(ii) Kuendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na usimamiaji wa mapato yasiyo ya kodi, hususan maduhuli ya Serikali (*retention),* ikiwa ni pamoja na kuboresha mfumo wa ukusanyaji kodi ya majengo;

(iii) Kuendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazotoa misamaha ya kodi;

(iv) Kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuendeleza juhudi za kuhuisha kada ya ukaguzi wa ndani;

(v) Kuendelea kuimarisha mfumo wa majadiliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo katika ngazi zote kama ulivyoainishwa kwenye MPAMITA;

(vi) Kutekeleza awamu ya nne ya Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma;

(vii) Kuendelea kujenga uwezo wa uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa bajeti katika ngazi zote za Serikali;

(viii) Kuendelea kusimamia udhibiti wa mfumuko wa bei;

(ix) Kuendelea kuimarisha mfumo wa malipo kwa njia ya elektroniki na kutoa mafunzo kwa watumiaji;

(x) Kufanya mafunzo ili kuwezesha uaandaaji wa hesabu kwa kutumia utaratibu wa “*IPSAS Accrual Basis*”;

(xi) Kuimarisha vitengo vya Ukaguzi wa Awali (*Pre – Audit*) na Ukaguzi wa Ndani kwa kuviongezea maafisa wenye ujuzi na sifa;

(xii) Kukamilisha mchakato wa kuandaa Sheria ya Msajili wa Hazina; na

(xiii) Kuandaa Sera ya Mali ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapato na Matumizi hya Mafungu ya Wizara kwa Mwaka 2011/2012. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ilipanga kupata mapato ya shilingi bilioni 206.48 kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato yasiyo ya kodi kupitia Fungu hili. Hadi kufikia Juni, 2012, Fungu 50 - Wizara ya Fedha lilikusanya mapato yasiyo ya kodi kiasi cha shilingi bilioni 214.62 sawa na asilimia 103.9 ya lengo. Kuvukwa kwa lengo kumetokana na kupata gawio kutoka Benki Kuu ambalo ni kubwa kuliko matarajio pamoja na baadhi ya taasisi ambazo hazikuwa zikichangia kuweza kuchangia kutokana na kuhamasishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya matumizi ya kawaida kwa mwaka 2011/2012 yalikuwa shilingi bilioni 113.67, kati ya hizo shilingi bilioni 4.32 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 109.35 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Juni, 2012, matumizi ya kawaida yalifikia shilingi bilioni 102.17. Kati ya matumizi hayo, shilingi bilioni 4.09 yalikuwa ni matumizi ya mishahara na shilingi bilioni 98.08 yalikuwa ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya matumizi ya bajeti ya maendeleo yalikuwa jumla ya shilingi bilioni 659.0. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 588 ni kwa ajili ya miradi ya *Millenium Challenge Account Tanzania* ikiwemo miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ya Usafirishaji, Nishati na Maji. Hadi kufikia Juni, 2012, matumizi yalikuwa shilingi bilioni 402.71, kati ya hizo fedha za ndani ni shilingi bilioni 78.65 na fedha za nje ni shilingi bilioni 324.06.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato yanayokusanywa na Fungu 21 – Hazina, Fungu hili yalifikia shilingi bilioni 6,511.2, sawa na asilimia 104.5 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 6,228.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2011/2012, bajeti ya Fungu 21 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ilikuwa shilingi bilioni 1,003.07. Kati ya fedha hizo mishahara ni shilingi bilioni 1.79 na matumizi mengineyo shilingi bilioni 1,001.28, ambapo, shilingi bilioni 162.41 ni matumizi ya idara na taasisi zilizo chini ya fungu hili, shilingi bilioni 394.87 ni nyongeza ya mishahara ya watumishi wa Serikali, shilingi bilioni 129.76 ni dharura na michango ya kisheria ya mwajiri, na shilingi bilioni 314.24 ni matumizi maalum. Hadi kufikia Juni, 2012 matumizi ya kawaida yalikuwa ni shilingi bilioni 1,002.73, kati ya hizo shilingi bilioni 175.00 ni kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo ya idara na taasisi zilizo chini ya fungu hili na shilingi bilioni 827.73 ni kwa ajili ya nyongeza ya mishahara ya watumishi wa Serikali, matumizi maalum na dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, bajeti ya Fungu 21 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ilikua shilingi

bilioni 51.49. Hadi kufikia Juni, 2012 matumizi ya fedha za maendeleo yalifikia shilingi bilioni 43.50. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 24.04 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 19.46 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 22 – Deni la Taifa. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, bajeti ya Fungu hili ilikuwa shilingi bilioni 2,526.08. Kati ya fedha hizo, malipo ya deni la ndani ni Shilingi bilioni 1,680.99, malipo ya deni la nje ni Shilingi bilioni 171.69 na *CFS Others* ni Shilingi bilioni 673.40. Hadi kufikia Juni, 2012 matumizi ya Fungu hili yalifikia shilingi bilioni 2,525.91.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, bajeti ya matumizi ya kawaida kwa Fungu hili ilikuwa shillingi bilioni 82.97, kati ya fedha hizo, mishahara ni shilingi bilioni 3.27 na shilingi bilioni 79.70 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Juni, 2012 matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 73.75.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, bajeti ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 6.86 na matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 6.64, kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi bilioni 4.19 na fedha za nje ni shilingi bilioni 2.45.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, bajeti ya Fungu hili kwa matumizi ya kawaida ilikuwa shilingi bilioni 34.75. Hadi kufikia Juni, 2012 matumizi ya kawaida yalifikia shilingi bilioni 34.54.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, bajeti ya maendeleo kwa Fungu hili ilikuwa shilingi bilioni 13.40 kati ya hizo fedha za ndani ni shilingi bilioni 7.55 na fedha za nje ni shilingi bilioni 5.85. Hadi kufikia Juni, 2012 matumizi ya maendeleo yalifikia shilingi bilioni 8.08 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 3.89 ni fedha za nje na shilingi bilioni 4.19 fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/13, Wizara kupitia Fungu 50 inakadiria kukusanya mapato yasiyo ya kodi yapatayo shilingi 124,420,645,627 (bilioni 124.42).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/13, Wizara kupitia Fungu 21 - Hazina inakadiria kukusanya mapato ya kodi yapatayo shilingi 8,070,088,000,000 (bilioni 8,070.09).

Mheshimiwa Naibu Spika, Maombi ya Fedha, Fungu 50 – Wizara ya Fedha. Katika fungu hili kwa mwaka 2012/13, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

Matumizi ya kawaida shilingi 98,412,912,000 (bilioni 98.41). Kati ya hizo Mishahara ni shilingi 5,852,488,000 (bilioni 5.85) na matumizi mengineyo shilingi 92,560,424,000 (bilioni 92.56).

(a) Miradi ya Maendeleo shilingi 546,514,113,000 (bilioni 546.51). Kati ya hizo:-

(i) Fedha za Ndani - shilingi 105,532,000,000 (bilioni 105.53).

(ii) Fedha za Nje - shilingi 440,982,113,000 (bilioni 440.98).

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2012/2013, Fungu 21 - Hazina. Katika Fungu hili kwa mwaka 2012/2013, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida shilingi 725,574,648,000 (bilioni 725.57). Kati ya hizo, mishahara ni shilingi 2,508,628,000 (bilioni 2.51) na matumizi mengineyo shilingi 723,066,020,000 (bilioni 723.07) ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya Idara na Taasisi zilizo chini ya Fungu hili, nyongeza ya mishahara ya Watumishi wa Serikali, pamoja na matumizi maalum.

(b) Miradi ya maendeleo ni shilingi 101,955,582,000 (bilioni 101.95) kati ya hizo:-

(i) Fedha za Ndani – shilingi 82,680,039,000 (bilioni 82.68).

(ii) Fedha za Nje – shilingi 19,275,543,000 (bilioni 19.27).

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 22 – Deni la Taifa. Katika Fungu hili kwa mwaka 2012/2013, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 2,735,909,673,000 (bilioni 2,735.91). Kati ya hizo deni la nje ni shilingi 373,255,893,000 (bilioni 373.26), deni la ndani ni shilingi 1,583,275,874,000 (bilioni 1,583.27) ikijumuisha kiasi cha shilingi 1,148,106,884,000 (bilioni 1,148.11) kwa ajili ya kulipia hatifungani zinazoiva *(Roll-over)* na *CFS Others* shilingi 779,377,906,000 (bilioni 779.38).

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali. Katika Fungu hili kwa mwaka 2012/2013, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya Kawaida - shilingi 75,128,765,000 (bilioni 75.12). Kati ya hizo Mishahara shilingi 4,731,503,000 (bilioni 4.73) na matumizi mengineyo shilingi 70,397,262,000 (bilioni 70.39).

(b) Miradi ya Maendeleo – shilingi 6,122,840,000 (bilioni 6.12) Kati ya hizo:-

(i) Fedha za ndani - Shilingi 3,500,000,000 (bilioni 3.50).

(ii) Fedha za Nje - shilingi 2,622,840,000 (bilioni 2.62).

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha. Katika Fungu hili kwa mwaka 2012/2013, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 1,998,246,200 (bilioni 1.99) kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 296,593,000 (bilioni 0.29) ni kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo shilingi 1,701,653,000 (bilioni 1.70).

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 13 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi. Katika Fungu hili kwa mwaka 2012/2013, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya kawaida - shilingi 2,163,807,000 (bilioni 2.16). Kati ya fedha hizo Mishahara shilingi 219,017,000 (bilioni 0.22) na matumizi mengineyo shilingi 1,944,790,000 (bilioni 1.94).

(b) Miradi ya Maendeleo, fedha za nje shilingi 267,800,000 (bilioni 0.27).

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Katika Fungu hili kwa mwaka 2012/2013, Wizara inaomba kuidhinishiwa kiasi cha fedha kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya kawaida shilingi 55,018,106,000 (bilioni 55.02). Kati ya hizo mishahara ni shilingi 7,980,773,000 (bilioni 7.98) na matumizi mengineyo shilingi 47,038,333,000 (bilioni 47.04).

(b) Miradi ya maendeleo shilingi 9,623,927,000 (bilioni 9.62), kati ya hizo:

(i) Fedha za ndani shilingi 7,500,000,000 (bilioni 7.50).

(ii) Fedha za nje shilingi 2,123,927,000 (bilioni 2.12).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Sasa niende moja kwa moja kwa sababu ya muda kuwa mdogo, naomba nimwite Mheshimiwa Dunstan Luka

Kitandula, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2012/2013: Fungu 50 – Wizara ya Fedha, Fungu 21- Hazina, Fungu 22 – Deni la Taifa, Fungu 23 – Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha na Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye ameniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi ilikutana na Wizara ya Fedha kwa nyakati tofauti na kupokea maelezo ya muhtasari wa Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013. Aidha, Kamati ilipokea Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara hiyo na mafungu yake kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012. Katika kikao hicho Waziri wa Fedha alitoa maelezo kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka wa Fedha 2011/12, changamoto za utekelezaji wa kipindi cha mwaka 2011/2012, malengo na maeneo ya vipaumbele pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012. Napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Wizara ya Fedha kwa kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka uliotangulia ikiwa ni pamoja na mipango mizuri waliyojiwekea kwa mwaka huu wa fedha. Ni matumaini ya Kamati kuwa katika mwaka huu wa fedha 2012/2013; Wizara itajitahidi kufikia malengo yake kwa usahihi na kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeendelea kutoa maoni, ushauri na maelekezo ambayo Wizara ya Fedha imeendelea kuyazingatia katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yake ya msingi. Majukumu hayo ni kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla; kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani na nje pamoja na matumizi ya Serikali; kufuatilia mipango ya kupunguza umaskini; kusimamia deni la Taifa; upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya miradi ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi; kusimamia Sheria, Kanuni na taratibu za Uhasibu, Ukaguzi wa Ndani Serikalini, ununuzi wa umma na usimamizi wa mali za Serikali. Aidha, Wizara ya Fedha imeendelea kushirikiana na Tume ya Mipango katika kutekeleza mipango ya maendeleo iliyoainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2011/2012 hususani katika kutekeleza Sera za Kodi, bado Wizara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Na.9 ya mwaka 1982 haijawianishwa na Sheria ya Fedha za Umma (SURA 348);

(ii) Kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za Umma sambamba na kuongeza mapato ya Serikali;

(iii) Kupunguza na kudhibiti Mfumuko wa Bei ili urudi kwenye viwango vya tarakimu moja;

(iv) Kuondoa upungufu uliopo katika Sheria ya Msajili wa Hazina na Sheria zilizoanzisha Asasi na Mashirika mbalimbali ya Umma;

(v) Kutokuwa na watumishi wa kutosha na wenye weledi katika masuala ya Ununuzi wa Umma na Ukaguzi wa Ndani;

(vi) Uwepo wa Matumizi ya fedha nje ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge;

(vii) Kutozingatiwa ipasavyo kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma; na

(viii) Kutokuwa na Sera ya Mali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto hizi, Wizara imejitahidi kuchukua hatua mbalimbali kukabiliana nazo ikiwa ni pamoja na: kukusanya mapato ya ndani kiasi cha shilingi trilioni 6.4 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi trilioni 6.3 katika mwaka wa fedha 2010/2011; Sheria ya Ununuzi wa Umma tayari imehuishwa kwa kutunga sheria mpya; Kujenga uwezo wa uandaaji wa bajeti kwa wakati;

Kusimamia kwa karibu deni la taifa; Kusimamia na kuhakiki malipo ya mishahara ya watumishi wa Serikali na Taasisi zake; Kufanya ukaguzi wa ndani pamoja na kwa miradi ya maendeleo; Kuimarisha mtandao wa malipo – *IFMS* katika ngazi zote; na kukamilisha kanuni na taratibu za ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya ubia pamoja na kuainisha miradi ya mwanzo itakayotekelezwa kwa njia ya ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi katika maeneo ya miundombinu, uzalishaji wa mazao ya chakula na utoaji wa huduma za kijamii kama vile usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa Fedha 2011/2012 pamoja na changamoto katika kutekeleza mpango na bajeti ya mwaka wa fedha wa 2012/2013. Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2011/2012, Kamati ya Fedha na Uchumi ilitoa maoni na ushauri juu ya utekelezaji katika maeneo mbalimbali ya kukuza uchumi hasa yale yaliyohusu Matumizi ya Serikali pamoja na Ukusanyaji wa Mapato; Misamaha ya Kodi; Manunuzi ya Umma; Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(Public Private Partnership)* na Urasimu uliopo katika kutekeleza wa miradi ya maendeleo. Kamati iliridhika na utekelezaji wa baadhi ya ushauri iliyoutoa kwa Wizara na hivyo kuliomba Bunge lako Tukufu lipitishe makadirio ya Wizara hii. Hata hivyo, bado yapo maeneo yanayohitaji kuangaliwa ili kuendeleza ufanisi na tija katika utekelezaji wa kuinua uchumi wa nchi pamoja na nidhamu ya matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwanzoni mwa Bunge hili, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kujadili kwa ndani taarifa zote za hali ya uchumi na ile ya mwelekeo wa bajeti zilizotolewa na Serikali pamoja na Mpango wa Maendeleo

wa Taifa kwa Mwaka 2012-2013. Taarifa hizi kwa ujumla wake zimebainisha mfumo wa uchumi mkuu na jinsi gani vipaumbele na mikakati itatekelezwa kupitia utengaji wa rasilimali baina ya sekta mbali mbali. Ni muhimu Wizara ya Fedha ikajipanga ipasavyo ili kuhakikisha kuwa fedha zilizopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa mipango na programu mbalimbali zinapelekwa kwenye sekta husika kwa wakati na kwa kuzingatia ratiba ya utekelezaji pamoja na upatikanaji wa fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa mipango na programu hizo. Usimamizi madhubuti na ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wa vipaumbele hivi pamoja na nidhamu ya matumizi ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya vipaumbele hivyo itakuwa ndio nguzo kuu ya mafanikio ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati na Waziri wa Fedha, Deni la Taifa *(debt stock)* katika kipindi kilichoishia Machi 2012 limeongezeka na kufikia shilingi bilioni 20,276.6 kutoka shilingi bilioni 17,578.9 kwa kipindi kilichoishia Machi 2011. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 15.4. Kati ya deni hilo la nje ni shilingi bilioni 15,306.9 na shilingi bilioni 4,969.7 ni deni la ndani. Kamati inatambua kwamba kutokana na mahitaji makubwa ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo ikilinganishwa na mapato ya ndani, Serikali imekuwa ikikopa na itaendelea kukopa kwa ajili ya kugharamia ya maendeleo na hivyo kusababisha Deni la Taifa kuongezeka. Angalizo la Kamati ni kwamba ongezeko la Deni la Taifa haliendani na kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Mfano Uchumi wa nchi yetu (*GDP growth rate)* tangu 2008/2009 hadi 2011/2012 umeongezeka kwa wastani wa asilimia 6.5 tu, wakati Deni la Taifa limeongezeka kwa

asilimia 15.4. Hali hii isipodhibitiwa upo uwezekano mkubwa wa Deni hilo kutokuwa himilivu kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba tathmini ya uhimilivu wa deni la taifa iliyofanywa mwaka 2011 inaonyesha kuwa deni hilo linahimilika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuzingatia mambo yafuatayo:-

(i) Ni muhimu Serikali ikachukua hatua ili kudhibiti kasi kubwa ya madeni yanayotokana na dhamana za Serikali;

(ii) Kuendelea kuwa na sera nzuri *(prudent)* za bajeti na fedha *(fiscal and monetary policies);*

(iii) Kutekeleza kwa dhati Mpango wa Maendeleo wa Taifa utakaohakikisha ukuaji wa kasi zaidi wa uchumi utakaowezesha pato halisi la Taifa kufikia asilimia 7.0 katika mwaka huu wa fedha na baadaye ukuaji huo kuendelea kupanda hadi kufikia asilimia 8.5 na hata zaidi ya hapo; na

(iv) Kuchukua uamuzi wa makusudi ili kupunguza mikopo ya kibajeti pamoja na na kuendelea kupanua wigo wa makusanyo katika maeneo mbalimbali pamoja na kurasimisha hatua kwa hatua sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hizi ndiyo zitahakikisha uchumi unakua kwa kasi na hivyo kujenga mazingira rafiki yatakayowezesha deni la taifa sio tu kuwa stahimilivu bali kuonekana kwa dhahiri kuwa stahimilivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu deni la Serikali la ndani pamoja na kukubaliana na utaratibu wa Serikali wa kuendelea kukusanya madeni yote kwa lengo la kuyahakiki

na kisha kuweka utaratibu wa kuyalipa, uzoefu unaonyesha kuwa zoezi hili lina mlolongo mrefu unaolalamikiwa kuchelewesha malipo kwa watumishi na wazabuni mbalimbali. Kwa kuwa ucheleweshaji wa muda mrefu wa malipo stahiki kwa madai ya watumishi na wazabuni unaathiri mzunguko wa fedha na kupelekea baadhi ya wazabuni kufilisika, Kamati inaishauri Serikali kuangalia kwa karibu eneo hili. Aidha, Kamati inapendekeza Serikali iweke kipindi maalumu cha kulipa madeni yaliyohakikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi ilikutana na wadau mbalimbali wakati wa vikao vya Kamati mjini Dar es Salaam na wakati wa kupitia na kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2012. Kilio cha wadau hasa wenye viwanda nchini ni kwamba tofauti na miaka ya nyuma safari hii Serikali imeamua kuweka viwango vya juu sana vya ushuru wa bidhaa za maji baridi, bia, sigara, soda na kadhalika. Huko nyuma ushuru wa bidhaa ulikuwa hauzidi asilimia 10. Safari hii ushuru wa bidhaa umepanda kati ya asilimia 20 na 25 kwa vinywaji baridi na bia. Hali hii yawezekana ikaikosesha Serikali mapato ambayo yalitarajiwa kupatikana katika mwaka huu wa fedha kwa sababu madhara ya ushuru wa bidhaa kwa kodi nyingine ni makubwa. Wadau hawa wamekuwa wakilalamika kuwa Serikali imekuwa ikitoza ushuru wa bidhaa *'excise duty'* kama njia mojawapo ya kuongeza mapato ya Serikali na sio kama inavyofikirika kuwa ni kwa ajili ya bidhaa za anasa. Ukweli ni kwamba hali hii inatokana na Serikali kung'ang'ania vyanzo vichache vya mapato vilivyozoeleka kila mwaka. Mfano mzuri ni ushuru wa bidhaa unaotozwa kwenye bidhaa za sigara, bia, soda na maji ya chupa. Pia ugonjwa huu unaonekana kuhamia kwenye eneo la kusindika maji ya matunda (*juice).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliweka sera nzuri ya kuhakikisha wananchi wake wanapata maji safi na salama. Hata hivyo kwa miaka ya hivi karibuni inaonekana sera hii imeanza kuvurugwa na Serikali kuanzia bajeti yake ya mwaka 2010/2011. Mfano mzuri ni kwamba Serikali kupitia Muswada wake wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2012 inatoa picha kuwa maji ni bidhaa ya anasa. Itakumbukwa kuwa tangu miaka ya 1990 bidhaa ya maji ya chupa ilikuwa haitozwi ushuru wa bidhaa ili kutekeleza sera ya Serikali ya kuwapa wananchi wake maji safi na salama. Hata hivyo, mwaka 2010 Serikali iliamua kuanza kutoza kodi ya ushuru wa bidhaa hii kutoka 0 kwenda TShs.12 kwa lita. Mwaka 2011/2012, ushuru huu ulipandishwa kutoka TShs.12 kwa lita hadi Tshs.69 kwa lita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi hicho, Kamati ilikubaliana na pendekezo hili kwa shingo upande ili kuiwezesha Serikali kupata mapato yake. Hata hivyo, Serikali ilitoa ahadi yake Bungeni kwamba ingefanyia marekebisho suala hili na ni kweli wakati wa Bunge la Mwezi Aprili, Serikali ilikuja na pendekezo la kupunguza makali ya maisha ya wananchi kwa kupunguza ushuru wa bidhaa hii kutoka TShs.69 kwa lita hadi TShs.12 kwa lita hata hivyo pendekezo hili lilipingwa na Wabunge kwa sababu hatua hiyo isingeweza kuwa na *impact* ya kupunguza makali ya maisha, hivyo ushuru huu ukaendelea kutozwa TShs.69 kwa lita.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka huu wa Fedha 2012/2013, Kamati ilitegemea kuwa Serikali ingekuja na hoja ya kutaka kuitetea sera yake ya maji safi na salama kama ilivyokusudia kwa kupunguza ushuru wa bidhaa za maji ya

chupa kutoka TShs.69 kwa lita hadi TShs.12 kwa lita au ingebaki TShs.69 kwa lita kama ilivyokuwa kwenye Bunge liliopita. Kinyume na matarajio hayo, Serikali imekuja na mapendekezo ya kuongeza ushuru huu wa bidhaa kutoka TShs.69 hadi TShs.83 kwa lita. Hii ni udhibitisho tosha kwamba muono wa Serikali ni kwamba maji ya chupa ni bidhaa ya anasa na hivyo inastahili kutozwa kodi ya juu. Kamati inaishauri Serikali kufikiria upya suala hili la kuongeza ushuru wa bidhaa kwa kiwango cha juu kwani hatua hii isipodhibitiwa tutakuwa na athari ya kudumaza uzalishaji wa viwanda vya ndani na hivyo kupunguza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikari kuwa kwa mwaka ujao wa Fedha 2013/2014 itenge fedha za kutosha kwa Tume ya Mipango ili kuipa uwezo wa kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado thamani ya shilingi ya Tanzania inayumba. Ni vema Serikali kupitia vyombo vyake vya fedha ikahakikisha kuwa hali hii inadhibitiwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali juu ya dhana nzima ya umuhimu wa kudhibiti na kusimamia matumizi ya Serikali ambayo yanaendelea kupanuka kwa kasi kubwa ikiwa ni pamoja kuendelea kuimarisha sera za mapato na matumizi, pamoja na maboresho mbalimbali katika sekta ya Umma ili kuleta ufanisi na tija na kuhakikisha kuwa Mafungu ya kila Wizara yanayoidhinishwa na Bunge yanatekelezwa kwa kuzingatia viwango vya matumizi vinavyoidhinishwa na Bunge hasa kwa miradi ya maendeleo na hivyo kuongeza juhudi za Serikali za kukuza uchumi na kupunguza umaskini. Kamati

inaendelea kusisitiza, Serikali ichukue hatua madhubuti za kuongeza mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuangalia eneo la sera na uendeshaji wa taratibu za kukusanya kodi;

(ii) Kuimarisha uzalishaji na ubora wa bidhaa za ndani na kuweza kuuza nje ya nchi ili kuongeza fedha za kigeni;

(iii) Kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini;

(iv) Kuhakikisha kuwa mashirika na taasisi za umma zinachangia katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa kuzingatia Sheria ya Fedha Na.13 ya mwaka 2008;

(v) Kupanua wigo wa kukusanya kodi katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta isiyo rasmi ambayo inakua kwa kasi;

(vi) Kuimarisha taratibu za kutoza na kukusanya kodi ya majengo *(property tax)* katika maeneo ya miji na majiji;

(vii) Kupitia upya utaratibu wa kutoa misamaha ya kodi kwa madhumuni ya kushusha misamaha hiyo angalau iwe asilimia moja (1%) ya Pato la Taifa kama Kamati ilivyopendekeza huko nyuma; na

(viii) Kuendelea kuhimiza uanzishwaji wa viwanda vya kusindika mazao hasa mazao ya kilimo ili kuongeza thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea kufanya Sensa ya Watu na Makazi mwezi huu, 2012. Kamati inatoa angalizo kwa Serikali kuhakikisha kuwa dosari zote ndogondogo zilizojitokeza wakati huu wa maandalizi hasa kwa upande wa malipo ya wasimamizi na upatikanaji wa vifaa zinarekebishwa haraka ili zoezi hilo lifanyike kwa ufanisi mkubwa. Kamati inatoa wito kwa wananchi wote kushiriki kikamilifu katika zoezi hili muhimu kwa kuwa upatikanaji wa takwimu hizi zitaiwezesha Serikali kupanga mipango ya maendeleo kwa uhakika na pia kuandaa sera mbalimbali zenye manufaa kwa jamii nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuwepo kwa wafanyakazi hewa ni changamoto kubwa kwa Serikali. Katika bajeti ya Serikali ya Mwaka 2011/2012, Bunge lako Tukufu lilielezwa kwamba Serikali ilikuwa imedhamiria kwa dhati kuchukua hatua mbalimbali za kudhibiti matumizi ikiwa ni pamoja na kuimarisha ukaguzi wa mishahara *(payroll audit)* ambapo Maafisa Masuuli wangekabidhiwa jukumu la kufanya ukaguzi wa malipo ya mishahara ya taasisi zao kila mwezi na kwamba chini ya utaratibu huo wa Wakuu wa Idara na Maafisa Wahasibu wangewajibishwa kwa malipo ya mishahara hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inahoji umakini na uwezo wa baadhi ya watendaji wa Serikali katika kusimamia na kutekeleza majukumu yao. Mfano katika uhakiki wa watumishi uliofanyika mwezi Januari 2012 kwenye Halmashauri 133 na kwenye Taasisi na Wakala za Serikali 154 majina 9,949 ya watumishi wasiostahili kuwemo kwenye orodha ya mishahara yalibainika na hivyo kuondolewa kwenye orodha hiyo. Tunapongeza kwa hatua hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za

kunidhamu dhidi ya watumishi wote wa Serikali wanaohusika katika ubadhirifu wa fedha za umma kupitia ulipaji wa mishahara ya wafanyakazi hewa ikianzia na kundi lililosababisha kuwepo kwa majina ya watumishi hewa 9,949. Serikali lazima itekeleze na ionekane inatekeleza dhamira yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa Serikali kwa kipindi kijacho, itafute maeneo mbadala ya kupata mapato kupitia bajeti ya Serikali kwa ajili ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu badala ya kutumia utaratibu huu wa sasa wa kukata asilimia nne (4%) kutoka asilimia sita (6%) zinazokatwa kama *Skills and Development Levy* zinazochangiwa na sekta binafsi pekee. Kwa upande wa *SDL*, Kamati inaendelea kushauri kwamba kwa kuanzia tozo hii ipungue kutoka asilimia sita (6%) hadi nne (4%) na wigo wa walipaji upanuliwe kwa kuhusisha baadhi ya taasisi na wakala wa Serikali na mgawanyo uwe kama hivi ifuatavyo: asilimia mbili (2%) ipelekwe *VETA* kama inavyofanyika hivi sasa na asilimia mbili (2%) ipelekwe kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Pengo litakalojitokeza lizibwe kutokana na vyanzo vingine vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, bado kuna waajiri wengi katika sekta binafsi wanaostahili kulipa kodi hii lakini wapo nje ya wigo. Serikali ifuatilie suala hili haraka ili kupanua wigo wa upatikanaji wa mapato hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilipewa kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na kupitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Sheria. Dhamira ya Sheria hii ni kuweka utaratibu mzuri zaidi katika kusimamia Ununuzi wa umma. Manunuzi ya

Umma yanagusa maeneo ya mengi ya kiuchumi na kijamii na pia yanagusa uwazi na uwajibikaji katika kuendesha na kusimamia rasilimali za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sheria mpya ya Manunuzi ya Umma tayari ilikwishapitishwa na Bunge lako Tukufu, Kamati inasisitiza juu ya umuhimu wa Serikali katika kukamilisha haraka maandalizi ya kanuni za Manunuzi ya Umma chini ya Sheria hiyo, pamoja na kuwa na mkakati maalumu wa kuwaendeleza Maafisa Ugavi kama ilivyokuwa kwa Wahasibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kufanyia marekebisho sheria mbalimbali zinazotoa nafasi ya misamaha ya kodi na kupunguza zile sehemu ambazo hazina ulazima sana wa kupata misamaha hiyo. Katika Muswada wa Fedha (*Finance Bill)* ujao, Kamati inategemea kuona mabadiliko haya. Kiwango cha misamaha ya kodi ya asilimia tatu (3%) ya Pato la Taifa kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ni kikubwa mno ukilinganisha na kasi ya ukuaji wa uchumi wetu na vinaathiri ukusanyaji wa mapato yetu. Aidha, Serikali iangalie misamaha ya kodi iliyopo sasa na itathmini gharama yake inavyoshabihiana na Pato la Taifa na vilevile iangalie faida na hasara za misamaha hiyo kwenye kukuza uchumi. Kamati inasisitiza kuwa kiwango cha misamaha ya kodi lazima kiwe asilimia moja (1%) ya Pato la Taifa kama ilivyo kwa nchi nyingine jirani za Kenya, Uganda, Msumbiji. Kamati inashauri Serikali kuonyesha dhamira ya kweli kufanikisha lengo hilo katika suala hili na kutoa taarifa ya utekelezaji mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bado bajeti yetu ni tegemezi na lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba

ifikapo 2015 kiwango cha utegemezi wa misaada ya wahisani kwenye bajeti ya Serikali kisizidi asilimia 10 na kwa kuwa imedhihirika pasipo shaka kuwa ahadi za baadhi ya washirika wa maendeleo hazitekelezwi katika muda uliopangwa, Kamati inaishauri Wizara ya Fedha kubaini mapema sababu zinazopelekea kwa baadhi ya misaada hiyo kuchelewa ili utekelezaji wa bajeti usikwame kama huko nyuma kutokana na kuchelewa kwa ahadi hizo. Kama mikopo na misaada hiyo ina masharti basi Serikali ione mapema ni vipi yaweza kutimiza masharti hayo mapema ili pesa hizo zipatikane kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kusimamia utekelezaji wa miradi iliyofadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la '*Millenium Challenge Corporation (MCC)*' hasa ile ya barabara, nishati, maji na viwanja vya ndege. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha miradi hii inakamilika kwa mujibu wa muda na makubaliano yaliyopangwa. Usimamizi mzuri wa utekelezaji wa miradi hiyo umejenga imani kwa Serikali ya Marekani. Kwa kuwa imani hujenga imani, Kamati inaamini Serikali yetu itaendelea kunufaika na misaada mengine kutoka *MCC* pindi mkataba *(compact)* wa sasa utakapomalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba mwezi Juni 2011, Bunge lilipitisha Azimio la kuongeza Muda wa uhai wa mpito wa Shirika Hodhi la Mali za Mashirika ya Umma *(CHC)* kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia tarehe 1 Julai 2011. Lengo la Azimio hilo lilikuwa kutoa fursa kwa *CHC* kukamilisha taratibu za kiutendaji na za kisheria pamoja na kuhamisha kazi zitazokuwa zimebaki kwenda Ofisi ya Msajili wa Hazina pindi kipindi cha mpito

kitakapofikia ukomo pamoja na kukamilisha marekebisho ya kimuundo na kisheria ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo itakabidhiwa majukumu ya *CHC*. Kamati inasisitiza marekebisho hayo ya kimuundo na kisheria yafanyike kwa umakini mkubwa katika kipindi hiki cha mpito ikiwa ni pamoja na kuwaongezea uwezo watendaji wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ili waweze kukamilisha majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Kamati inapenda kuikumbusha Wizara ya Fedha kuwa yenyewe ndio kitovu cha Wizara zote. Kushindwa kuwajibika vyema kwa Wizara hii, mwisho wa siku kutapelekea kushindwa kufikia malengo kwa Wizara nyingine. Kwa mantiki hiyo, Kamati inaishauri Wizara kutekeleza mipango yake kwa umakini na uangalifu ili kufikia malengo iliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda kumalizia kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya na ushirikiano wao walionipa katika kujadili na kupitia Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2012/2013. Naomba nitumie fursa hii kuwatambua wajumbe wa Kamati hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mtemi Andrew John Chenge, Mwenyekiti, Mheshimiwa Dunstan Kitandula ambaye ndiye Msomaji, Mheshimiwa Jesephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu, Mheshimiwa Devotha M. Likokola, Mheshimiwa Martha J. umbulla, Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mheshimiwa Abdulaziz M. Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo,

Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Richard M. Ndassa, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Amina Abdulla Amour, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Alhaj Mohammed H. Missanga, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na Mheshimiwa Subira K. Mgalu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa - Waziri wa Fedha na Manaibu wake Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum. Naomba niwashukuru Watendaji Wakuu wa Wizara, Benki Kuu, Mashirika, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara ya Fedha kwa kuandaa Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Spika kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha

2012/2013 kama alivyowasilisha mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kitandula, tunakushukuru sana kwa niaba ya Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kusoma hotuba yako. Sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Fedha, ambaye ni Waziri Kivuli, Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. KABWE Z. ZITTO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni ya 99(7), toleo la mwaka 2007 na kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, napenda kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu ya Wizara ya Fedha – Fungu 50 Wizara ya Fedha, Fungu 21 Hazina, Fungu 22 Deni la Taifa na Fungu 23 - Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali. Vilevile Fungu 10 Tume ya Pamoja ya Fedha na Fungu 13 Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafungu yote yaliyo chini ya Wizara ya Fedha yanaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi bilioni 4,208 (trilioni 4.2) ili yaweze kutekeleza majukumu yake. Mafungu haya maombi yake ya Fedha ni sawa na asilimia 28 ya Bajeti nzima ya Serikali ya mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha ndiyo msimamizi mkuu wa uchumi wa nchi ikitekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo, kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani na ya nje, kusimamia matumizi ya Serikali, kusimamia utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma, kusimamia manunuzi ya Serikali na Taasisi na Mashirika ya Umma, kusimamia Deni la Taifa na dhamana za Serikali, kutafuta suluhisho na kusimamia mfumo wa kodi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kupambana na Fedha haramu. Sambamba na hayo ni kusimamia na kutekeleza mpango wa kupunguza umaskini nchini kupitia utekelezaji wa MKUKUTA II.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha na mafungu yote yaliyo chini yake ndio moyo wa Serikali na hivyo ni lazima kuitazama Wizara hii kwa jicho kali na kutilia mashaka kila jambo ambalo inalifanya ili kuhakikisha kuwa moyo huu hausimami maana madhara yake ni kwa taifa zima na watu wake. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupitia Waziri Kivuli wa Fedha inatekeleza wajibu huu kwa Uzalendo, Uadilifu na kwa misingi ya Uwajibikaji. Tumetekeleza wajibu huu na tunaendelea kuutekeleza bila kujali maneno na kuweka maslahi ya Taifa letu mbele ya kila kitu kingine. Maslahi ya Taifa ni zaidi ya vyama vya siasa, mahala tunapotoka au dini tunazoamini. Maslahi ya Taifa ni kwa ajili ya Watazania na hasa Watanzania milioni 30 *(The Bottom 30M)* ambao bado wanaishi katika ufukara mkubwa sana wakikosa huduma muhimu za jamii na wanaoishi vijijini ambapo hakuna umeme, barabara hazipitiki na wanahangaika kutwa kutafuta maji safi na salama. Maslahi ya Taifa sio faida ya wachache wenye kuishi mijini au wanasiasa wanaotafuta ushawishi kwa umma bila kujali matakwa ya Umma. Watanzania wanyonge wa vijijini

wanajua maslahi yao ni nini. Wanajua kina nani wanapigania maslahi ya Wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapato ya Serikali. Kwa mujibu wa taarifa ya mwenendo wa Uchumi ya mwezi Julai *(Monthly Economic Review, July 2012)* iliyotolewa na Benki Kuu ya Tanzania, katika kipindi cha mwezi Juni, Serikali iliweza kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 998.0. Hata hivyo, matumizi halisi yalikuwa kiasi cha shilingi trilioni 1.9 hali iliyopelekea kuwepo kwa nakisi baada ya kuondoa msaada wa masharti wa masharti wa shilingi bilioni 400.2; nakisi hiyo ililipwa kwa vyanzo vya ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo ilionyesha kuwa mapato yote ukiondoa fedha zilizokusanywa na Serikali za mitaa kwa mwezi Juni, yalikuwa kiasi cha shilingi bilioni 887.5 ambacho ni zaidi ya asilimia 38.1 ya malengo yaliyokuwa yamewekwa kukusanywa mwezi huo. Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* ilikusanya kiasi cha shilingi bilioni 753.3, kiasi ambacho ni zaidi ya asilimia 22.3 ya malengo ya makusanyo kilichokuwa kimewekwa na mamlaka hiyo. Makusanyo haya ni makubwa zaidi kukusanywa na *TRA* kwa mwezi mmoja tangu Mamlaka hiyo ianzishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika makusanyo hayo ya mwezi Juni, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikuwa imejiwekea lengo la kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 242.4 kama kodi ya Mapato, lakini ilikusanya kiasi cha shilingi bilioni 366.0 kiasi ambacho ni zaidi kwa asilimia 60.8 ya malengo yaliyokuwa yamewekwa. Kambi ya Upinzani inapenda kulikumbusha Bunge na Taifa kwamba katika Bajeti Mbadala iliyowasilishwa hapa Bungeni tulisema kwamba *TRA* wanao uwezo wa kukusanya mpaka shilingi

trilioni moja kwa mwezi iwapo tutadhibiti misamaha ya kodi, tutakusanya kodi stahili katika Sekta ya Madini na tutasimama kidete kuzuia ukwepaji kodi wa Makampuni ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania kuimarisha zaidi marekebisho yanayofanyika katika mfumo wa kodi ili kufikia lengo tajwa la kufikia makusanyo ya zaidi ya asilimia 20 ya Pato la Taifa. Mabadiliko kadhaa tunayoyafanya kwenye Sheria ya Fedha itakayosomwa hapa Bungeni katika Mkutano huu wa Bunge yana lengo hilo la kupanua wigo wa kodi na hivyo kulifanya Taifa liweze kujitegemea lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mauzo ya nje. Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu ya Tanzania inapaswa kuhakikisha kuwa Akiba ya Fedha za Kigeni nchini inakuwa imara muda wote. Biashara ya nje ndio inaingiza Fedha za kigeni nchini kwa hiyo ni eneo la kutazama kwa makini na kuchukua hatua mwafaka. Taarifa ya mwenendo wa uchumi kwa mwezi Julai iliyotolewa na Benki kuu inaonyesha kuwa jumla ya mauzo ya Tanzania nje yalikuwa dola za kimarekani bilioni 7.99 ukilinganisha na kiasi cha dola bilioni 7,05 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2011. Hali hii ilisababishwa kwa kiasi kikubwa kutokana na kuongezeka kwa bei ya mauzo ya dhahabu**.** Hata hivyo, manunuzi yetu kutoka nje yamefikia dola za Kimarekani bilioni 12.96.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo inaonyesha kuwa mauzo ya dhahabu nje kwa mwaka 2011 yalikuwa kiasi cha dola za kimarekani bilioni 2.3 sawa na aslimia 56.7 ya mauzo yote nje, wakati mauzo ya nje kutokana na bidhaa

zilizozalishwa viwandani yalikuwa ni jumla ya dola za marekani milioni 922.0 sawa na asilimia 22.4 ya mauzo yote ya nje. Aidha, mauzo ya mazao mbalimbali kama Pamba, Katani, Korosho, Chai, Kahawa na mengineyo yalikuwa na thamani ya dola za kimarekani 761.1 katika kipindi hicho cha mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo imeendelea kuonyesha kuwa tuliagiza bidhaa kutoka nje zenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni 12.96. Katika manunuzi hayo tuliyofanya mafuta peke yake yalikuwa na thamani ya dola za Kimarekani bilioni 3.6 ambalo ni ongezeko la asilimia 60.1 ukilinganisha na kipindi kama hicho kwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizi zinaonyesha kwamba fedha zote za kigeni zilizotokana na mauzo ya dhahabu, bidhaa za viwandani na korosho zilitumika kuagiza mafuta pekee yake. Hali hii ni mbaya sana kwa uchumi wa Taifa letu na juhudi zote za kuongeza mauzo nje zinaliwa na uagizaji wa mafuta ambao umepanda sana katika siku za hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa, kuanzia mwaka jana Serikali imekuwa ikitekeleza mpango wa umeme wa dharura ambao umepelekea matumizi makubwa ya mafuta. Hata hivyo, ieleweke kuwa Mpango mzima wa Manunuzi ya Mafuta ya kuendesha mitambo ya Umeme inaligharimu Taifa fedha nyingi sana. Takwimu zinaonyesha kuwa Serikali inapaswa kutumia zaidi ya shilingi 42 bilioni kila mwezi kuendesha mitambo ya dharura ya umeme. Manunuzi yenyewe ya mafuta yamejaa mazonge ya ufisadi uliokithiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya kutaka Spika aunde timu ya kuchunguza ufisadi katika manunuzi ya mafuta na licha ya Kamati ya Bunge kutaka uchunguzi wa kibunge kufanyika katika manunuzi haya, bado hakuna hatua inayochukuliwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Mamlaka ya Manunuzi ya Umma *PPRA* kufanya uchunguzi wa kina kuhusu manunuzi ya mafuta kuzalisha umeme ambayo yanachoma bilioni 42 za Serikali kila mwezi. *PPRA* hapaswi kufumbia macho manunuzi yanayotafuna shilingi bilioni 1.4 kila siku na yanayoongeza manunuzi ya nchi kutoka nje (*imports*) na hivyo kupoteza fedha nyingi sana za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha ambayo ndio Wizara Mama ya *PPRA* kupitia Fungu 50 na ndio Wizara yenye kusimamia uchumi wa nchi kwa ujumla, ituletee Bungeni Taarifa ya Uchunguzi utakaofanywa na *PPRA* kuhusu manunuzi shilingi 1.4 bilioni kila siku ya mafuta kuendesha mitambo ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Deni la Taifa. Fungu 22 ambalo ni Deni la Taifa, linaombewa jumla ya shilingi bilioni 2,735 ili kuweza kulipa madeni ikiwemo deni la nje la shilingi bilioni 373 na trilioni 1.5 kama deni la ndani. Kwa mujibu wa taarifa ya mwenendo wa uchumi ya mwezi Julai 2012, deni la nje la Taifa *(external debt)* mpaka mwisho wa mwezi Juni 2012 lilikuwa limefikia kiasi cha dola za Kimarekani milioni 10,354.6 kiasi ambacho ni ongezeko la zaidi ya dola milioni 385.9 kwa kipindi kama hicho mwaka 2011. Aidha, katika kipindi hicho deni la ndani lilikuwa kiasi cha shilingi bilioni 4,174.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni ina taarifa kwamba takwimu hizi za Deni la Taifa hazihusishi dhamana ambazo Serikali imezitoa kwa Mashirika ya Umma na kampuni binafsi. Dhamana ni lazima katika siku za usoni ziwe ni sehemu ya deni la Taifa, maana tumeshuhudia sasa ambapo kampuni nyingi binafsi zimeshindwa kulipa mikopo iliyodhaminiwa na Serikali. Mfano ni malipo ya deni lenye thamani ya shilingi bilioni 60 la kukodisha ndege ya *Airbus* kwa Shirika la *ATCL* kutoka kampuni ya *Wallis Traders ya Lebanon* na deni lililochukuliwa na Kampuni ya *Kiwira Coal and Power limited* ambapo mbia wake alishindwa kuendesha mradi wa Makaa ya Mawe Kiwira licha ya kudhaminiwa na Serikali Mkopo kutoka kwenye taasisi za fedha hapa nchini, ambapo sasa Serikali imepanga kulipa shilingi bilioni 40 katika Bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haina tatizo na ustahimilivu wa Deni la Taifa *(Debt sustainability)* kwani tunajua kuwa mataifa makubwa yanakopa sana na yana uwiano mkubwa wa Deni kwa *GDP* kuliko sisi. Tatizo letu ni namna ambavyo fedha za mikopo zinatumika. Matumizi ya mikopo tunayochukua sio endelevu maana sehemu ya mikopo hiyo hutumika kwa matumizi ya kawaida badala ya matumizi ya uzalishaji au kuongeza uwezo wetu wa kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaendeleza wito wake wa kutaka Fungu 22 la Deni la Taifa lifanyiwe Ukaguzi Maalum *(Special Audit)* ili tuweze kujua mikopo hii tunayochukua kila wakati inatumika kufanyia nini? Miradi iliyotekelezwa kutokana na madeni ambayo Waziri wa Fedha aliitangaza wakati wa kufunga mjadala

wa Bajeti Kuu ya Serikali ifanyiwe ukaguzi kutambua ukweli na kuona thamani ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaendelea kuhoji kama tulivyohoji mwaka 2011/2012 kuhusu matumizi mabaya ya fedha za umma. Katika Fungu 21, kasma 229929, Serikali imetenga shilingi bilioni 26.4 kwa ajili ya kulipa fidia kwa mikataba mbalimbali ambayo Serikali imeingia. Hii inaonyesha kuwa Serikali inatumia fedha nyingi sana kwa ajili ya mikataba iliyoingiwa na Mashirika ya Umma na kuliletea hasara Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na kutaka majibu kutoka kwa Serikali, bado tunataka kuwe na usimamizi thabiti ili kulinda fedha za umma zinazotumika kwenye Mashirika ya Umma, ambapo kumekuwa na usimamizi mbovu sana na unaopelekea Taifa kupoteza fedha nyingi sana kutokana na ubadhirifu katika Mashirika ya Umma. Hii ni kweli kwa Mashirika ambayo Serikali inamiliki sehemu ya hisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkopo wa kununua Rada Iliyogubikwa na ufisadi. Sehemu ya malipo ya Deni la Taifa ni mkopo ambao Serikali ilichukua ili kununua Rada kutoka kampuni ya *BAE* ya Uingereza. Suala hili la rada limejadiliwa sana nchini kwa upande mmoja tu wa ufisadi wa kupandisha bei ya Rada na hatimaye kurejeshwa kwa kile kilichoitwa chenji ya Rada. Hiyo ilikuwa ni nusu tu ya ukweli kuhusu suala la Rada kwani Serikali ilikopa kiasi cha dola za kimarekani 40 milioni kutoka Benki ya *Barclays* ya Uingereza kwa ajili ya kununulia Rada. Mkopo huo ulikuwa na Riba ya asilimia 4.9 juu ya kiwango cha riba zinazotolewa na Benki ya Dunia au *IMF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua kama mkopo huu umeshalipwa wote na jumla tulilipa kiasi gani cha fedha. Ukilinganisha fedha iliyorejeshwa kama chenji ya Rada na fedha ambayo Tanzania ililipa Benki ya Barclays *(Principal amount na Interest*), je chenji ya Rada ilikuwa na thamani yoyote kifedha? Mjadala wa ununuzi wa Rada hauwezi kwisha kwa kufurahia kurejeshewa chenji tu. Mjadala huu bado mbichi kabisa kwani tunataka ukweli na ukweli mtupu uelezwe kwa umma na kuona Taifa lilipata hasara kiasi gani kwa ufisadi huu wa kimataifa na hatua stahiki za kisheria kuchukuliwa dhidi ya wote walioingiza hasara kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu. Taifa letu limekuwa na sheria nyingi ambazo ziliwahi kutungwa kwa ajili ya kukabiliana na tatizo la fedha haramu, rushwa na uhalifu uliopangwa hapa nchini mwetu tangu tupate uhuru, na hii inathibitishwa na uwepo wa sheria zaidi ya 15 kuwahi kutungwa tangu uhuru. Sheria hizo ni:-

*(i) The Establishment of the Permanent Commission of Inquiry, or Ombudsman, 1966;*
*(ii) The Foreign Exchange Control Act 1966;*
*(iii) The Anti-Corruption Act, 1971;*
*(iv) The Establishment of an Anti-Corruption Squad in 1975;*
*(v) The Economic Sabotage Act, 1983;*
*(vi) The Economic and Organised Crime Act, 1984;*
*(vii) The Proceeds of Crime Act, 1991;*
*(viii) The Leadership Code (Declaration of Assets) Act, 1995;*

(ix) *The Appointment of the Presidential Commission of Inquiry into Corruption, 1996;*

(x) *The BOT Circular to Banking and Non-banking Financial Institutions, No.8 of 2000, on Money Laundering;*

(xi) *The Drugs and Illicit Traffic of Drugs Act, 1995;*

(xii) *The Arms and Ammunition Act, 1991;*

(xiii) *The Mutual Assistance in Criminal Matters Act, 1991;*

(xiv) *The Tanzania Intelligence and Security Act, 1998;*

(xv) *The Anti-Money Laundering Act, 2007; na*

(xvi) *The Anti-Money Laundering (amendment) Act, 2012.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Bunge liliimarisha Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu mwaka 2011. Hata hivyo bado nchi yetu imegubikwa na fedha chafu na hasa wizi katika mabenki hapa nchini. Wakati Sheria ya Fedha Haramu inayataka mabenki kutunza kumbukumbu sahihi za wateja, kumekuwa na matukio (yaliyoripotiwa na yasiyoripotiwa) ya wafanyakazi wa mabenki hapa nchini kushirikiana na baadhi ya wananchi kuiba fedha za wateja na hasa wateja ambao wamefariki dunia na ndugu na jamaa zao kutojua taarifa za kibenki za marehemu hawa. Serikali inapaswa kufahamu kuwa wizi kwenye mabenki ni moja ya sifa mbaya sana ya mfumo wetu wa fedha na hivyo kusababisha benki kuweka riba kubwa sana ili kufidia ‘*risk’* kama hizi za watu ‘kupiga’ amana za wateja kwenye mabenki. Kambi Rasmi ya upinzani inaitaka Wizara ya Fedha kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu kudhibiti wizi kwenye Benki za hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata maelezo ya kina juu ya matatizo ya mtaji “*capital under pressure”* yanayoikabili benki ya *NBC* na hatua zilizochukuliwa na Serikali kama mmoja wa wanahisa

dhidi ya mwanahisa mwenye dhamana ya kuisimamia Benki hiyo (*ABSA*) kwa kushindwa kuisimamia kwa umakini na hivyo kuiingiza katika matatizo hayo ya mtaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa wanahisa (ambapo Serikali ni mmoja wao) wanapaswa kuongeza mtaji katika benki ya *NBC* ili kuinusuru, Benki ambayo ni moja ya benki kubwa kabisa hapa nchini ambayo kama ingekuwa na usimamizi mzuri ingepaswa kujiendesha yenyewe na kutoa gawio kwa wanahisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia inataka kupata maelezo ya kina kuhusu utata uliopo kwenye Benki ya NBC ambayo sasa imewekwa chini ya uangalizi wa Benki Kuu ya Tanzania. Tusingependa kueleza zaidi suala la NBC maana laweza kuleta machafuko nchini na hivyo tunahitaji maelezo. Lakini pia tunaomba Gavana wa Benki Kuu atokee mbele ya Kamati ya Fedha na Uchumi ili kuweza kuelezea sakata hili la Benki la NBC. Hili lifanyike haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa iliyotolewa na Benki Kuu ya Uswissi na kuchapishwa na magazeti mbalimbali ya hapa nchini mwezi Juni, 2012 inaonesha kuwa viongozi wa Serikali pamoja na wafanyabiashara wakubwa wametorosha fedha kupeleka kwenye mabenki ya Uswissi kiasi cha shilingi bilioni 315.5. Habari zaidi zinaeleza kwamba mabilioni haya yanatokana na '*deals*' zilizofanywa na watendaji wa Serikali na wafanyabiashara kadhaa kwenye sekta za Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepata taarifa kuwa mmoja wa Viongozi wa juu

kabisa wa Tanzania na baadhi ya Mawaziri wa Serikali za awamu zilizopita ni miongoni mwa wamiliki wa fedha hizi. Sehemu kubwa ya fedha zililipwa na Kampuni za utafutaji wa Mafuta na Gesi katika Pwani ya Mkoa wa Mtwara zilizopewa mikataba kati ya mwaka 2004 na 2006. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa taarifa rasmi ya hatua gani imechukua mara baada ya taarifa ile kutoka Benki ya Taifa ya Uswissi ilipotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaitaka Serikali kuliambia Taifa hatua itakazochukua kurejesha fedha hizi na nyingine zozote ambazo zimefichwa ughaibuni. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni italazimika kuweka wazi taarifa na majina ya watu wenye umiliki wa fedha katika Benki nchini Uswissi iwapo Serikali haitatoa taarifa rasmi kuhusu suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuna taarifa nyingine zinaonyesha jinsi ambavyo taifa linaibiwa kupitia kesi mbalimbali ambazo Serikali imeshitaki au kushitakiwa kwenye Mahakama za Kimataifa. Mfano mzuri ni Kesi ya *IPTL* na *Standard Chartered Bank* ya Hong Kong ambayo imechukua muda mrefu bila kuisha na kuliingizia taifa hasara kubwa sana. Tunapenda kufahamu ni kwa nini mpango wa kumaliza kesi hii nje ya Mahakama hautekelezwi na vilevile mpango wa kugeuza Mtambo wa kufua umeme wa *IPTL* kuwa wa Gesi kwa nini hautekelezwi? Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata majibu kuhusu mambo yafuatayo:-

(i) Fedha zilizoko kwenye Escrow Akaunti Benki Kuu za *IPTL* (Tegeta *escrow*) zimefikia kiasi gani mpaka sasa na usalama wa fedha hizo ukoje? Ikumbukwe kwamba kuna

uamuzi wa Bunge kwamba fedha hizi zisitumike wala kutolewa mpaka maamuzi kuhusu mtambo wa *IPTL* kufikiwa na hasa uamuzi wa kugeuza mtambo huu kutumia Gesi Asilia.

(ii) Suala hili la kesi ya *IPTL* limechukua muda mrefu sana na sasa ni wakati muafaka likamalizwa nje ya Mahakama kwa Waziri wa Fedha kukutana na pande zote za mgogoro huu ili liweze kufikia mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *Oxford University Press Tanzania* Kufungiwa. Mnamo tarehe 3 Julai 2012, Benki ya Dunia ilitangaza kuifungia kampuni ya uchapishaji ya *Oxford University Press Tanzania Ltd. (OUPTL)* kutokana na vitendo vya rushwa ambavyo kampuni hiyo ilikiri kuhusika kwake kwenye miradi mbalimbali ya elimu iliyokuwa inafadhiliwa na Benki hiyo katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni hiyo ilikiri kuhusika katika kuwahonga Maafisa mbalimbali wa Serikali katika mkataba wake wa kusambaza vitabu na kampuni hiyo ilikubali kuilipa Benki ya Dunia kiasi cha dola za kimarekani 500,000 kama sehemu ya makubaliano yake kutokana na kashfa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (*PPRA*) ilitangaza kuifungia kampuni hiyo hapa nchini kwa kipindi cha miaka saba, wakati ambao tayari tulishawapa zabuni ya kusambaza vitabu vilivyotokana na fedha iliyorudi ya chenji ya rushwa ya Rada ambazo ziliamuliwa kuwa zitaenda kununua vitabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuinyang'anya kampuni hii zabuni ya kuchapisha na kusambaza vitabu hivyo na badala yake kazi hiyo yapewe makampuni ya ndani ya nchi yetu. Tabia ya Serikali kufanya kazi na kampuni ambazo tayari zina dosari ama za kifisadi au kukiuka sheria na maagizo ya Serikali inatoa picha mbaya kwenye uchumi. Hali kadhalika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwachukulia hatua Maafisa wote wa Wizara waliohusika katika "rushwa ya *Oxford*".

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara hewa nchini. Katika hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu makadirio ya mapato na matumizi katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2012/2013, tulitaja kiasi cha shilingi bilioni tisa (9) ambazo zililipwa kama mishahara kwa watumishi hewa kama ilivyoripotiwa na magazeti ya '*The Daily News'* na '*The Guardian'* ya Machi 23, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya tarehe 31 Machi, 2012 inaonesha kwamba kwa mwaka wa fedha 2010/2011, jumla ya shilingi 142,715,827.99 zililipwa kama mishahara kwa wastaafu, watumishi walioacha au kufukuzwa kazi na watumishi wengine ambao hawakustahili. (Tazama Ripoti ya *CAG*, toleo la Kiingereza uk.37) Aidha, ripoti hiyo imeonesha kiasi cha shilingi 1,842,607,565.29 zilizolipwa kama mishahara hewa kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Fedha kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Fedha na Uchumi ya tarehe 7 Agosti, 2012 ni kwamba uhakiki wa watumishi uliofanyika mwezi Januari, 2012 kwenye Halimashauri 133 na kwenye taasisi na wakala za Serikali 154 ulibaini majina 9,949 ya watumishi wasiostahili kuwemo kwenye orodha ya mishahara. Idadi hii ya watumishi hewa ni sawasawa na takribani idadi ya watumishi walioajiriwa katika sekta nzima ya madini kwenye migodi ya dhahabu hapa nchini. Watumishi hewa wanaokaribia 10,000 ni wengi mno na inaonyesha dhahiri namna Serikali isivyo makini katika suala hili ambalo linasababisha upotevu mkubwa wa fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Fedha alikiri mbele ya Kamati ya Fedha na Uchumi kwamba mwezi Februari Serikali ililipa shilingi bilioni 5.1 kama mishahara hewa. Hii maana yake ni kwamba Serikali hutumia zaidi ya shilingi bilioni 70 kila mwaka kwa watumishi hewa wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka fedha hizi wanazolipwa watumishi hewa zitumike kuwalipa Walimu na Madaktari madai yao kwani ni nyingi na zinatosha sana. Siku zote sababu za Serikali kutotimiza matakwa ya wafanyakazi kwenye sekta ya Afya na Elimu ni kwamba Serikali haina fedha. Lakini hapa tunashuhudia shilingi bilioni 70 kila mwaka zikiteketea kulipa watumishi hewa ambao hawapo, hawafanyi kazi na hivyo kufaidisha mtandao wa kifisadi ambao kwa vyovyote vile unaanzia Wizara ya Fedha na Wizara ya Utumishi. Serikali inakosa vipi fedha za kulipa madai ya Walimu na inapata za kulipa watumishi hewa? Serikali inakosa vipi fedha za kulipa Madaktari na Manesi lakini inapata shilingi bilioni 70 kila mwaka kulipa watumishi hewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka mradi huu wa watumishi hewa wenye mauzo *(turnover)* ya shilingi 70 bilioni kwa mwaka uvunjwevunjwe ili kupata fedha za kulipa Walimu na Madaktari. Waziri wa Fedha asambaratishe mtandao huu mwovu ambao sasa umeota mizizi kwenye Taasisi za Serikali. Vilevile Waziri agawe kwa Wabunge taarifa ya uhakiki wa wafanyakazi wa Serikali na pia hatua ambazo Serikali imechukua dhidi ya vinara wa mtandao wa watumishi hewa Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu ya Tanzania *(BOT).* Taasisi hii ndiyo yenye dhamana ya kutayarisha na kusimamia sera za fedha na utendaji mzima wa taasisi za fedha kwa ujumla. Katika kutekeleza hilo, Benki Kuu ndicho chombo kinachoweka miongozo kwa taasisi za fedha, taasisi za bima na taasisi za hifadhi za jamii ili kuhakikisha fedha za wanachama katika taasisi hizo zinalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi za fedha zimegawanyika katika sehemu kuu mbili, ambazo ni tasnia ya benki (*Banking industry*) na tasnia ndogo ya fedha (*Microfinance industry*). Tasnia zote hizi zinahudumia wateja tofauti kwa kulingana na wanachojishughulisha nacho katika kuinua kipato cha familia inayomtegemea, mteja yuko kwenye sekta binafsi au sekta rasmi ya ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki Kuu katika kutimiza wajibu wake inailazimu kutoa vigezo vitakavyozingatiwa katika utoaji wa mikopo ili kukabiliana na wakopaji ambao wanaweza kuwa na lengo la kuchukua fedha wakati hawana nia ya dhati ya kurejesha mikopo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, riba Katika Taasisi za Fedha. Tofauti kati ya viwango vya riba vinavyotozwa kwenye mikopo na vile vinavyotolewa kwenye amana kama faida vimeendelea kuwa juu, licha ya kuongezeka kwa ushindani katika sekta ya kibenki. Hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na kukosekana kwa taarifa sahihi za wakopaji *(credit reference data bank)* na kutokuwepo kwa taasisi ya utoaji wa taarifa sahihi za waombaji mikopo *(Credit Rerefence Bureau)* nchini. Aidha, gharama kubwa za kufanya biashara kutokana na miundombinu hafifu, nazo zimechangia kuongeza viwango vya riba vinavyotozwa kwenye mikopo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaomba taarifa ya kuanzishwa kwa *Credit Reference Bureaux* kwa mujibu wa Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, usimamizi wa Tasnia Ndogo ya Fedha *(Microfinance Industry-MFI).* Tasnia hii ndiyo inayoshughulika moja kwa moja na kundi kubwa la Watanzania ambao hawako kwenye mfumo rasmi wa ajira kwa kuwapa mikopo midogomidogo kwa shughuli rasmi au zisizo rasmi, ili kuhakikisha kuwa kipato cha familia kinapanda na hivyo uchumi wa mwananchi mmojammoja unakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tasnia hii inalenga kuboresha maisha ya wananchi wa vijijini na maeneo mbalimbali ya mijini. Tasnia hii inalenga kuboresha maisha kwa wananchi mmojammoja au makundi *(SACCOS)* na benki jamii *(VICOBA)* ambazo zimekuwa na wanachama wengi wanaoendelea kujiunga ili kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa mdhibiti anayeelewa jinsi tasnia hii inavyofanya kazi zake na aina ya wateja inaowahudumia, ni udhaifu mkubwa unaosababisha tasnia hii kushindwa kukua. Kukosekana kwa udhibiti wa sekta ndogo ya fedha kunasababisha wananchi maskini kuumia sana. Mfano tumeshuhudia namna Kampuni za kukopesha zinavyowafanya Walimu vijijini kuwa maskini zaidi kwa kuweka riba kubwa sana. Hata hivyo Serikali imekaa kimya bila kusaidia wanyonge hawa kwa kuchukua hatua madhubuti za kudhibiti na kusimamia sekta hii. Mfano mzuri wa Serikali kushindwa kusaidia wanyonge ni pale ambapo wanachi wengi sana kujikuta wamepoteza fedha zao kupitia *'schemes'* kama vile *DECI* ambapo wananchi walikusanya zaidi ya shilingi bilioni 16 ambazo mpaka sasa hata riba yake hatujui inakwenda wapi? Kungekuwa na Mamlaka ya kusimamia sekta ya fedha kwa ajili ya wanyonge, tusingeshuhudia unyonyaji huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuunda Mamlaka ya Usimamizi wa sekta ndogo ya Fedha *(Tanzania Microfinace Regulatory Authority)* hapa nchini badala ya Benki Kuu ya Tanzania ambayo ndiyo msimamizi wa tasnia ya benki. Lengo ni kuhakikisha kuwa wananchi wa vijijini wanaopata mikopo kutoka kwenye taasisi za benki wanalindwa na dola. Mamlaka italinda haki za wanyonge dhidi ya '*loan sharks'* na wajibu wa wanyonge wenye kuchukua mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuundwa kwa chombo chenye mamlaka ya kusimamia taasisi ndogo ya fedha, ni lazima kutokana na ukweli kwamba kuna utofauti wa muundo baina ya mabenki na taasisi ndogondogo za

fedha; inakuwa ni vigumu kudhibiti riba na utoaji wa vigezo vya kifedha katika kuhudumia wananchi na kutoa mikopo kwa wateja wa tasnia hizo mbili zilizo tofauti kimuundo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa chombo chenye mamlaka pia itasaidia kuwa na *Credit Reference Bureau* itakalokuwa na taarifa za wakopaji kutoka taasisi ndogondogo za fedha tofauti na itakayosimamia wadaiwa wa mabenki na taarifa hizi zitasaidia udhibiti wa wateja wa taasisi hizi kuchukua zaidi ya mkopo mmoja kwenye taasisi tofautitofauti ambapo hali hii husababishwa na ucheleweshaji wa mikopo inayotolewa na taasisi hizi pamoja na uhafifu wa mikopo katika kumsaidia mlengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Mifuko ya Hifadhi za Jamii ni mojawapo ya sekta ambayo ina uwezo mkubwa wa kupunguza ukosefu wa ajira kwa vijana wetu, kama uwekezaji unaofanywa kwa kutumia mifuko hiyo utasimamiwa vizuri.

Meshimiwa Naibu Spika, inaonesha kwamba Mifuko hii imekuwa ikikusanya michango ya wanachama na kulipa wastaafu wanachama wa Mifuko hii vizuri. Kutokana na maelekezo ya sheria mpya iliyoleta mjadala baina ya wafanyakazi na Serikali juu ya mabadiliko ya sheria na utoaji wa mafao kwa wafanyakazi, pamoja na Bunge kutaka mabadiliko ya sheria hiyo bado kuna haja ya kutazama namna mifuko ifanyavyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka wazi utendaji wa Mifuko hii katika maeneo nyeti yafuatayo, kwanza Ukwasi wake *(Liquidity of the Social Security funds).* Pili, uwekezaji *(Investments)* pia

*Risk Management reports.* Taarifa katika maeneo haya hupelekwa na mifuko kwenye Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma na kutokana na utaratibu wa Kazi wa Kamati hii ya *POAC*, ni vigumu wananchi wote kuona taarifa hizi ambazo ni muhimu kuwa wazi kwa umma. Taarifa kama hizi zitaliwezesha Bunge kuelewa kiwango cha usalama wa Mifuko hii na uwezo ziada *(excess financial capacity)* kuendelea kutoa huduma zinazohitajika. Kama ilivyo kwa mabenki, tunashauri kuwa taarifa za robo mwaka za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ziwe zinatangazwa kwenye magazeti yanayosomwa zaidi nchini ili wananchi na hasa wanachama wa mifuko waone namna mifuko yao inavyofanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa kuwa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kipindi chote imekuwa ikitoa ushauri katika sekta hii, hatuna budi kurudia ushauri tulioutoa mwaka jana kama ifuatavyo:-

"*Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza kwa Mifuko ya PSPF na PPF kuangalia namna ya kuwekeza katika maeneo yanayochochea ukuaji wa uchumi na hivyo kuzalisha ajira na kupata wanachama zaidi. Maeneo kama uwekezaji kwenye Bandari na Reli yanapaswa kuangaliwa kwani kutokana na jiografia ya nchi yetu ni maeneo yanayoweza kuzalisha faida kubwa sana. Tunaitaka Serikali ilieleze Bunge kuna mipango gani katika Mashirika haya (PSPF na PPF) kuangalia maeneo mapya ya uwekezaji katika miundombinu na hasa Bandari".*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifuko ya Hifadhi ya jamii, imewekeza katika miradi ya ujenzi wa nyumba nafuu kwa ajili ya wanachama wao na pia wanachi kwa ujumla.

Tunasisitiza Miradi hii isiwe Dar es salaam na Mwanza tu bali ienee nchi nzima kama ambavyo mfuko wa *PSPF* umeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani pia inashauri kwamba fao la Elimu ambalo Mfuko wa *PPF* unatoa kwanza litolewe na Mifuko mingine pia lakini pia lipanuliwe hadi kufikia elimu ya Chuo Kikuu. Fao hili la Elimu ambalo ni muhimu sana na twapongeza mfuko wa *PPF* kwa kulianzisha ni fao ambalo litasaidia sana kuhakikisha kuwa yatima ambao wazazi wao wanakuwa wamefariki wanapata uhakika wa kuendelea na masomo. Fao hili liwe fao la lazima kwa mifuko yote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni bado inasisitiza ushauri wake kuwa Mifuko yote ya Hifadhi ya Jamii ihamishiwe Wizara ya Kazi na Ajira kama Wizara inayohusika na *'social security'.* Hoja hii inatiliwa nguvu na uhalisia kwamba Mdhibiti wa Mifuko *(SSRA)* yupo chini ya Wizara ya Kazi. Vilevile Wizara ya Fedha kama mlipaji mkuu wa Pensheni asiwe na Taasisi hata moja ya Pensheni chini yake ili kuweka *'checks'.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika hakuna sababu ya kuwa na utitiri wa mifuko mingi kama ilivyo sasa. Ipunguzwe na kubakia na mifuko miwili tu, mmoja wa wafanyakazi walio katika sekta binafsi na sekta isiyo rasmi na mwingine kwa wafanyakazi wa sekta ya umma. Tunarejea pendekezo letu kwamba mifuko ya *NSSF* na *PPF* iunganishwe kuwa mfuko mmoja kwa ajili ya sekta binafsi na sekta isiyo rasmi na mifuko ya *PSPF*, *LAPF* na *GEPF* iunganishwe kuwa mfuko mmoja kwa ajili ya kushughulika na wafanyakazi wa Sekta ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya vipaumbele vya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mwaka 2012/2013 ni kupunguza misamaha ya kodi ya kutozidi asilimia moja ya *GDP*, kutokana na Mapato mengi ya Serikali kupotea kwa sababu ya kutoa misamaha ya kodi kwa wadau mbalimbali wanaotakiwa kulipa kodi na ikizingatiwa moja ya michango ya Waziri akiwa Mbunge tarehe 25/8/2011 alisema, *"kupunguza misamaha ya kodi ya kutozidi asilimia moja ya GDP".* Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini Waziri alikuwa na nia ya dhati na kukubaliana na Kambi Rasmi ya Upinzani uwezekano wa jambo hili. Hivyo basi, ili kuonesha kuwepo kwa dhamira ya kweli, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Waziri alijulishe Bunge juu ya utekelezaji wa azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msajili wa Hazina na Bodi za Mashirika ya Umma. Itakumbukwa kuwa mnamo mwaka 2010 Sheria Na.2 (*the Written Laws (Miscellaneous Amendments) No.2, Act 2010* ilipitishwa na katika eneo la kumi *(part X)* ilifanyia marekebisho Sheria ya Mashirika ya Umma *(The Public Corporations Act, Cap.257).* Sheria hii ilisainiwa na Rais mnamo tarehe 20 Mei 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mabadiliko hayo ya sheria, Ibara ya 20 na 21 ilibainisha bayana majukumu ya Msajili wa Hazina na ndipo iliweka majukumu yake ya kazi kuwa ni kusimamia mashirika yote ya umma. Aidha, mabadiliko hayo yalibainisha wazi kuwa Msajili wa Hazina hatakuwa mjumbe wa Bodi za Mashirika haya na wala hapaswi kushiriki kwenye vikao vya Bodi vya mashirika haya kwani yeye ni Msimamizi Mkuu wa mashirika hayo na anapaswa kusimamia utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mabadiliko hayo ya sheria, bado Msajili wa Hazina amekuwa akihudhuria vikao mbalimbali vya Bodi za Mashirika ya Umma kama mjumbe jambo ambalo ni kinyume na sheria na amekuwa akishiriki moja kwa moja kwenye maamuzi ya Bodi hizo jambo ambalo linamfanya kushindwa kutimiza wajibu wake wa kuwa msimamizi kama ambavyo sheria inaelekeza. Kambi ya Upinzani inataka kupata maelezo ya kina ni kwa nini hali hii imeendelea kuachwa iwe ilivyo kwa Msajili wa Hazina kuendelea kuwa mjumbe wa vikao vya Bodi za mashirika ya umma kinyume na sheria. Aidha, tunataka kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kupata maelezo ya Serikali kuhusu masuala yafuatayo:-

(i) Sakata la uuzwaji wa hisa za Shirika la *UDA* umefikia wapi?

(ii) Serikali imefikia wapi katika utungaji wa Sheria mpya ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ili kuimarisha usimamizi wa Mashirika ya Umma?

(iii) Serikali imefikia wapi katika pendekezo la kulifanyia marekebisho Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma *(CHC)* ili liweze kumiliki, kusimamia na kuziendesha hisa za Serikali katika Kampuni binafsi ambapo umiliki wa Serikali ni chini ya asilimia 50. Pendekezo hili lilikuwa ni uamuzi wa Bunge na hivi sasa mwaka mzima umepita bila Bunge kupatiwa taarifa yeyote kinyume na maelekezo yake.

(iv) Serikali imefikia wapi katika utekelezaji wa Waraka Namba Moja wa mwaka 2012 kuhusu usimamizi na

uendeshaji wa Mashirika ya Umma na hasa mahusiano kati ya Mashirika ya Umma na Wizara Mama? Waziri wa Fedha kama Msimamizi Mkuu wa Mashirika ya Umma amechukua hatua gani kuhakikisha falsafa ya *'eyes on, hands off'* katika kusimamia Mashirika ya Umma inatekelezwa kikamilifu na kuhakikisha Mashirika ya Umma yanaendeshwa kwa faida na bila kuingiliwaingiliwa na wanasiasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Takwimu ya Taifa. Ofisi ya Taifa ya Takwimu (*National Bureau of Statistics – NBS)* ilizinduliwa rasmi tarehe 26 Machi, 1999 kama Wakala wa Serikali *(Executive Agency)* kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya mwaka 1997, *(The Executive Agencies Act 1997) (Act No. 30 of 1997)* na ndio chombo rasmi kinachojihusisha na kutafuta, kuandaa na kusambaza takwimu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupanga mipango ya maendeleo na kuandaa sera mbalimbali za nchi husika, upatikanaji wa takwimu rasmi zinazotokana na Kanuni na Mbinu za Kitaalamu iliyowekwa na Ofisi ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa *(United Nations Statistical Division*) ni muhimu. Takwimu zote zilizo rasmi duniani hutolewa na Ofisi za Takwimu za nchi husika kupitia Sheria za Takwimu za nchi mbali mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imekua ikitoa Mapendekezo ya kuboresha utendaji wa Ofisi ya Takwimu katika Nyanja mbalimbali na Serikali kutothubutu kuchukua mapendekezo hayo na kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya miaka hamsini ya Wizara, taarifa inaonesha Wizara kuwa na nia ya kuboresha Ofisi ya Takwimu ya Taifa kwa kuboresha miundombinu ya utoaji takwimu nchini, kuimarisha mfumo wa takwimu nchini *(NBS),* kutoa takwimu sahihi na kwa wakati. Kutokana na nia hii ya Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzingatia Ofisi ya Takwimu kuwa na uhisiano wa moja kwa moja wa Ofisi ya Takwimu ya Taifa na ngazi za Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Kata na Vijiji kurahisisha upatikanaji wa takwimu ili zisaidie katika kupanga mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mapato - TRA. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania ijenge uwezo wa kukagua mahesabu ya kikodi kwenye Kampuni za Utafutaji wa Mafuta na Gesi, Kampuni za Madini na Kampuni za Simu ambazo uzoefu unaonyesha kuwa katika maeneo haya kuna mbinu nyingi sana za kukwepa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msisitizo mkubwa sana, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania kushirikiana kwa karibu na Mamlaka ya Mawasiliano nchini kukagua mapato ya Kampuni za simu na hasa kampuni ambazo zinatoa huduma kwenye kampuni za Simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mjadala wa Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano kulikuwa na mjadala kuhusu namna ambavyo wasanii wa Tanzania wanavyonyonywa mapato na Kampuni zinazotoa huduma ya miito kwenye kampuni za simu. Bunge lako lilielezwa kwamba biashara ya miito kwenye simu ina thamani ya shilingi bilioni 43 kwa mwaka

lakini msanii anayetengeneza kazi zinazouzwa anapata asilimia saba (7%) tu ya mapato hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zaidi za ziada zinaonyesha kuwa kampuni ya *On Mobile* yenye mkataba na Kampuni za Simu za *Vodacom* na *Airtel* kama '*aggrigator'* wa miito ya simu yenye miziki ya wasanii hapa nchini hailipi kodi kutokana na mapato yake. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa taarifa za kikodi za kampuni hii na washirika wake na hatua ambazo Serikali imechukua dhidi yao. Kambi ya Upinzani inashauri pia kwamba mapato yanayotokana na miradi kama hii kwenye Kampuni za simu yawe *'ring fenced'* na kutozwa kodi stahiki au kodi maalumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani-*Internal Auditor General*. Ofisi ya Mkuguzi Mkuu wa Ndani *(Internal Auditor General)* iliyoanzishwa na mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2010 inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikileta migongano katika maeneo ya kiutendaji na uwajibikaji, sheria haipo wazi juu ya upatikanaji wa mtaalam huyo kama inavyotakiwa na Sheria na 8 ya Utumishi wa Umma, kwa mfano kutangazwa kwa nafasi hizo na waombaji kufanyiwa usaili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na utata wa uteuzi wa Mkaguzi wa Ndani kama Sheria ya Utumishi wa Umma inavyoelekeza, Mkaguzi wa Ndani anasimamiwa na Katibu Mkuu Hazina (*Paymaster General*) ambaye naye ni mkaguliwa - kwa hiyo kunakuwa na mgongano wa kimaslahi, ofisi ya Mkaguzi wa Ndani inaweza kukosa uhuru. Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali katika ofisi ya

Mkaguzi wa Ndani *(Internal Auditor General office)* ingepaswa iwe na Bodi maalumu ambako wangekuwa wanaripoti ili kuweka uhuru unaofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakaguzi wa Ndani ni waajiriwa wa Serikali na hufanya kazi zao za ukaguzi kwa kipindi chote ambacho shughuli za Serikali zikifanyika. Mfano, katika Halmashauri Wakaguzi hutakiwa kuwajibika kuanzia upokeaji wa fedha kutoka Hazina hadi kutumika kwake. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji Serikali nini nafasi ya Wakaguzi wa Ndani kama ubadhirifu wa fedha za umma umeendelea kuwepo kama ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinavyothibisha?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ushughulikiaji wa matumizi mabovu ya rasilimali za umma, Serikali imekuwa legelege hasa pale taarifa zinapotolewa na Wakaguzi wa Ndani ambao hutoa taarifa mara kwa mara na Serikali kukaa kimya. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutambua umuhimu wa taarifa hizi za Wakaguzi wa Ndani na kuhakikisha inachukua hatua stahiki pasipo kusubiri taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo ukaguzi wake hufanyika kwa kuchelewa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2011/2012 pamoja na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2012/2013. Katika bajeti ya Wizara ya Fedha mwaka 2011/2012 Fungu Namba 50, Wizara ilitenga shilingi bilioni 659 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na fedha zilizotumika hadi kufikia Juni 2012 ni shilingi bilioni 402.7 ambapo fedha za ndani zikiwa shilingi bilioni 78.65 sawa na asilimia 11.9 ya bajeti ya maendeleo hivyo kutegemea fedha za nje katika kutekeleza miradi ya

maendeleo kwa asilimia 88.1. Kambi Rasmi ya Upinzani, pamoja na Serikali kutokukubali kutumia mapato ya ndani zaidi katika kugharimia miradi ya maendeleo, lakini inazidi kuishauri Serikali kuwa na mkakati wa dhati wa muda mrefu wa kuachana na utaratibu wa kutegemea misaada ya nje. Mkakati huo ulenge kuiongezea mapato kwa kutumia mbinu mbalimbali za kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya 2012/2013, Serikali imetenga shilingi bilioni 546.51 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni pungufu kwa asilimia 18 ya bajeti ya mwaka 2011/2012 ambapo Serikali ilitenga shilingi bilioni 659. Katika bajeti ya 2012/2013 ni asilimia 19.3 tu ya fedha za ndani ndizo zimeelekezwa kwenye miradi ya maendeleo na asilimia 80.7 ya makadirio ni fedha za nje ikiwa ni mikopo ya kibiashara na misaada. Kambi Rasmi ya Upinzani inahoji, ni maendeleo yapi ambayo Serikali inadhamiria kwa kutenga fedha ya maendeleo ambayo ni pungufu kwa asilimia 18 ya bajeti ya mwaka jana?

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Kambi ya Upinzani Bungeni inasisitiza umuhimu wa kuisimamia vema Wizara ya Fedha katika kusimamia uchumi wa nchi. Tuna imani kwamba Waziri wa Fedha, Mheshimiwa William Mgimwa na Manaibu wake Mheshimiwa Janeth Mbene na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum wataweza kukabili changamoto tulizoainisha katika hotuba yetu na kufanyia kazi mapendekezo ambayo tumeyatoa. Tumeona dalili za Wizara hii na hasa Waziri na Manaibu wake kusikiliza katika masuala ya kikodi, hivyo, tuna imani kwamba wataendelea kusikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani haitasita kutoa ushirikiano kwa lengo la kuleta maendeleo katika nchi yetu. Hata hivyo, tutakosoa kwa nguvu zetu zote na kuchukua hatua za kiuwajibikaji dhidi ya njama zozote za kudhoofisha maendeleo ya Taifa na watu wake. Siku zote tutasimama upande wa wanyonge na kuwasemea wasio na sauti, Watanzania milioni 30 wanaoishi vijijini na kwenye dimbwi la Umasikini (*The Bottom 30M*).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa hotuba yako na hasa kwa teknolojia ya kisasa katika kupitia hotuba yako, nikushukuru sana.

Sasa kabla ya wachangiaji na nikwambieni kabisa uchangiaji wa leo tutakuwa na wachangiaji wachache, kwa hiyo, nina *pressure* kubwa sana hapa mezani. Watakaopata nafasi basi washukuru, ambao hawatapata nafasi basi tuwiane radhi. Nitajitahidi angalau tuhakikishe kila chama, pande za muungano yaani tu-*balance* kidogo kwa hizi nafasi chache tulizonazo.

Nilitaka kusema neno moja tu kabla hatujaanza kuchangia kuhusu hili neno chenji ya rada. Mlitutuma hapa Bungeni mimi, Mheshimiwa Cheyo, Mheshimiwa Zungu na Mheshimiwa Kairuki, tukaenda kule Uingereza kwa niaba yenu. Fedha iliyorudishwa ni fedha yote pound milioni ishirini na tisa na nusu yaani zote na rada mali yetu. Sasa sijui kama hiyo ni chenji au ni nini. Hili neno chenji tu ndiyo huwa linanipa tabu.

Baada ya hapo sasa wachangiaji wetu wa mwanzo ni Mheshimiwa Hamad Rashid, atafuatiwa na Mheshimiwa John Cheyo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE- SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Naomba tufanye mwisho kabisa kwa sababu ya muda wangu mdogo sana. Mheshimiwa Hamad Rashid!

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nawapongeza Waziri na Manaibu wake na watendaji wao wote kwa kazi nzuri walioifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze na Tume ya Pamoja ya Fedha ambapo Waziri sasa hivi ameeleza majukumu iliyonayo. Nilitaka tu Mheshimiwa Waziri aangalie Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 133 na 134 na Katiba ya Zanzibar, Ibara ya 114 na 115 kwamba yale ndiyo majukumu ya msingi ya Tume. Sasa haya aliyoyaeleza hapa nilitegemea atatoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya msingi yaliyomo ndani ya Katiba na hatimaye ndani ya Sheria, kwa bahati mbaya hakufanya hivyo. Nategemea atakapofanya *winding up,* atatueleza haya majukumu ya msingi ya Kikatiba yaliyomo ndani ya Tume ili tuelewe wamefikia wapi. Kwa mfano Akaunti ya Pamoja ya Fedha, *formula* ya mgawanyo wa mchango wa muungano na kadhalika. Hayo ndiyo yamo ndani ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na bahati mbaya

Mheshimiwa Waziri hakuyaeleza. Hili lilikuwa jambo la kwanza ambalo nilitaka atusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nataka niwashukuru sana Serikali ya Marekani kwa miradi ya *MCC*, imetusaidia sana, tuna umeme wa kutosha sasa Pemba na Zanzibar nafikiri karibu Unguja watapata nao umeme wa kutosha na zile barabara wanazozitengeneza ni nzuri, tunawashukuru sana, waendelee kutusaidia lakini tunahitaji na sisi kujifunza katika hilo. Nasema hilo, deni la Taifa linakuwa, tunakopa kwenye miradi ambayo wakati mwingine hatufanyi utafiti wa kutosha. Nitoe mfano ulio hai. Kiwanja cha ndege cha Zanzibar kimekopewa China dola milioni 110, *consultant* aliyekwenda pale anasema akipewa dola milioni 25 atajenga kiwanja kizuri kuliko kile cha milioni 110 na hili linaongezwa katika deni la Taifa. Sasa nasema pengine tunakopa lakini hatufanyi uchambuzi wa kina juu ya madeni tunayoyachukua. Kwa hiyo, tulijiongezea madeni kwa kazi ambazo pengine ni rushwa tu na ufisadi ndani yake unatembea, nasema hayo ni mambo yanahitaji kuangaliwa sana. Deni letu linaweza kukuwa lakini hatufanyi utafiti wa kutosha na mfano hai nimeutoa, ndiyo maana uwanja wa ndege wa Zanzibar umesimama muda mrefu, haujajengwa kwa sababu *consultant* amekataa na kusema kwamba hao wenzao *quotation* zao, *biding* zao walizofanya si sahihi na kadhalika. Naomba sana Serikali iangalie katika kutubebesha mzigo wa deni la Taifa wakati kumbe tuliyokopa ni kukopa hewa kama vile tunavyolipa wafanyakazi hewa na kuna madeni hewa mengi tu tunaomba tuyaepuke. Hili lilikuwa jambo la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni ukusanyaji wa mapato. Nashukuru sana na naipongeza sana taarifa ya Kamati ya Fedha pamoja na ya Kambi ya Upinzani kwamba tunalo tatizo la ukusanyo wa mapato. Nimekuwa nikitoa mfano sana, tuna meli 50 hivi sasa zinavua Bahari Kuu, meli zinazovua *shallow waters*, wanavua *prawns* na kadhalika, wanatozwa asilimia tano (5%) ya *levy*. Meli zinazovua Bahari Kuu wakishatoa leseni hawatozwi kitu chochote yaani ni sawasawa na umetoa leseni ya kujenga kiwanda, halafu unamwambia wewe endesha kiwanda chako, kula kila kitu basi mie kazi yangu nilishakusanya leseni nimeondoka. Biashara ya wapi hii inayotokea duniani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana tulikuwa na meli 77, mwaka huu tuna meli 50 zinavua na hakuna meli iliyoko Baharini ambayo haina *capacity* au *tonnage* ya tani 300, 400, hii fedha inapotea bure, hii ni fedha ya kuvuna, haitaki *TRA* wengi wala nini ni kumwambia mwenye meli *tonnage* yako *weight* yake ni kiasi gani, unategemea kuvuna kiasi gani, tunampigia hesabu ya kodi, tunamwambia tupe asilimia tano (5%) au (6%) ya mapato yako, biashara imekwisha. Hizi fedha zingesaidia kuwalipa Walimu vizuri, kuwalipa Madaktari vizuri, kuwalipa ma-*Engineer* vizuri, kuwalipa wanafunzi vizuri, ni fedha nyingi sana. Meli 77 kwa wastani ya tani 300 kwa msimu ni fedha nyingi sana zinapotea na ushahidi tumeuona hapa tulipokamata meli ile ya Magufuli, dola milioni mbili na samaki zilikuwemo ndani yake, ushahidi ulio wazi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nauliza kwa nini Serikali haikusanyi yale mapato ya rahisirahisi tu? Hayana kazi kubwa wala hayana kutafutana, hayo ni ya kusanya tu

ama unamwambia mwenye meli ukishavua, njoo bandarini, ukishaegesha bandarini hapa weka mafuta, chukua maji kwetu, chukua chakula kwetu, ndiyo wenzetu wanavyofanya kupata mapato. Sasa hii *fishing industry* imeachwa kabisa, matokeo yake ni nini? Tunakwenda kuwaonea wavuvi wadogowadogo kuwanyanyasa na kuwasukuma na kuwatoza kodi ambazo hana hata uwezo wa kulipa. Hebu tuache hii biashara ndogo ndogo, hilo lilikuwa jambo la tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, ni utaratibu wa kupata mikopo. Hakuna benki hapa Tanzania unaweza kuomba mkopo usichukue miezi tisa kupata mkopo wako, *by the time* wakikupa mkopo, hata thamani ya ule mradi wako tayari imeshapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tutafute *mechanism*, tumeona hapa taarifa ya Waziri kwamba Watanzania sasa wamekuwa walipaji wazuri, kwa hiyo, kama mtu ni mlipaji mzuri, lazima apate mikopo kwa urahisi. Maana shida ya kupata mkopo ni kama mtu sio mlipaji mzuri, kama tuna takwimu zinaonyesha asilimia 98 watu wanalipa vizuri, kwa nini bado tatizo la kupata mikopo linachukua muda mrefu? Hili lazima liwe *addressed* ndiyo uchumi wa nchi hii utaweza kufumuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tano, suala la mfumuko wa bei na suala la umaskini. Asubuhi niliuliza swali hapa, nikasema ni asilimia 20 ya Watanzania ndiyo ambao wanatumia mfumo rasmi wa kibenki, asilimia 80 bado pesa ziko mikononi mwa watu. Utaratibu wetu, sisi tunatumia zaidi sana hiyo *monetary policies* zetu ili ku-*control inflation*. Haya yanafanyika zaidi kwa nchi ambazo watu asilimia 98

wanatumia mabenki, sasa kwetu sisi bado asilimia kubwa hawatumii benki. Kwa hiyo, unapoziba ule mfumo wenyewe ndiyo unakuta ndani humu pesa haionekani. Inapokuwa haionekani maana yake unawaongezea watu umaskini na benki haziwezi kukopesha, matokeo yake mzunguko ni tatizo. Sasa mimi ushauri wangu ni kwamba hebu tufike mahali tuwe *focused*, tuangalie maeneo ambayo yatatuwezesha kuondokana na mfumuko wa bei. Tumeona *policy* ya Kilimo Kwanza na kadhalika, lakini *we are not focused*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo tukiulizwa Tanzania tunahitaji tuzalishe tani laki ngapi au milioni ngapi za mchele na zitapatikana katika maeneo gani na gani, tukawa *focused* katika maeneo hayo, tukaondokana na hili tatizo la chakula. Hili ni tatizo rahisi sana kulikabili lakini bado tumeendelea na taratibu zetu za kawaida na kwa maana hiyo bado uzalishaji wetu umeendelea kuwa duni *day by day*. Kwa maana hiyo tutaendelea kuwa na umaskini kwa sababu mzunguko wa fedha kwa mfumo tunaoutumia haumsaidi mtu kuweza kupata fedha kwa urahisi na hilo linaambatana na nini? Linaambatana na hata madeni ya ndani hayalipwi. Kama hulipi madeni ya ndani, maana yake mzunguko wa fedha ndani ya nchi haupo, Serikali ndiyo inafanya biashara kubwa na bado madeni ya ndani hayalipwi, tumeyasema haya miaka na miaka lakini bado tunaendelea na utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, moja, tuhakikishe tunauwa *focused* kwamba tunataka kuondoa tatizo la chakula na ni kazi ya miezi mitano, sita, saba tukijipanga vizuri tunaweza kuifanya kazi hiyo na chakula ni pamoja na samaki. Tunaweza kabisa vilevile tukajipanga

vizuri, tukahakikisha tunakusanya kodi za Bahari Kuu na samaki wale wanaovuliwa, wanatupwa baharini angalau wakaja huku wakasaidia kupata chakula, linawezekana kufanyika hilo. Sasa haya ni mambo ya kujipanga tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho ni suala zima la kusimamia bajeti. Tuna tatizo la msingi la kusimamia bajeti. Tumeona makusanyo ya mapato, lakini kila Wizara iliyokuja hapa ni asilimia 50 mpaka 63 ndiyo wamepewa bajeti yao, sasa unauliza kama kweli tumepitisha bajeti, makusanyo yametokea asilimia 98, hii fedha imekwenda wapi hata Wizara isipate fedha zake? Tena sio kupata fedha tu hata kupata fedha yenyewe kwa wakati, hata hiyo ndogo inayotoka nayo haitoki kwa wakati. Kuna tatizo la usimamizi wa bajeti. Sasa nafikiri kilio chetu cha Wabunge, Kamati, tunaomba sasa usimamizi wa bajeti uwe imara zaidi na kwa maana hiyo basi mtu awe *accountable* pale ambapo ameshindwa kusimamia bajeti. Huu utaratibu wa kuja hapa tukaambiana nimepata asilimia 56, haelezwi ni nani aliyesababisha upate asilimia 56 wakati mapato na matumizi ya Serikali yanaonekana tofauti. Haya lazima tuelezwe na haya ni matatizo ya msingi, nafikiri yatakuwa *addressed* na mimi nashukuru sana Mheshimiwa Waziri kama atakabiliana na hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa ni suala la *interest rate,* bado ni kubwa; 13%, 20%, haiwezekani kabisa, tunahitaji nalo liangaliwe, itafutwe *mechanism* ya kuangalia *interest rate.* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nakushukuru sana kwa niaba ya Wananchi wa Bariadi na Chama cha *UDP. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kabla sijatoa mchango wangu, nataka kutoa tahadhari moja. Nasikia kila wakati mfumuko wa bei uteremke na tutumie njia ya kuhakikisha bei ya chakula haipandi; ni matumaini yangu mnapofikiria hivyo, hamna fikra ya kuwafanya wakulima wapate bei nzuri, kila wakati wanapata bei ya chini, waendelee kuwa tu watumishi wa Ghala la Taifa. Napenda *clarification* kwa jambo hilo kwa sababu, walio wengi katika nchi hii ni wakulima na wenyewe lazima tuwaangalie, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninalotaka zaidi kuchangia ni mfumo wetu wa bajeti. Tumekaa katika Kamati, kama unavyofahamu, Kamati ya Utawala ya Bunge, *Steering Committee,* tumefanya semina na tunaona jinsi tunavyoendesha bajeti yetu, tumebakia ni sisi tu katika *East Africa* ambapo tunaendesha mchakato wa bajeti mpaka mwezi, karibu sasa tunamaliza mwezi wa nane na bajeti ilipaswa kumalizika tarehe 30 mwezi wa Juni; Zambia hawafanyi hivyo, Kenya hawafanyi hivyo, Uganda hawafanyi hivyo, mimi nafikiri kwa nini tusiige basi mfano wa watu wengine ili ifikapo tarehe 30, tuwe tumemaliza kabisa mchakato wa bajeti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri angelitaja jambo hili, angalau ile nia ya kuanza kulifikiria, lakini nimemsikiliza kwa makini kabisa, naona ataendelea tu hata mwaka kesho na mtindo huohuo ambao umepitwa na wakati. Tungependa uhakika

wakati wa majumuisho, atuambie mwaka unaokuja tunageuza kwamba tarehe 30 itakapofika, mchakato wa bajeti utakuwa umeisha na tarehe 01, kila mmoja awe na mafungu yake na aanze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunavyozungumza, tunavyojadili, hata Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali amesema katika ripoti yake, hauna tija. Kwa sababu, kuna sababu gani tuzungumze juu ya *general budget* siku za kwanza, halafu tunapitisha *main frame work,* halafu baadaye tunakaa hapa miezi miwili, wote tunalalamika, hela hii haitoshi, hiki hakipo, sijui hii ingekuwa kipaumbele ili Waziri afanye nini wakati tayari tumeshapitisha *main frame work* ya bajeti? Kwa hiyo, tunapokuja mwisho mwisho huku ni sawasawa na sisi wote tunapeana ma-*rubber stamp* tu, tunapiga aah, ndio, twende na sasa hivi kwa sababu hatuna muda ndio kabisa kwa mafungu, twende. Mimi naona hatuwatendei haki Watanzania, ni afadhali sasa tuanze kuzungumza kwanza bajeti za sekta, tunazimaliza, tunamaliza na ya Wizara, ndio Waziri afanye majumuisho na ku-*consolidate the budget* ambayo ndio inakubaliwa na Bunge zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nishukuru kwamba, nafikiri jambo hili lingefanywa haraka ili mwaka kesho na sisi tunapotembea kule nje tujivune kwamba na sisi sasa tuna mtindo mpya wa kisasa na ulio na tija wa kubadili bajeti yetu. Hivyohivyo Bunge, ninatumaini katika mwaka utakaokuja tutakuwa tayari tumetengeneza *Budget Committee,* tumetengeneza *Parliamentary Budget Office,* ili tuweze kuifuatilia bajeti yetu mpaka mwisho ili kuhakikisha sio kwamba tunaikubali halafu tunaiacha, ikimalizika tunakuja tena tunakubaliana karibu mambo yaleyale.

Natumaini haya mambo mawili yakifanyika vizuri katika mwaka huu, tutakuwa na utaratibu ulio mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, mapato. Nimeona hata leo, Waziri amethibitisha tena; upande ambao haufanyi kazi kwenye bajeti yake ni upande wa maendeleo. Hii ni kwa sababu, upande wa maendeleo unategemea zaidi fedha ya kutoka nje, fedha ya wafadhili, ambao hatuna utaratibu nao, ambao unatofautiana hata na mwaka wa bajeti. Kwa sababu, zaidi ya wafadhili wengi, miaka yao inamalizika mwisho wa mwaka na sisi mwisho wa mwaka karibu tumeshamaliza miezi sita (6) ya bajeti yetu. Kwa hiyo, ni vigumu hata kama ulikuwa na nia nzuri kwamba hizo fedha zote ambazo tumekubaliwa zitaweza kufika katika wakati ambao ni wa bajeti. Kwa hiyo, kila mahali *performance* ya upande wa bajeti ya maendeleo ni *50%, if we are lucky,* lakini ni zaidi katika sehemu nyingine na zaidi umeme, maji na sehemu hizo kwa kawaida pesa hizo hazipatikani; sasa mtindo huu hauwezi kuendelea. Kwa hiyo, mimi nilitegemea kwa kujua kwamba nchi hii na sisi tumepata vitu kama gesi na mambo mengine, Waziri angetupa angalau ahueni ya kusema jamani katika miaka mitano (5) inayokuja au miaka miwili (2) inayokuja, bajeti yetu ya maendeleo itakuwa *fully funded* na pesa ambazo zinatoka ndani ambazo tuna uhakika nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa nilipokuwa natembelea Kigali, waliniambia kwamba bajeti yao wanapoisoma *is fully funded,* sio bajeti ya *deficit* labda Mungu akipenda, atatupa pesa, hapana! Kwa hiyo, unakuta yeye kule anatumia zaidi ma-*Regional Commissioner* wake, ma-*DC,* Mheshimiwa Rais anawaita, anamwambia kwamba, pesa ninazokupa ni hizi na zitakuja

sasa lakini nataka kuhakikisha yaliyosemwa kweli utayatenda. Sisi hatuwezi kufanya hivyo kwa sababu kila *Accounting Officer* ukimuuliza mbona hukutimiza hili, anasema *I am sorry,* Hazina na kila wakati unaambiwa Hazina haikunipa hela; sasa huyu Hazina, ambaye hatoi hela anakuja hapa kufanya nini kama hatoi hela ambazo tumemwambia tumekukabidhi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, *we must have a budget* ambayo iko *fully funded.* Mimi naona njia moja ni kuhakikisha kwamba vyanzo vyetu vya mapato viwe vya uhakika. *TRA* kila siku wanasema wanapanda, wanapanda sawa; leo hapa nimeona kwamba mwaka jana ilikuwa shilingi trilioni sita (6), mwaka huu tunatakiwa shilingi trilioni nane (8), Mungu atubariki, kama kweli tutapata shilingi trilioni nane (8) kwa hali halisi ya uchumi wa mwaka huu, sijui itakuwa namna gani? Ni matumaini yangu hamkum-*force* mtu wa *TRA* awape shilingi trilioni 8 (8) ili ku-*balance* tu mahesabu lakini mimi nina mashaka kama pesa zote hizi kweli zitaweza kupatikana. Kwa hiyo, tunahitaji kufanya kila nguvu ili tubuni vyanzo vipya vya mapato vilivyo na uhakika vya kuweza ku-*fund budget* yetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, jambo lingine, Waziri amezungumzia juu…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa…

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *what do you mean?* Hii ni kengele ya kwanza Mheshimiwa!

**NAIBU SPIKA:** Ya kwanza? *Okay,* endelea!

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *thank you, you are good men. (Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, *weakness* kubwa ya Serikali ninayoiona ni kutojali mali zake, haijali kabisa. Ina magari zaidi ya *50* trilioni*, I think if I can remember,* yatakavyo-*disappear* hakuna mtu anayejua, lakini yatakwenda tu. Serikali ina majengo kila mahali, kuna majengo ya Ubalozi, mengine yako katika *very expensive areas* kama vile London, hakuna aliye na *register,* hakuna anayejali, mengine yanapasuka yanakaa namna hii. Waziri ndiye ndiye aliyekabidhiwa kazi ya *assets,* viwanja vya Serikali, havijulikani wala havina hati, kwa hiyo, ndio maana watu wengine wanaweza kuingia pale na siku hizi ardhi ina matatizo, anaingia pale na huna njia ya kisheria ya kuweza kumzuia, *asset* ndio mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri hebu mliwekee jambo hili mkazo, tujue *assets* zetu ni ngapi na tujue ni nani anaangalia, *is it Treasury Registrar, is it Tanzania Building Agency* kwa upande wa majengo? Sheria itamke hivyo ili pasiwe na jambo lolote ambalo halijulikani sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG.* Natumia nafasi hii kumpongeza *CAG* na watu wake kwa kufanya kazi nzuri mpaka kuteuliwa kwenda Umoja wa Mataifa. Nawatakia kila la kheri na ndio hii heshima ya Tanzania na ni heshima ya Bunge hili kwa kumuimarisha *CAG* wetu, afike mahali ambapo anaweza akaonekana huko nje. Lakini sasa bado

kuna matatizo kidogo, pesa kweli *Public Accounts Committee* tunakubali na huzigeuzi kisheria lakini inapokuja kwa kumpa hela zote bado na yenyewe anasuasua.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Kazi ya *CAG* ni muhimu, pesa zote zipelekwe na mengine yote.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Mbatia!

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia muda huu niweze kutoa mchango kidogo kwenye Wizara hii yetu ya Fedha. Nina shida kidogo kwa sababu, majukumu yetu sisi Wabunge ni manne (4); la kwanza kwa Taifa letu na kila Mbunge anayezungumza hapa anaweka kipaumbele kwenye jukumu lake Kitaifa kwanza, halafu mengine yatafuata. Sasa tukifikiri kwa mapana, *let us think globally but act locally,* wenzetu duniani wanafanya vipi katika uendeshaji wa Serikali zao na sisi hapa kwetu tunafanya vipi? Kwa nini tunalalamika zaidi na tunasema sana lakini vitendo vinakuwa ni kidogo zaidi? Kwa nini tumefikia mahali tunataka huduma lakini hatupendi kufanya kazi, tuwe wakweli. Ukiangalia sekta zetu nyingi uadilifu wao, uwajibikaji wao, utamaduni ambao unakua siku hadi siku katika Taifa letu; wachache wanafanya kazi wengi hawafanyi kazi. Tunasifia *TRA,* sawa inafanya kazi nzuri; je, sheria zetu tunazotunga hapa zinazoendana na mapato zikoje? Nitatoa mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Sheria ya Kituo cha Uwekezaji *(TIC),* wakishatoa cheti cha kuruhusu mwekezaji aweze kuingiza bidhaa, hasa za kwenye sekta ya ujenzi, *deemed capital goods,* hawana Wataalamu wa *Quantity Surveyors* wa kuweza kuhakiki je, bidhaa hizi zinazoingizwa ni sahihi kwa mradi uliokusudiwa? Hali kadhalika *TRA* hawana wataalamu hao na ndio maana unaweza ukakuta mwaka wa fedha uliopita, kwa miezi nane (8) tu, kuanzia mwezi Julai mpaka mwezi Februari mwaka huu, kwenye *area* ya *TIC,* kwenye ukwepaji huu na misamaha ya kodi kwenye *area* hii, ilikuwa ni zaidi ya shilingi 179.8 bilioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu tunasema kwamba Taasisi kwa mfano za dini, ndio zinasamehewa kodi, lakini kipindi hicho Taasisi za Dini zimesamehewa shilingi milioni 114 tu. Lakini ukienda kwenye *mining* na kama *TIC* na kwingine huko unakuta msamaha wa kodi kwa muda wa miezi nane (8) ilikuwa ni shilingi trilioni 1.05. Shilingi trilioni 1.05 wakati Wizara ya Elimu, jana tumepitisha bajeti yake hapa ya shilingi bilioni 700 hivi. Sasa tunajiuliza, ndio maana nilisema *let us think globally but act locally,* rasilimali kubwa kuliko yote ambayo tunaweza tukawekeza na ikawa na matumaini na manufaa kwetu sisi ni rasilimali watu. Tunaweza tukazungumzia suala la madini yatapita, tukazungumzia gesi itavunwa itakwisha lakini je, rasilimali watu tumewekeza namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano, ili nieleweke vizuri. Ukichukua nchi kama ya Uholanzi, Uholanzi nchi yao ina kilometa za mraba 36,000 tu. Hawana rasilimali kama za kwetu hapa lakini *population* yao ni zaidi ya milioni 16, wameweza kusukuma maji waka-*reclaim land from the sea,*

wakaweza kujenga bandari ya Rotterdam, wakajenga uwanja wa ndege wa Amsterdam, Schipol Airport, ndizo *source* zao kuu za mapato ya kuendesha Serikali yao na kutoa misaada duniani kote. Wamesukuma maji, wakapata ardhi, wakajenga bandari, wakajenga uwanja wa ndege. Hii ni *human resource.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa kwetu tunazungumza sana, suala la maadili, uwajibikaji, suala la ufisadi ambao umetamalaki, ni hulka ya mwanadamu kukataa kulipa kodi, lakini je, uadilifu huu katika kutokulipa kodi ukoje? Kwa nini, inakuwa hivyo? *I think we need spiritual counceling rather than* kuzungumzazungumza tu. Yaani, tunatakiwa tuponywe kiroho kwanza kama Taifa kwa sababu kila siku tutakuwa tunaimba, kila siku ufisadi, ufisadi, ufisadi, ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuchukue taasisi, tuwe wakweli tu, tuchukue taasisi, wala sina tatizo nao; taasisi kama *Agakhan Foundation, Agakhan Foundation* tangu kuanza kwa Taifa hili, tangu Serikali ya Awamu ya Kwanza hawalipi kodi, kwa nini wakati taasisi nyingine zinalipa kodi? Eti wana *a presidential diplomatic status order,* ili waweze kuhudumia walalahoi. Ni walalahoi wa namna gani nchi hii wanaotibiwa *Agakhan?* Ni walalahoi wa namna gani nchi hii wanaosoma kwenye shule za *Agakhan? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tulinganishe tuwe wa kweli tu. Hata kama mtasema wengine labda *NCCR* hamjaingia madarakani, msubiri na nyie muingie muone, lakini tunazungumzia suala la utu. Utu wa mwanadamu huwezi ukaulinganisha na kitu chochote kile. Tukiangalia wawekezaji kwenye sekta labda tuseme ya ardhi, je, ardhi

kama Mzee Cheyo amesema hapa, suala la *asset* kama ardhi je, wanailipia kodi kwa kiasi gani wakati ardhi iko kwetu hapa Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiwa makini na tukawa wa kweli, Bunge hili linayo nafasi kubwa. Nakumbuka mwaka 1648 wakati wenzetu kule Ulaya wanatoka kwenye Ukabaila kwenda kwenye Ubepari, walianzisha kitu kinachojulikana kama *Democratic Principle, no representation no taxation.* Sasa *taxation* ambao ni walipa kodi hawa wa Tanzania hii, hizi kodi zinazokusanywa kwa Watanzania hawa, kuna suala la *Direct Taxation and Indirect Taxation.* Kodi tunazozungumzia zaidi hapa, tunazungumzia *Indirect Taxation, how about Direct Taxation?* Wafanyabiashara ambao ni wakubwa wakubwa, wanakwepa kodi, wanaenda huku wanafanya ujanjaujanja, lakini tukiwa wa kweli wa dhati wa dhamira zetu, kwa nini wanafanya hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa Bunge ndilo lenye dhamana kwa ajili ya Watanzania, ndio lenye dhamana kwa ajili ya walipa kodi, inabidi tujitafakari upya, tuangalie mifumo yetu. Tunaweza tukazungumza, tukapambana hapa na Waziri na Manaibu wake, lakini je, mifumo tuliyojiwekea ya kukusanya mapato, mifumo tuliyojiwekea ya kuhakikisha kwamba Taifa linaingia kwenye mistari iliyo sahihi, mifumo tuliyojiwekea ambapo leo hii tumeingia kwenye mfumo ambao sio rasmi, hatujaurasimisha, mfumo unaoitwa ufisadi, kila mahali tunasema, ni mfumo ambao haujaingia rasmi, lakini tuwe wa kweli tu kwa sababu, dhamira zetu kila kona unashindwa kujua nani amfunge paka kengele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu upo kila kona unaenda hapa na hapa, leo unaiba huku, unaiba kule; sasa tukidhamiria na tukawa wa kweli kwa Taifa letu, tukaweka utu wa huyu mwanadamu mbele, maeneo mengi angalia majengo kama ya Jiji la Dar-es-Salaam ambayo mengi yako Kariakoo, katikati ya Jiji, makubwa makubwa tu ambayo yamekua kama uyoga yale, hebu yaangalie je, yanalipa kodi? Je, bidhaa zilizojenga majengo hayo zimelipiwa kodi? Je, huyu anayejenga jengo leo kwa kusamehewa kodi, kesho anauza jengo lake kwa *market value,* wakati hakulipia kodi wakati wa kujenga jengo hilo, tumethamini kiasi gani? Uadilifu uko mkubwa kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo, leo hii tutazungumza mengi tu, lakini nina uhakika na ninaweza nikaisaidia Wizara kuwaambia jengo hili halijalipiwa kodi, jengo hili halijalipiwa kodi, jengo hili halijalipiwa kodi na wamefanyafanyaje wakiwa wanafanya uharamia huo na watu ambao sio waadilifu katika Taifa hili. Kwa hivyo, ili tuwe wa kweli na Taifa liweze kufika kwenye mstari, wote hapa, wenzetu wa CHADEMA watasema, ‘*Peoples’ Power’,* wengine mtasema, ‘Kidumu Chama cha Mapinduzi’, wengine *NCCR* mtasema, ‘Pamoja Tutashinda’, wengine watasema, ‘*UDP* Upendo Daima’, wengine *TLP* watasema, ‘Uhai wa Mtanzania’, *CUF* watasema, ‘haki sawa kwa wote’, lakini siku ya mwisho Tanzania itabaki ni hii moja.

Sasa kama Tanzania ni yetu sisi sote kwa pamoja na tunaweka maslahi yetu kwa pamoja na tunafikiri kama Taifa kwa pamoja, hebu tusirushiane madongo sana bali tutiane moyo ili Taifa letu la Tanzania lifike mahali

tuhakikishe sisi kama Taifa la Tanzania tunafika mahali ambapo ni sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafika mahali ambapo Taifa la Tanzania kama mwingine akiona, basi hata mwingine akiingia madarakani, sote tunabaki kuwa salama, lakini kutiana hofu na uaminifu ukikosekana Taifa letu litakwenda mahali ambapo siyo sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote ni Watanzania, basi tuweke Utanzania na Utaifa wetu mbele na hakuna mtu mwenye hati miliki ya mawazo. Wazo lolote lile ni zuri, hata kama limetoka kwa mtu usiyempenda, chukua wazo lake, usiangalie sura yake, lakini tukianza kurushiana madongo naamini hatutafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Lakini kwa dakika chache zilizobaki namwita Mheshimiwa Luhaga Mpina!

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, lakini niwashukuru pia watoaji wa hotuba waliotangulia hususani Makamu Mwenyekiti wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Kitandula na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Kivuli, Mheshimiwa Zitto Kabwe kwa hotuba zao nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia katika hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi, Mipango na Utawala nilisema kwamba kulingana na taarifa ya *Global Financial Integrity Report* ya mwaka 2008 Tanzania

imepoteza trilioni 11 katika miaka 39 na Tanzania ni nchi ya 13 kati ya nchi 20 zinazoongoza kwa utoroshaji wa fedha nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niliainisha kwamba, Taasisi za Serikali zinalifahamu suala hili, TAKUKURU wanalifahamu, Benki Kuu wanafahamu, *Financial Intelligence Unity* wanajua, lakini cha kushangaza ni kwamba, toka mwaka 2008 taarifa hii itolewe Serikali haijachukua hatua yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye Gavana wa Benki Kuu alijibu kupitia gazeti la Mwananchi la tarehe 5/7 akisema kwamba, taarifa hizo Serikali haina na siyo lazima kila taarifa ambayo Mheshimiwa mmoja au mwananchi mmoja anaweza kuwa nayo sisi tunayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nasisitiza kuwa Serikali inafahamu, taarifa hizi za *Global Financial Integrity* inazo na ndiyo maana katika Mpango wa Maendeleo *first draft* iliyotolewa mwezi Agosti, 2011 ime-*quote* taarifa ya *Global Financial Integrity* katika ukurasa wa 71. Kwa hiyo, Serikali kusema kwamba haina taarifa hizi siyo kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa ni Serikali iseme na iamue kwa dhati yaani iwaambie Watanzania utafiti uliofanywa na Shirika hilo una ukweli gani na kama kuna ukweli hatua gani za makusudi ambazo zinachukuliwa kwa sababu *report* ile imeainisha mwaka hadi mwaka fedha zilizokuwa zikitoroshwa kwenye mabenki nje ya nchi.

Nimekuja kuona taarifa nyingine za juzi za Uswisi ambazo amezitaja Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambazo

hizi ni matokeo kwa sababu ndiyo *average* yenyewe ya fedha zinazotoroshwa kila mwaka wa fedha kwenda kwenye mabenki nje ya nchi yanakwenda kufichwa na wafanyabiashara wakubwa, lakini na watendaji wakubwa wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuona hayo, Serikali inasema haina taarifa hizo. Naomba kwa idhini yako leo sasa hivi, nikabidhi taarifa ya *Global Financial Integrity Report of 2008* yenye *heading illicit Financial out Flow From Africa Hidden Resources for Development* inayoonesha ubadhirifu wa fedha wa kuanzia mwaka 1970 mpaka mwaka 2008 ambayo inaonesha Tanzania ilipoteza dola milioni 7356.4 ambazo ni sawasawa na trilioni 11.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikabidhi *report* ya Ndikumana *and Boyce* ya mwaka 2008 ambayo nayo inaonesha utoroshaji wa fedha za umma wa kuanzia mwaka 1970 mpaka mwaka 2008 na upotevu wa fedha uliobainishwa katika *report* hiyo ni dola milioni 5185 ambayo ni sawasawa na trilioni 8.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba nikabidhi *report* ya Dev Kar *and* Devon Cartwright-Smith ya mwaka 2008, *A List Financial Flow From Development Countries* ya kuanzia mwaka 1970 mpaka mwaka 2004 ambayo nayo inathibitisha wazi kwamba, Tanzania ilipoteza dola milioni 6,561 ambayo ni sawasawa na trilioni 10.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba nikabidhi *report* ya juzi ya *the One Billion Dollar Question on How Can Tanzania Stop Losing so Much Tax Revenue* ambayo

inaonesha wazi kuwa kila mwaka Tanzania imekuwa ikipoteza dola 300 ambazo ni sawa na bilioni 478.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kuzikabidhi *document* hizi Serikalini ni kwanza kumaliza mzizi wa fitina kwamba Serikali hawana *documents* hizi, lakini pili ni kuhakikisha kwamba Serikali inazichunguza taarifa hizi na kuchukua hatua zinazostahili na kuliarifu Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikabidhi *documents* hizi kama nilivyoziainisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Naomba uniletee mezani hapa kama umeshamaliza kuchangia.

**MBUNGE FULANI:** Endelea tu!

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Nilete?

**NAIBU SPIKA:** Kama umeshamaliza kuchangia zilete tu.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, *okay*! Baada ya kumaliza dakika zangu nitakuja kukabidhi rasmi mezani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumza suala la upotevu wa rasilimali za umma, lakini suala zima kubwa kabisa la upotevu wa rasilimali nyingi za umma ni kwamba, Sheria za Fedha zote zinazosimamia rasilimali hii ya Taifa bado hazijakaa sawasawa, zinahitaji marekebisho makubwa ili ziweze kuwa na nguvu ya kudhibiti upotevu wa fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Serikali kupunguza matumizi yake bado tunaendelea kusisitiza kwamba Serikali ina uwezo kabisa wa kupunguza matumizi yake, hata kipindi hicho nilichokuwa nasema Serikali inaweza ikapunguza matumizi yake ya shilingi bilioni 500 ili kufidia katika miradi ya maendeleo na bado mpaka sasa hivi ukipitia vitabu vyote inaonesha kabisa kwamba Serikali ina uwezo wa kupunguza matumizi hayo, lakini ambacho bado kinakosekana ni dhamira ya dhati ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo nataka nilisisitize ni suala la Mashirika ya Umma. Kila siku si Waziri, si Kamati zinatangaza kuanzishwa kwa Mashirika ya Umma yaani utitiri wa kuanzishwa kwa Mashirika ya Umma, sasa hivi katika matumizi yetu ya Kawaida trilioni 1.7 inagharamia Mashirika ya Umma na kila siku yanatangazwa na yanakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Tume ya Mipango ianze kupitia upya kwanza uhalali wa kuwepo Mashirika yote hayo ya umma kama bado tunayahitaji katika uchumi wa sasa hivi kwa sababu mashirika mengine yanafanya kazi ile ile. Wizara inafanya kazi hiyo na kuna idara katika Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile kuna taasisi inayofanya kazi hiyo, matokeo yake Serikali imekuwa na mzigo mkubwa na Serikali imekuwa ni kubwa, fedha za Watanzania zinakwisha ku-*service* tu ukubwa wa Serikali, lakini fedha kwa ajili ya wao kuwafikia kwenye maendeleo imekuwa ni tatizo kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwa dakika chache zilizobaki kwamba, fedha tunazo nyingi ukiondoa kupunguza matumizi ya Serikali kwa ajili ya kuongeza kwenye miradi ya maendeleo lakini vile vile hizi fedha tunazozizungumza nchi kama Peru, Nigeria na Philippine, wao kama kila mwaka hutenga fungu kwa ajili ya kupokea fedha na kuzitaifisha fedha na kuzifilisi akaunti za watu ambao wametorosha fedha na kwenda kuficha Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaweza kabisa katika mwaka huu wa fedha tukaamua kutengeneza utaratibu wa kuhakikisha kwamba, kila mwaka tunaziokoa hizo fedha ambazo zimefichwa kwenye mabenki Ulaya na tunaweza kufanya hivyo. Kadhalika tuna uwezo wa kukusanya, siyo chini ya bilioni 500 kila mwaka kwa kutaifisha tu hizo trilioni zetu 11 ninazozizungumza zilizopo huko tukaanza kuzichukua kidogo kidogo bilioni 500 kila mwaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile sasa hivi kuna fedha za umma nyingi sana ambazo zimeachwa kwenye akaunti mbalimbali yaani *unclaimed funds*. Lakini ni kwamba watu mbalimbali, hisa mbalimbali zinazoombwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam, halafu kuna madai mbalimbali ya watumishi wa umma ambao wengine walishafariki na hawajulikani walipo na ambao wengine walishaachishwa kazi lakini bado wakaendelea kulipwa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa fedha hizi ni nyingi sana zinakaa kwenye mashirika na kwenye *Pension Funds* na kwenye mabenki lakini hizi siyo mali za mabenki wala sio mali za *Pension Funds...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mpina. Nimepata ushauri pia kwamba hizo *report* Mheshimiwa Waziri wa Fedha zipo *online,* kwa hiyo mnaweza mkazipata kwa urahisi zaidi.

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na uchangiaji jioni kwa sababu muda ni mdogo sana tutaanza na Mheshimiwa Mrema na Waheshimiwa Wabunge tutaendelea kwa sababu muda wetu ni mchache mno.

Nimemwona Mheshimiwa Sendeka, nakuomba utumie dakika moja tu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona, nimesimama kuomba Mwongozo wako chini ya Kanuni ya 68(7), kufuatia hotuba iliyotolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani wa Wizara ya Fedha Mheshimiwa Zitto Kabwe, mmoja wa Wabunge ninaowaheshimu sana.

Akidai katika ukurasa wa tisa wa hotuba yake kwamba, kuna Shilingi bilioni 315 zilizopo Uswissi zinazodaiwa kuwa ni za Viongozi wa Serikali na wafanyabiashara. Lakini miongoni mwa viongozi hao ni pamoja na Kiongozi mkubwa sana wa Serikali au Kiongozi wa juu kabisa wa Serikali ya Tanzania na kwamba fedha hizi zinatokana na

ugawaji wa vitalu vya utafutaji wa gesi katika Ukanda wa Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuhuma hizi ni kubwa sana na hakuna Kiongozi wa Serikali aliyesimama kuomba majina haya yatajwe, ni tuhuma ya jumla jumla, lakini inaweka *image* ya Serikali mahali pabaya sana na kwa maana hiyo, ukimya huo unaweza kutafsiriwa tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama kuomba Mwongozo wako, ili kulinda hadhi ya Bunge kuepusha tuhuma za jumla jumla na kulinda heshima ya Serikali katika suala hili ambalo ni nyeti sana la kuhusishwa na utoroshaji wa Shilingi bilioni 315, fedha za walalahoi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kwamba nani abebe mzigo huu, ni Mheshimiwa Zitto ataje majina ya wanaohusika au Serikali iwataje viongozi hao wanaohusika katika utoroshaji wa fedha hizo ambazo zimekwenda ughaibuni ili kila mmoja abebe msalaba wake pindi itakapothibitika kwamba fedha za wananchi wa Tanzania zimepelekwa nje ya nchi bila kufuata taratibu za kisheria. Ni fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Chief Whip* nini tena?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu kwa kuhusiana na Mwongozo ambao umeombwa punde.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu uliopo kwenye kanuni za Kudumu za Bunge unasema, kama kuna Mbunge anadhani anayosema anasema uongo, kanuni ya 64 (1) inasema omba utaratibu, sema kwamba huyu anayezungumza, hiki anachokizungumza siyo cha kweli. Pili, utaratibu huo unasema, ukishasema anasema uongo unatakiwa uthibitishe huo uongo. Tatu, ukishathibitisha huo uongo huyo aliyekuwa anasema ndiye anatakiwa sasa athibitishe kauli yake.

Sasa hiki kinachoombwa nani athibitishe, alitakiwa amkatishe wakati anazungumza aseme hizo taarifa unazosema siyo za kweli na atoe uthibitisho wake mwenyewe, halafu ndiyo Mheshimiwa Zitto apewe huo mzigo anaoudai.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu Mwongozo unaoombwa hapa siyo mahali pake. Naomba Kiti chako kisishiriki katika kukanyaga kanuni za Bunge.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na nakushukuru sana *Chief Whip,* lakini ulichofanya ni kukifundisha Kiti jambo ambalo siyo wajibu wako. Nikishaombwa nifanye kazi yangu unatakiwa uniache tu na unipe nafasi.

Sasa kwa dakika moja ambayo bado ninayo, nianze na Mwongozo wa Mheshimiwa Deo Filikunjombe wa kuhusu Waheshimiwa Mawaziri kutaja majina wakati wanapojibu hoja ni kwamba inachukua muda.

Ni kwamba, huu umekuwa ni utaratibu humu ndani lakini jambo hili ni pendekezo ambalo ni vizuri Kamati ya Uongozi ikaja kulijadili baadaye na kuona namna gani ya

kuenenda. Baadhi yenu msipotajwa majina, mnanuna kwelikweli. Sasa huu ndiyo umekuwa mtihani, lakini tutaliangalia mbele ya safari.

Kuhusu Mheshimiwa Kangi Lugola, yeye alisema kwamba Serikali imejibu swali namba 382 la Mheshimiwa Kakoso bila kuonesha ni mpango gani, inasema tu imejipanga vizuri na kadhalika.

Hapa nimemshangaa kidogo Mheshimiwa Kangi Lugola kwa sababu swali namba 382 lilikuwa *very specific* kwamba, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa zahanati katika Vijiji vya Vitonge, Bunge, Ngomalusambo, Igalula, Kasinde na Bujombe, *very specific.*

Lakini Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI katika majibu yake ambayo nimetaka nipate *original* kabisa amejibu kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda mwaka 2012/2013, imetenga shilingi milioni 176.7 kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) ambao ndio unahusika na masuala ya ujenzi wa zahanati na vituo vya afya.

Halmashauri imeweka kipaumbele cha kutumia fedha hizi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi na Zahanati za Kapalamsenga, Sibwesa, Milala, Kasekese, Kabungu na ukarabati wa Zahanati za Msimbo na ukarabati wa Kituo cha Afya Mwese na kadhalika.

Waheshimiwa Wabunge, hivi vijiji ambavyo Mheshimiwa Kakoso alivitaja kwa fedha ile ambayo wametenga wao wenyewe kwenye bajeti yao na Madiwani wake wamelenga katika vijiji vingine, yaani

walipewa fedha lakini wamepeleka katika vijiji kadhaa, halafu Mheshimiwa anauliza Bungeni vijijini vingine ambavyo yeye na wenzake walipaswa kwa fedha walizopewa waziwekee vipaumbele katika hivyo, sasa Serikali ishike la nani?

Ishike la Madiwani na Mbunge kwa pamoja kama vipaumbele au ishike vya Mbunge humu ndani? Sasa hili naamini kabisa ni la Madiwani wa Mpanda na Mbunge akiwepo kuamua kipaumbele chao kiwe nini. Kwa hiyo, kwamba jibu halikuwa sahihi, hapana! Ni kwamba Mheshimiwa Kangi Lugola hakusikiliza tu jibu lake, hili lilikuwa ni swali *very specific* na limejibiwa katika *specificity* hiyo hiyo.

Kuhusu hili la mwisho la Mheshimiwa Ole Sendeka ni lazima nipitie nione tena hotuba ya Mheshimiwa Zitto Kabwe ilikuwa inahusu nini na kama kuna tatizo lolote katika hotuba hiyo jioni ya leo nitaelezea.

Mwisho kabisa, kuna wageni na naomba kuwatambulisha. Yuko mtangazaji maarufu Bwana Seleman Semunyu wa *ITV*, ni mara ya kwanza kuingia katika Bunge letu. Karibu sana pamoja na watangazaji wenzako ambao mmefuatana katika Bunge letu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili jioni. Mnaombwa kuwahi ili tumalize shughuli hii ya Wizara ya Fedha kama ilivyopangwa. Ahsanteni. (*Makofi*)

*(Saa 7.15 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 10.00 jioni)*
*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge majadiliano yanaendelea na kwa hiyo wachangiaji wangu wale waliowahi ndiyo hao hao nitakaowapa nafasi. Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, mchangiaji wa kwanza.

**MHE. AGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitakushukuru sana. Naona leo umetupanga vizuri katika uchangiaji vyama vyote, hukujali kikubwa au kidogo. Umeanza na *CUF, UDP, NCCR* Mageuzi, CCM na sasa hivi *TLP*. Hongera sana kwa ulivyotulea leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetumwa na wakulima wa kahawa wa *KNCU* niyaseme haya nitakayoyasema leo. Jambo la kwanza itakumbukwa kwamba, mwaka 2008/2009 kulikuwa na mdororo mkubwa wa uchumi na Serikali yetu ikafanya vizuri sana ikatafuta ruzuku kwa ajili ya kuwafidia wakulima wa pamba na wakulima wengine ili waendelee kuwa kwenye uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wakulima wa pamba walipata fidia. Ni kazi nzuri ambayo Serikali ilifanya. Hata sasa hivi ukienda Ngorongoro, Monduli, sijui na Wilaya gani nyingine, wakulima wamesaidiwa fidia na Rais wetu amekwenda katika Wilaya hizi kugawa ng'ombe ili kuwasaidia wafugaji wasididimie.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa upande wa wakulima wa kahawa Moshi tuna kilio, tuna malalamiko makubwa, nashukuru leo Waziri wa Fedha yupo, Naibu Mawaziri wake wawili wapo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha yupo na Gavana wa Benki Kuu pia yupo, kwamba

wakulima wa kahawa wa Kilimanjaro hamkuwatendea haki, mmewabagua, hamkuwapa fidia na hatuoni kwa nini wakati wao ni Watanzania tena wakulima wazuri wanaozalisha Kahawa inayotupatia fedha za kigeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninazo nyaraka za Wizara zinazoonesha walivyoshughulikia huu mdororo wa uchumi. Kwa upande wa Chama Kikuu cha Ushirika cha *KNCU* tulipata hasara kubwa sana wakati wa kuzalisha hilo zao la kahawa na kuuuza mwaka 2008/2009. Hasara tuliyopata ni kama shilingi bilioni 130.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tukategemea Serikali yetu itatufidia kwa sababu sasa hivi *CRDB* imetukaba koo inataka kufilisi wale wakulima wa kahawa wa KNCU, wanataka kukamata mali zao na hamna namna ya kupata hizo fedha zinazodaiwa na *CRDB* kama hatutapata fidia. Hii ina maana wakulima wa kahawa watakatwa, *the little money that they have* sasa hivi, ni fedha zile ndogo kulipia madeni ya huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliambiwa tuandike barua na mwaka 2009 *KNCU* ikaandika barua kwa Waziri wa Fedha, Gavana wa Benki Kuu anayo nakala na sisi tukasema kutokana na huo mdororo wa uchumi tumeumia, tumefilisika na Serikali ika-*respond positively*. Hapa ninayo barua ya tarehe 16 Septemba, 2010 ya Ramadhani Kija, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi yuko pale ananiangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, anamwandikia Meneja Mkuu wa *KNCU* anasema: “Malipo ya fidia ya hasara iliyotokana

na mdodoro wa uchumi duniani. Tafadhali rejea barua yako ya tarehe 22 Juni, 2010 yenye kumb. Na. *KNCU/GF/MFC/Vol*.3/06/279 kuhusiana na kupatiwa fidia ya hasara iliyotokana na mdororo wa uchumi wa dunia kupitia mpango wa kunusuru uchumi.

Ombi la *KNCU* 1994 *Limited* limepitiwa upya na kubainika kuwa inastahili kulipwa fidia ya hasara iliyotokana na madhara ya msukosuko wa uchumi. Kwa hiyo, tunawatumieni sh. 255,105,570.17, kwa hiyo, kiasi hicho kimeidhinishwa kwa ajili ya hasara hiyo. Hivyo unatakiwa kuwasiliana na benki yenu kwa ajili ya taratibu za kupunguza deni lenu katika benki ya *CRDB* kwa kiasi kilichotajwa hapa". Ametia saini, Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasikitika sana watu wa Kilimanjaro. Tangu hiyo tarehe 14 Septemba, 2010 hizo fedha hazijaja. *KNCU* hawajapata hizi fedha ingawa hii ni *advanced.* Shilingi milioni 255, siyo hizo, sisi tulikuwa tunadai shilingi 1,000,030,000/= Wanasema wamefanya mahesabu. Wamefanya na nani wakaona kwamba tunatakiwa kupewa hizi milioni 255?

Nyie watu wa Hazina mmefanya mahesabu na nani? Sisi tulioko kwenye kazi tumewaletea kwamba tunadai fidia ya sh. 1,000,030,000/=, sasa nyie mnakwenda kusema milioni 255, *okay* ni *advanced* tukajua kwamba kama mmeanza na hizo, hizo nyingine zilizobaki tutapata. Lakini nasikitika sana Wizara ya Fedha mnavyotenda kazi zenu. Zile fedha mpaka leo hatujapata na katika lile deni zilikuwa zimebaki shilingi milioni 800, aah, ngoja niangalie vizuri.

*(Hapa Msemaji alirejea nyaraka alizokuwa nazo ili kujiridhisha kuhusiana na kiwango cha fedha alichotaka kukitamka)*

**MHE. AGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, lilikuwa limebaki deni la sh. 858, 877,997.30/=, kwa hiyo, kwanza zile milioni 255 hamkulipa, pili zile zilizobaki milioni 858 mpaka leo riba imeendeela ku- *accumulate,* sasa *KNCU* inadaiwa shilingi bilioni 1.3. Sasa naomba kama hamtatu- *bailout*, hamtatusaidia hizi fedha, ina maana *KNCU* imefilisika na wale wakulima wamefilisika.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa kwa Waziri Mkuu nikamdokeza hatari ya kutowapa wakulima wa kahawa hizi fedha. Msipowapa mwaka 2015 mtaendaje kuomba kura kule? Mtasema wale wananchi ni wabaya, lakini ubaya unatokana na ninyi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuwaambia, siyo vitisho, lakini unaona Rombo imekuja kwetu Upinzani, Vunjo Upinzani, Hai Upinzani, mmebakiwa na Majimbo ya Siha na Moshi Vijijini. Sasa kwa mtaji huu kama hamuwapi hizi fedha mnategemea kwamba Majimbo yale mtayapata tena jamani? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilimwambia Waziri Mkuu aokoe chama chake kwa kuwalipa wale wananchi wa Moshi kile wanachostahili. Kwa hiyo, nimeona niliseme hili mbele ya Waziri wa Fedha na Manaibu wake na kwa kuwa Katibu Mkuu yupo hapa na Gavana wa Benki Kuu na barua zenyewe ndiyo hizi, hebu watafute fedha mahali popote na wawasaidie wale wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kule, *The Tanzania Coffee Research Institute (TaCRI)* inafanya kazi nzuri sana ya kuboresha ile kahawa na wananchi wanahangaika. Tumepata kahawa ambayo baada ya miaka mitatu inazaa na hakuna wadudu wale wanaotuhangaisha. Sasa tupeni uwezo, sisi hatuombi cha ziada, tunaomba basi kama Serikali mliamua kuwafidia wakulima wa pamba, wafidieni na wakulima wa kahawa. Tumekuwa tunafuatilia, tukakuta kwamba kumbe wale matajiri wenye fedha wamepata fidia, lakini wakulima maskini hawajapata.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. AGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha unisaidie kusimamia hili. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mrema. Mheshimiwa Seleman M. Nchambi atafuatiwa na Mheshimiwa Zungu.

**MHE. SELEMAN M.N. SELEMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa kuna utaratibu mzuri wa Serikali kuendelea kuona ni namna gani tunaongeza vyanzo vya mapato. Hili ni jambo zuri sana kwani tukiongeza mapato mengi, wananchi wanapata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sikio huwa kuna hereni. Kazi ya hereni katika sikio huwa ni kulifanya sikio

lionekane vizuri tu, lakini hereni hiyo haiwezi kulifanya sikio lisikie zaidi. Hereni Inaweka urembo tu kwenye sikio na kukufanya mtu uonekane kuwa mrembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Kishapu zimepotea shilingi bilioni 6.5, fedha hizi ni zile ambazo Serikali inaendelea kukusanya kwa jitihada na kupeleka huko. Lakini fedha zinapelekwa zinaliwa. Sasa naomba niseme yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama shilingi bilioni 6.5 za walipa kodi zimepotea, huku Watanzania Wanakishapu maskini wanahitaji huduma mbalimbali za maendeleo, huduma za kiafya, maji na mambo mengine, lakini fedha hizi zilizopotea siyo sawa na ndege wanaporuka angani wanapotea. Fedha ina hesabu zake. Mimi nashindwa kuelewa kwa nini fedha hizi zimepotea!

Mheshimiwa Naibu Spika, wako waliopoteza fedha hizo ambao ni Watanzania 14 na kati ya hao ni wanne peke yao ndiyo waliofikishwa Mahakamani, wengine kumi (10) hawajulikani waliko. Hata waliopelekwa Mahakamani hakuna hata Mkurugenzi mmoja ambaye ndiye *Chief Accountant* wa Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wananchi wa Kishapu wako 340,281 waliofikishwa Mahakamani wako wanne (4) kwa hesabu hiyo kila mmoja amekula fedha ya Watanzania 85,000 Bunge lako hili linachukua wananchi takribani 600 peke yake. Katika Watanzania 85,000 walioibiwa fedha zao na mtu mmoja, unahitaji Mabunge kama haya zaidi ya 100 ili waenee.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinakusanywa, zinapelekwa, zinaliwa. Mimi hapa nikiivua kofia yangu hii nikaiweka chini utanitaka nitoke nje kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, lakini aliyekula shilingi bilioni 6.5 mpaka sasa hivi anatamba, anatembea nje, Watanzania maskini wanaendelea kufa kwa maradhi, watoto wetu wanaendelea kukaa chini, wakulima wetu wanaendelea kulima kwa jembe la mkono, yule aliyekula fedha hana tatizo. Kofia yangu nikiitoa Kanuni za Bunge zinasema toka nje, sheria pale pale inachukua mkondo wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wako watu wamefungwa zaidi ya mwaka mmoja kwa kuiba kuku mwenye thamani ya shilingi 800, lakini aliyekula shilingi bilioni 6.5 mpaka leo hafuatiliwi. Sasa naomba maelezo ya kina, Waziri anatushawishi sisi tuendelee kuibana Serikali ikusanye fedha. Je, ikusanye fedha ziende zikaliwe ama zikatekeleze miradi kwa ajili ya Watanzania walio wengi?

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi mojawapo iliyosaidia sana fedha hizi zitafunwe ni Benki ya *NMB*. Fedha zimetolewa nje ya utaratibu. Fedha ya Serikali inatolewa *cash*, kama mimi akaunti yangu ya mshahara wa Bunge ninavyokwenda kuchukua!

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kushanga hata *statements fake* zipo zilizotoka *NMB*. Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* anazo. Ushahidi upo, kwa nini Benki ya *NMB* haijashitakiwa, irudishe fedha ya wananchi wa Kishapu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Benki ya *NMB* imeshiriki kwa asilimia mia moja kupoteza fedha za wananchi wa Kishapu.

Kwa nini haijashitakiwa, anakwenda kushtakiwa mtumishi mmoja? Benki ile ina *policy* gani na watumishi wale? Ina maana Watanzania wanaoweka fedha zao *NMB* ipo siku watadondosha machozi kama sisi Kishapu leo tunavyolia? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa angalizo na nakuomba tafadhali Serikali hii iko kwa ajili ya wananchi kwani hakuna Serikali duniani inaweza ikawepo bila ya kuwepo wananchi. Lakini upo uwezekano wa wananchi kuwepo na wasiwe na Serikali. Sasa kuhusiana na *NMB* naomba, tumesema sana kwenye Baraza la Madiwani, lazima washtakiwe warudishe fedha za wananchi wa Kishapu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakurugenzi ambao ndiyo walikuwa wasimamizi wa fedha hakuna hata mmoja aliyekamatwa. Leo hii mwingine ameletwa mkoani pale, amesogezwa pale, bado upelelezi unaendelea huku milioni 754 hazijulikani zilikokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shilingi bilioni 1.6 zimehamishwa hamishwa kwenye akaunti. Hii fedha ni ya Serikali, ni ya wananchi, wamegawana, mtu amefanya *transaction* kupitia benki ya CRDB shilingi milioni 300 anapelekea mkewe, mtumishi wa Halmashauri, bado tunahitaji ushahidi wa aina gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wameshindwa kufanya ile kazi tunaomba sisi wananchi tufanye kazi. Kama yupo mwananchi wa Kishapu hata mmoja na mimi Nchambi nikiwemo, aliyekula fedha zile na akatajwa,

niambieni mimi nikawashawishi wananchi tumkamate tumlete hapa ndani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliotajwa hawakamatwi, kesi iko Mahakamani inasua sua. Serikali ndiyo imetoa hii fedha, waliokula ni watumishi wa Serikali, kwa nini leo wanaadhibiwa wananchi wangu wa Jimbo la Kishapu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba fedha ije kwa sababu Serikali ndiyo ilitoa fedha, waliokula ni watumishi wa Serikali hakuna mwananchi hata mmoja aliyekula fedha ile. Rudisherni shilingi bilioni 6.5 ikatekeleze miradi iliyokusudiwa kwa wananchi wa Kishapu. Kuwafikisha Mahakamani watuhumiwa hakusaidii akinamama watibiwe vizuri, hakusaidii wananchi wa Kishapu wanywe maji safi na salama. Yale ni mambo yenu, naomba mrudishe shilingi bilioni 6.5. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo lingine ambalo lazima Waziri wa Fedha alifahamu. Pale tuna mtu anaitwa *Internal Auditor*, *functionally* anaripoti kwa Wakuu wa Idara, *administratively* anaripoti kwa Mkurugenzi wa Wilaya. Sasa huyu mbweha (Kabweha) mdogo anakwenda kuripoti kwa fisi, hiyo kesi itakuwaje? Tafadhali huo utaratibu ubadilishwe kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano mmoja, watu wanapojenga nyumba huwa wanaweka *grill*, ukuta, *fence* za umeme na mbwa. Hii yote ni kwa sababu ya ulinzi wa mali yao. Nyumba ni ya kwake, kitanda ni cha kwake, vilivyomo ndani ni vya kwake, lakini anaimarisha ulinzi.

Serikali hii mbona imeshindwa kuimarisha ulinzi wa fedha za wananchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kishapu wanalia, ni maskini, wanapata tabu, hawana huduma za afya, hawana maji safi na salama, fedha tulizoomba zimekwenda zimeliwa. Tunaomba zingine ziende zikaliwe katika utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana ndugu yangu Mheshimiwa Mgimwa, ameanza vizuri, tumeona makali yake na Manaibu hawa akinamama, lakini ninachosema fedha ya kishapu isipokuja shilingi bilioni 6.5 nitafanya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mimi ninayewakilisha wananchi 340,281 nitaonekana sifanyi kazi, nitakwenda Kishapu nitawahamasisha wananchi wote 340,000 mwenye maparage aweke mgongoni, mwenye maji, waje wapange foleni hapa, Mheshimiwa Naibu Spika uanze kuwasikiliza mmoja baada ya mwingine pengine unaweza ukatatua kero zao kwa sababu mimi ninayesema kwa ujumla kama mwakilishi wao pengine sisikilizwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana wakati Waziri na Wasaidizi wake wanajibu haya mambo kwa kushirikiana na Mawaziri mbalimbali kama vile wa TAMISEMI na Mambo ya Ndani ya Nchi na kila anayehusika, niwaeleze kwamba fedha ya Kishapu imeliwa, Benki ya *NMB* imeshiriki, lazima watoe fedha na waliokula washtakiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Nchambi. Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee, CHADEMA hajaongea hata mmoja. Mheshimiwa Zungu!

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru. Kwanza na-*declare interest,* mimi ni Mjumbe wa *PPRA*, lakini sijawahi kuona taarifa ya *PPRA* inajadiliwa ndani ya Bunge hili. Chombo hiki ni muhimu sana kama ripoti ya *CAG*. Ni chombo ambacho kinachunguza mambo mengi na kinagundua mambo mengi sana. Lakini ripoti ya *PPRA* kwa mujibu wa sheria inatakiwa ijadiliwe humu ndani, lakini huwa haijadiliwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupunguza matumizi tumewahi kusema na tunaendelea kusema, inakuwaje viongozi wa Serikali ambao wamekopeshwa fedha za kununua magari mpaka leo wanatumia magari ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kuwanyang'anya haya magari ili iepuke matumizi na gharama za ku-*service* magari haya, kulipia mafuta, magari haya ambayo yanatupia fedha nyingi sana wakati viongozi wote wamekopeshwa magari. Nataka kujua hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mahoteli yanauzwa na kwenye Bunge hili tukajibiwa *capital gain tax* hazitozwi kwa sababu hoteli hizi haziuzwi badala yake wanabadilisha Menejimenti kitu ambacho sio kweli. Hoteli ya *Movenpick* imeuzwa na hata ukienda kwenye mitandao Mheshimiwa Waziri wewe na Manaibu wako au watendaji wako

mkienda kwenye mtandao *Movenpick* pamoja na *Four Season* za Indonesia zimeuzwa na mwenye mali mmoja hatukupata *capital gain tax* hata moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu na Serikali inakuja ndani inatetea vile vile kusema imebadilisha Menejimenti. Hii ni mbaya sana ndiyo maana tunakosa mpaka fedha za kuwalipa Walimu sababu sisi wenyewe tulijifanyia mambo ya kutetea mambo ya kutokukusanya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumzia suala la rada. Hii rada utakumbuka mimi na wewe na Mzee Cheyo na Mheshimiwa Kairuki tuliambiwa fedha za rada zimewekwa kwenye akaunti maalum Uingereza na ina *attract interest*. Mpaka leo naambiwa *figure* iliyokuja Tanzania ni ile ile tu ambayo ndiyo ya rada, *interest* ya rada wala haizungumziwi. Sasa namwomba Waziri inawezekana labda na wao hawana taarifa walifuatilie ili ile *interest* nayo vile vile iweze kurudi isaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye ripoti ya Waziri, kusimamia udhibiti wa viza kwenye Balozi zetu. Mimi nimerudi hivi karibuni kutoka Japan mashine ya viza ambayo inatakiwa iende Melbourne, Australia mpaka leo ipo kwenye Ubalozi wa Japan Tanzania zaidi ya miezi minane mpaka mwaka, hawana njia ya kuipeleka na hii ni kazi ya Hazina na Mabalozi hao ambao wanatoa viza bila ya kutumia *sticker* ndio wanaoibia Hazina fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Ubalozi Holland kwa takwimu za watu wa *Immigration* wanatoa viza zaidi ya shilingi 50,000 kwa mwaka kwa gharama ya viza moja dola 50 tu ni shilingi *million 2.5 US Dollars*. Tunataka Waziri afanye

*audit* katika Balozi. Afanye *audit* kwenye Balozi zote ambazo zinatoa viza bila ya kutumia *sticker* ili tujue Serikali inapoteza mapato shilingi ngapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hatari kubwa sana na hii sio mwaka mmoja, hii ni zaidi ya miaka saba viza zinatolewa kwa kupiga mihuri na hakuna takwimu sahihi. Hivi tunalalamikia fedha wakati fedha tumezikalia wenyewe, halafu tunalalamika hatuna fedha za kulipa ada.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi kwenye Wizara ya Nishati nimezungumzia kuhusu *capital gain tax.* Tuige wenzetu wa Uganda wanavyofanya, namna wanavyopata mapato kwenye kuuza, watu wanavyouziana *shares* wanavyouziana mali na Serikali inapata fedha na mifano ipo niliitoa hapa. Nasema hawa waliouziana mali iwekwe sheria with *retrospective.* Tudai madeni yote ya miaka sita iliyopita, ili Makampuni hayo yalipe kodi ambayo Serikali inayostahili kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko habari za Msajili wa Hazina anataka kuzi-*dispose share* za *UDA*. Sisi hatukatazi *shares* kuwa *disposed*. Tunachokisema taratibu za kisheria na uwazi uwepo. Watu wasiuziane *shares* hizi kwa mlango wa pembeni na Serikali ikajikuta inakosa mapato makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mipango mingi sana ambayo tulizungumzia Makampuni ya Simu yanavyokuwa hayalipi kodi. Chukua mfano mdogo tu wateja wa simu nchini mwetu zaidi ya milioni 26 kila mmoja wao angeweza kulipa shilingi 200 kwa siku na Serikali ikajipatia zaidi ya trilioni 1.8, lakini haya mambo bado hayajashughulikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumza kwenye Wizara ya Nishati na Madini (*Pan African Energy)* toka tumezungumza hatujapewa majibu kama Serikali imeshaanza kuzidai fedha ambazo tunaidai *Pan African Energy*. Ukitazama kwenye taarifa mbalimbali za kiuchumi, *Pan African Energy* wanasema hawalipi na hakuna mtu yoyote wa kuwasumbua kulipa fedha hizi. Shilingi bilioni 52 ni fedha nyingi sana na wanasema wao hawalipi kwa sababu wamewekeza shilingi bilioni 256 nani ame-*audit* fedha hizi kama kweli ziliwekezwa katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumza hapa na narudia tena kwa sababu ndio maeneo ya fedha. Miundombinu ya gesi isishikwe kabisa na Makampuni ya nje. Miundombinu ya gesi imilikiwe na Serikali na wananchi na njia rahisi ya kupenyeza uchumi huu ni kuwamilikisha wananchi waweze kununua *shares* katika mradi huu wa gesi ili wanufaike na wao waweze kumiliki mali ya nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukapata wawekezaji, Serikali inaweza ikachangia lakini kiwango kikubwa cha kumiliki bomba hili linapelekwa kwa wananchi wa kawaida na wao wana uwezo mkubwa sana. Sioni sababu kwa nini suala kama hili haliwezi kushughulikiwa na hizi fedha za *Pan African Energy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo kabisa taarifa za kwenye mitandao, *TPDC* wanasema suala hili tuliache pembeni halina sababu ya kuzungumziwa sasa hivi na jina la mtu lipo vile vile limetoka, limetoka kwenye ripoti ya *Revenue*…. Limezungumzwa hapa juzi kwenye Wizara ya Nishati, tunataka kujua *action* gani sasa hivi Serikali

imeshachukua kudai hii fedha ambazo zinafahamika ni za nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni Mabenki. Kuna nchi nyingi sana duniani zimeziwekea masharti Mabenki ambayo yanavuna fedha katika nchi husika kama hapa. Mabenki haya yote yanatumia fedha za Tanzania kutajirika, kwa nini hakuna sheria ya kuzifanya Benki katika faida zao walizopata asilimia tano, nne au sita zikatengwa makusudi kwa kukopesha wakulima na wavuvi.

**MBUNGE FULANI:** Sema.

**MHE. MUSSA Z. AZZAN:** Hatu-*capitalized* kwenye vitu kama hivi, haya Mabenki yanatengeneza fedha na faida zao zote zinakwenda kujenga nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwanza, nataka Wizara kupitia Waziri watupe majibu kutokana na barua ya Umoja wa Wastaafu wa Serikali Kuu wa Morogoro ambao inasemekana nakala wameleta Wizarani na Waziri unalijua kuhusiana na madai yao ya malimbikizo ya fedha zao za pensheni ambazo Mfuko Mkuu wa Hazina ndio unawajibika kuwalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupatia hii nyaraka kwa ajili ya kuokoa muda ili utupe mustakabali wa malimbikizo ambayo wanadai kutokana na waraka na kuna nyaraka mbili ambazo Serikali ilizitoa zilizoonesha kwamba kulikuwa kuna nyongeza ya pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili nataka nipate taarifa tu kutoka Serikalini kuhusiana na mustakabali wa fedha za *DECI* kwa sababu kwa kweli hili suala linaumiza wapiga kura wengi nchi nzima na kesi imechukua muda mrefu sana. Tunajua mara nyingi kesi zinachukua muda mrefu kwa sababu ya uzembe wa Serikali. Sasa nataka nijue *status* ya *DECI*, fedha za umma na kama zile riba ambazo zinapatikana kutokana na fedha hizi zilipowekwa zitanufaisha wenye fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la tatu kuhusiana na suala la *PRIDE*. Nilivyoingia Bungeni miaka miwili na nusu ya mwisho moja kati ya Mashirika katika ile orodha ambayo tulipewa ya Mashirika ya Umma ilikuwepo Shirika la *PRIDE*. Nashukuru Mwenyekiti wangu wa Kamati *POAC* yuko hapa, lakini hiyo ilikuwa mwaka 2008 tulivyopangwa kwenye Kamati kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ghafla mwaka 2009, Shirika la *PRIDE* likawa limejigeuza limekuwa Kampuni ya mtu binafsi. Leo ukizungumza *PRIDE* inajulikana ni Kampuni ya mtu fulani. Sasa tulitaka tu Bunge letu Tukufu liweze kujua huu mustakabali wa hii *PRIDE* na ilikuwaje kuwaje ikatoka kuwa Shirika la Umma kwenda kuwa Kampuni binafsi, kwa sababu kuna majina ya vigogo wengi yanasemwa yamehusika huku.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ili kuondoa huu mgogoro usiokuwa na tija tungependa kujua *PRIDE* na mustakabali wake na Mheshimiwa Waziri kwa kuwa tunaamini utendaji kazi wako, tunaamini uaminifu wako, tunajua kabisa hakuna makandokando yoyote ambayo utayaficha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine nikubaliane kabisa na hoja ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na kesi na gharama za kesi. Shirika letu la *TANESCO* linaonekana ni mfu kwa kipindi kirefu sana, lakini ukiangalia moja ya fedha ambazo zinatumika kwa mabilioni ni kwa ajili ya kesi ya *IPTL* ambayo nadhani Kampuni ya *Mkono Advocates* imepewa hii kazi kwa ajili ya shughuli ya *arbitration*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma *Commercial Law,* nadhani *arbitration* ni kumaliza suala kwa muda mfupi na kwa gharama nafuu. Sasa *Mkono Advocates* kwa mwaka mmoja shilingi bilioni nne, sasa bilioni nne kwa mwaka mmoja kwa ushauri wa kisheria tena *arbitration* hii nchi tunakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka pia tupate msimamo wa Serikali kuhusiana na mabilioni haya ya shilingi ambayo yanatumika kwa masuala ya kisheria, wakati tuna vijana wetu wasomi, tuna Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalam, Wakili lukuki kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa hiyo, nataka nipate maelezo ya kina kuhusiana na hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine ni hili suala la tasnia ndogo ya fedha. Imezungumzwa kwa kina na Kambi ya Upinzani. Tulikuwa tunaiomba Serikali kama ambavyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo mnaitekeleza mnasema dhamira yenu ni kuwasaidia wanyonge. Mwangalie kwa namna gani mtaunda *Regulatory Authority,* Mamlaka ya Udhibiti ya hizi tasnia ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sote tunajua kwamba, kukopa Benki kwa mwananchi wa kawaida, ni tatizo kwa sababu Benki zetu zina masharti makubwa sana na imefikia kipindi sasa hivi wananchi wenyewe wanaopata nafasi ya kukopa Benki wamezilalamikia, baadhi ya Benki kwa kuzitaja majina kwamba lazima umpe asilimia kumi yule Afisa Mikopo ndiyo uweze kupata mkopo Benki. Lakini kutokana na ugumu huu wananchi wengi maskini wanategemea hii tasnia ndogo ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii haina kitu ambacho kinaidhibiti, mtu anaamka, anatunga jina lake, ataliita Halima Mdee, ataita Fincha, ataita sijui *Platinum,* anakwenda anakopa mkopo Benki, anakuja anaanzisha kijikundi chake kidogo anakopesha watu wadogo wadogo. Sasa *interest rates* inatisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake Walimu wetu, Manesi wanageuka ombaomba kwa sababu wanakopa shilingi milioni mbili, wanalipa shilingi milioni saba, anakopa sh. 500,000, analipa shilingi milioni tatu. Kuna Walimu wamenipa ushuhuda, kwa hiyo tulikuwa tunaomba Serikali hii *Regulatory Authority* ni muhimu sana kama tunataka kumsaidia Mtanzania wa chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine ni suala la mishahara hewa. Nashukuru Mheshimiwa Waziri amefanya utafiti mwenyewe, kama tumeweza kupoteza shilingi bilioni 70 kwa mwaka mmoja, tuliuliza miaka mitano ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi tumepoteza shilingi ngapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu Mkaguzi Mkuu wa Serikali amekuwa akilizungumzia hili suala kila mwaka na Serikali mkaamua mjaribu kwa mwezi mmoja. Lakini niwaambie kuna taasisi zingine ambazo mkazitupia macho kwa mfano, Chuo Kikuu cha *UDOM*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu cha UDOM kinalalamikiwa kina tatizo kubwa la mishahara hewa, kinalalamikiwa tokea mwaka 2007 ambapo kilianza, mpaka sasa kuna wafanyakazi zaidi ya 200 wameacha kazi lakini mishahara bado inaendelea kupelekwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Maprofesa na Madaktari na majina yao yapo wamekufa lakini mishahara inaendelea kupelekwa pale. Kuna wafanyakazi wako pale wana *check number* mbili, mimi naitwa Halima Mdee, wakasema Halima James Mdee mkwanja unaingia. Uongozi wa *UDOM* unajua, baada ya Serikali kutangaza kwamba inakwenda kukagua mwezi Januari wakaandika barua kuwaambia eti wana fedha za ziada watumie vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani Mheshimiwa Waziri tunajua utaratibu gani wa Serikali kama unapelekewa fedha matumizi yanazidi. Wametumiwa fedha kwa miaka yote wameona Serikali ina nia ya kwenda kukagua wakaandika barua ili kujilinda. Sina nia mbaya na mtu lakini ukweli lazima usemwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu alikwenda pale akaambiwa kwa namna gani wafanyakazi 400 ambao hawako kwenye *payroll* walikuwa wanalipwa kwa sababu kulikuwa kuna fedha zinazagaazagaa. *CAG* alifanya

ukaguzi maalum baada ya lile sakata la migomo la wafanyakazi na wanafunzi, wakagundua madudu mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti ya *CAG* Waziri Mkuu anaijua, imekwenda kwa Waziri Mkuu imeonekana, imepelekwa kwa Rais mambo yamechakichia. Sasa kama kweli umeingia una dhamira safi kabla hawajakuharibu wale wachafuchafu, kwa sababu wengi wanaingia wasafi, wakikaakaa kidogo wakionja neema na wao wanabadilika na inawezekana wewe umeletwa na Mungu pamoja na wasaidizi wako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaomba hizi taasisi tuzitupie jicho. Kuna kero kubwa sana *UDOM*. Watasema mengi, watayahadaa kwa mengi, lakini tunataka Bunge lako Tukufu lipate taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuhusiana na *UDOM*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Wizara ya Fedha ni Wizara muhimu sana kwa nchi zote duniani. Hawa ndio wanasimamia uchumi wa nchi na ndio wanasimamia maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia kwenye maeneo machache: La kwanza, mfumuko wa bei umefika asilimia 17.2. Lakini wakati tuliambiwa Julai ingekuwa imefika *single digit* mpaka leo hatujafika *single digit,* majibu bei ya mafuta duniani, njaa, chakula. Lakini Rwanda wananunua mafuta kwenye soko hilo hilo ambalo na sisi tunanunua, Kenya wananunua kwenye soko hilo hilo

ambalo na sisi tunanunua, lakini wao *inflation* yao inashuka kwa kasi, kwa nini ya kwetu haishuki, maana yake *Monetary policy* ya kwetu tuiangalie. Naomba Waziri wa Fedha aiangalie *Monetary Policy* yetu, naamini liko tatizo, tuliangalie upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni matumizi ya Serikali. Tusipohangaika kwenye matumizi ya Serikali, tusipohangaika kuwekeza kwenye kilimo hicho na chakula kingi hatuwezi kuhangaika na suala la *inflation* na *inflation* ndiyo maisha ya watu wa kawaida. Kwa hiyo, lazima tuhangaike na suala la mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu. Kila mwaka tunaongeza kodi kwenye maji, bia, soda na sigara. Miaka yote hii huu ni mwaka wangu wa saba niko Bungeni, ulikuwa ukiuliza Waziri yoyote wa Fedha aliyekuwepo, jibu lilikuwa tuna-*adjust* kulingana na *inflation* iliyopo. Hilo ndilo limekuwa jibu na kwa kweli hakuna wakati tunapandisha *excise duty* zaidi ya asilimia 10. Tulikuwa tuna-*adjust* kulingana na *inflation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Waziri wa Fedha amekuja hakuna kigezo, bia ameongeza asilimia 25, maji asilimia 20, soda asilimia 20, sigara asilimia 20, yeye kigezo chake kipi mwenzetu. Wenzake wote waliopita kigezo chao kilikuwa ni *inflation rate* wana-*adjust*. Lakini tukiongeza bidhaa hizi maana yake *production* itapungua, watu hawa hawatawekeza, kwa hiyo kodi tunaweza tukaipata au tusiipate.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu atuambie leo tunaongeza kodi

kwenye maji ya kunywa wakati tukijua katika vijiji vyote bado tuna maeneo ambayo hatuna maji safi na salama. Maji pekee yaliyokuwa yanawasaidia Watanzania ni maji ya chupa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunakuja kwenye Bunge hili tunaongeza bei ya maji ili tupate kodi, kodi hii tutapata, lakini tutaipeleka kwenye kutibu watu wanaoharisha kwa sababu ya kunywa maji machafu, ina maana wangepata maji mazuri tungepunguza magonjwa, lakini leo tunapandisha kodi kwenye jambo hili!

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni suala la Dar es Salaam *Stock Exchange,* soko hili linasuasua, lakini linasuasua kwa sababu ya maamuzi ya Serikali. Ningeomba Mheshimiwa Waziri, hivi tunasubiri nini kufungua *capital account,* kwa nini ina kuwa *much rebelized,* kwa nini hatuifungui yote ili watu wenye fedha kuwekeza waende wawekeze, *Pension Funds* waende wawekeze nje na wengine wawekeze ndani, kwa kufanya hivi soko hili litakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili tunasema kwenye *I.P.O* watu wa nje wasije lakini kwenye *secondary market* tusiweke *limitation* yeyote, mwenye mtaji aje awekeze kwa sababu zile *shares* tulizonazo zitapata *value* na soko litachangamka na ndiyo biashara ya soko la hisa itaongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kwenye Soko la Hisa, naomba *C.H.C* ambayo inafanya *privatisation,* wasifanye chochote, wapitie kwenye Soko la Hisa ili watu wengi waende kwenye biashara na jambo hili litakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mishahara ya wafanyakazi nchi hii, wafanyakazi wanalipa pesa nyingi sana, ukienda kwenye jedwali la wafanyakazi nchi hii *Pay As You Earn* wafanyakazi wa nchi hii wanalipa pesa nyingi sana. Wanalipa *direct tax,* wanalipa *indirect tax*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna *contradiction;* wafanyakazi wa nchi hii mnawatoza kodi kubwa sana, lakini pia wafanyakazi wa nchi hii wanapanga nyumba hamuulizi bei zake wanalipa shilingi ngapi, masoko yao hamuulizi wanalipa shilingi ngapi, kila kitu chao hamfuatilii, hiki ni nini? Naomba sana Waziri mwaka kesho uje uangalie upya *rate* za kuwa-*charge* mishahara kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaolipa kodi nyingi kwa nchi hii ni wafanyakazi, haiwezekani Bunge hili tukawa tunakaa kila siku wafanyakazi wanatozwa pango lao la *rent.* Ukienda Dar es Salaam chumba kimoja laki mbili, mtu huyu kodi yake ni kubwa haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wafanyakazi hewa limesemwa, ni aibu kuendelea kuwa na wafanyakazi hewa, benki ya *NMB* wakati wanakuja kuinunua masharti walisema ni *Microfinance Bank, Rable Bank* ni *Bank* inayojulikana Duniani kwa ajili ya ku-*invest* kwenye *agriculture,* nataka Waziri uniambie *NMB* imewekeza kiasi gani kwenye *Agriculture?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyokuja kununua benki hii, masharti yale ya mwanzo wangeyatekeleza tusingehitaji benki ya *agriculture,* leo lakini kwa sababu wamekuja *NMB* hawawekezi kwenye *agriculture* na

*account* yote ya Serikali tumewapa *NMB*, ukiondoa *account* ya Serikali, *bank* hii inakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo yake nenda Mikoani wafanyakazi Walimu wanashinda benki, watu wanakaa masaa manne, mpaka matano *efficiency* inatoka wapi? Karne ya 21 moja mtu unakaa benki masaa matano kwa sababu gani hawa-*invest* kwenye *system, account* mmewapa wao peke yao sasa mme-*rebelize* mabenki mengine ya nini? Kwa nini msiwashindanishe na wengine? Lakini mnawashindanisha kwa kuweka masharti ambayo atabaki *NMB* peke yake. Nasema uwe na benki kila Wilaya maana yake benki ya *NMB* haiwekezi kule

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine naomba Waziri wa Fedha uchunguze, *NMB* unaweka pesa zinatakiwa zihamishwe ndani ya dakika 15 mpaka 30 lakini wanakaa na fedha hizi mpaka wiki mbili mpaka tatu. Tukifanya *audit* ndani ya benki hii yale yaliyotokea *Backlays* Uingereza tutayakuta katika benki hii. Tutakuta watu wanachukua pesa wanakopesha mabenki mengine kwa siku tatu mpaka nne ndiyo wanawapelekea wafanyakazi wetu, hili haliwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kama muda wangu utaniruhusu...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Serukamba, kwa dakika tano utapigiwa kengele moja tu. Mheshimiwa Likokola!

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Waziri kwa ajili ya kuhakikisha kuwa analeta Sheria mbalimbali lakini ninaomba ushahuri kuwa katika Sheria atakazoleta katika kipindi cha mwaka ujao wa fedha lazima ahakikishe Sheria ya bajeti inaingia katika Bunge letu Tukufu. Tumekuwa na matatizo makubwa sana na bajeti yetu mfumo mzima haueleweki vizuri. Kwa hiyo, tunaomba Sheria ya bajeti iweze kufika katika Bunge Tukufu ili tuweze kuwa na bajeti ya uhakika na tuweze kuifuatilia vizuri bajeti yetu, naomba nichangie pia katika eneo la *Community Banks*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu tuna Halmashauri karibu 138 na zaidi lakini tuna *Community Banks* nane tu na Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa c*ommitment* yake kuwa atahakikisha Serikali inatoa mchango katika kuanzisha *Community Banks*. Leo tunaona kuwa wananchi wameanza kunung'unika mabenki yameanza kutoa huduma ambazo haziko sawa. Kwa hiyo, tungependa kila Halmashauri iweze kuwa na *Community Bank* hizi zinaweza kusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Halmashauri ambazo zina *community bank* na zinafanya sana mfano, Halmashauri ya Mbinga tuna *Community Bank* ya Mbinga ambayo inafanya kazi vizuri sana, *Community Bank* ya Njombe, *Community Bank* ya Mufindi, *Community Bank* ya Mwanga, *Community Bank* ya Meru, hizi ni Halmashauri chache ambazo zimepata ukombozi wa kweli kwa sababu

ukiwa na *Community Bank,* hisa ni za wananchi wenyewe na pia faida ni kwa wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote mtegemea cha nduguye hufa masikini, tunavyoendelea kutegemea benki za nje kuna siku tutakuja kuadhirika. Naendelea kuishauri Serikali isaidiane na *CBA* iweze kuanzisha *Community Banks* kwa sababu ni suala rahisi sana na kila Halmashauri inaweza ikawa na *Community Bank* na ikafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ina kigugumizi, nashangaa eti Serikali inatoa mwongozo kuwa hakuna ruhusa kufanya biashara na *Community Banks*, biashara yote ya Serikali ifanyike na mabenki mengine kwa nini na hizi ni benki zetu? Ni lazima iziwezeshe hizi benki zetu na Serikali ifanye kazi na *Community Banks* kwanza ni jambo la kujivunia kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Sheria zingine ambazo siyo za haki, *Community Banks* zinakuwa *regulated* sawa na *Commercial Banks, why?* Hizi ni *Community Banks* kwa hiyo, ziwe na Sheria ambazo zitasaidia ukuaji wake. Kama tukizigandamiza hizi *Community Banks* hazitakuwa nchi zote duniani zinaendelea kupitia C*ommunity Banks.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ametembea dunia nzima amekwenda Japan ambayo imeendelea kwa *Community Banks*, amekwenda Marekani imeendelea kwa *Community Banks* na hapa Tanzania tunategemea sana *NMB, NMB* imeungana na *Rable Bank, Rable Bank is a Community Bank* ya Netherland.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini sisi tunashindwa kuziimarisha *Community Banks* zetu. Namshukuru Waziri amesema kuwa ataleta *Microfinance Act*. Katika hilo nampongeza na kwa niaba ya wana *VICOBA* tunakushukuru sana na tunataka hiyo Sheria itoe mwongozo kamili kwa wana *VICOBA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza sana kwa hilo, lakini *microfinance* ziko nyingi na zinahitaji mafunzo, zinahitaji uendelezaji, litengwe fungu kubwa la kuendeleza sekta ndogo ndogo za fedha. Tunataka hizi sekta kwa sababu ndiyo zinazomgusa mwananchi wa chini, haya mabenki wananchi wa ngazi ya chini hayawafikii, lakini tukiendeleza sekta ya *microfinance* nina hakika wananchi wengi watafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kazi nzuri sana wanayoifanya *TAFI, TAFI* ni *association ya microfinance* imefanya kazi nzuri na naomba Serikali ishirikiane na *TAFI* ili Sheria itakayokuja hapa iwe nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii inafanya kazi na Kitengo cha Kuondoa Umaskini, naomba kipewe bajeti ya kutosha lakini pia kiboreshwe kwa sababu tatizo kubwa la Tanzania, watu wengi ni maskini tunataka watu wengi wawe na kipato cha hali ya kati. Kwa hiyo, kama kitengo cha kuondoa umasikini kikiboreshwa na kikapewa fedha za kutosha hali nzuri itapatikanika Tanzania.

Mheshimiwa Waziri ame-*quote Millenium Goals,* ame-*quote* MKUKUTA, lakini ukisema *millenium goal* namba *one* ni kuondoa umaskini kwani lazima zitengwe fedha za kutosha ili umaskini uweze kuondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge huyu ni Mheshimiwa Devotha Likokola Rais wa *VICOBA* Tanzania. Palikuwa na akinamama walikaa *Basement* asubuhi natumaini wako hapa ambao ni wawakilishi wa *VICOBA* Mikoa ya Mbeya, Njombe, Ruvuma, Dodoma, Iringa na Arusha. Pale mlipo naomba msimame, karibuni sana akinamama wa *VICOBA*. Tunawakaribisha sana hapa Bungeni Dodoma karibuni na mnaona Rais wenu kazi anayoifanya.

Baada ya hapo, naomba nimkaribishe moja kwa moja Waziri wa fedha dakika zako ni chache sana kama tulivyoongea sijui umezigawaje, una dakika 40 tu kwa ujumla wake, tunamaliza saa kumi na moja na nusu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa namna ulivyotuongoza vizuri na tumefika salama mpaka dakika hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ya pekee mlivyochangia kwa uwazi na katika njia ya kutusaidia sisi katika Wizara ya Fedha itende yale ambayo Serikali inataka na wananchi wanatarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi ninapenda kuwahakikishia kuwa Wizara ya Fedha kama mlivyoeleza wenyewe na nitaeleza baadaye, ni Wizara ambayo lazima tuangalie ukweli kuwa, kama mtu umempa akutunzie pesa

ni lazima yeye mwenyewe ajue kuwa anaaminiwa, ili ajiamini na atunze pesa. Naomba kuwahakikishia kuwa tutajitahidi na kufanya tunaloweza na msiogope kutukosoa mkiona tuna tetereka hatutarajii kufanya hivyo. Tunataka tuwe na mwelekeo ambao watu watakuwa na amani na mtunza pesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nianze kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata michango mingi kwa Waheshimiwa Wabunge na michango yao yote ni mizuri. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe kama nilivyosema na Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge kwa umakini katika majadiliano na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha katika Mwaka huu 2012/2013. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru Wajumbe wa Kamati mbalimbali za Bunge kwa michango na ushauri mliotoa wakati wa kupitia makadirio ya mapato na matumizi, Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii pamoja na maoni yenu yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wapiga kuwa wangu wa Jimbo la Kalenga kwa uvumilivu wao kwa kipindi chote nilichokuwa hapa Bungeni kwa kuwa ilikuwa ni lazima nitumikie sehemu hii. Kwa uvumilivu wao nachukua nafasi hii kuwashukuru sana, nitakuja punde baada ya kumaliza vikao vya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze kwa ufupi maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge ambayo yatasaidia sana katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha kwa mwaka huu 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ziko baadhi ya hoja ambazo ni muhimu nikazitolea maelezo kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwa umma hotuba yangu imechangiwa na jumla ya Wabunge waliopata nafasi ya kuzungumza 12 na napenda kuchukua nafasi kusoma majina yao kwa ruhusa yako:

Wa kwanza ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi Mheshimiwa Dunstan Kitandula; wa pili ni mzungumzaji kwa niaba ya Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe; Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa John Cheyo, Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa Joelson Mpina, Mheshimiwa Augustine Lyatonga Mrema, Mheshimiwa Seleman Nchambi, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Devotha Likokola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kuwa inawezekana kuwa nitakuwa nimefanya makosa katika kunukuu majina kwa jinsi walivyozungumza, lakini kama kuna Mheshimiwa Mbunge nimeruka jina lake asisite, nipate taarifa. Lakini hapo hapo majina ya waliochangia kwa maandishi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri hao tuwaruke ili muda wako uweze kutimia. Waheshimiwa Wabunge tuvumiliane tumpe muda Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA FEDHA:** Kwa maelekezo ya Mheshimiwa Naibu Spika na muda unavyotutupa mkono, naomba niende moja kwa moja katika kujibu maswali au hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue kiujumla, tumekuwa na mchango mkubwa kutoka kwenye Kamati yetu ya Fedha na Uchumi ambapo tumepata ushauri mkubwa na katika mambo ambayo tumeshauriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, ni kuwa fedha zinazotengwa na bajeti katika mchakato wa bajeti tuhakikishe kuwa zinakwenda moja kwa moja katika miradi ile tuliyopanga kwa ajili ya maendeleo. Hili tunalichukua moja kwa moja, ni ushauri ambao ni lazima tuzingatie na tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa pili ambao tumeelekezwa na Kamati ya Fedha na Uchumi ni kwamba, Serikali iweke utaratibu wa kulipa madeni ya ndani yaliyohakikiwa. Kwanza ni kweli mpaka sasa tunayo orodha ya madeni ya ndani ambayo tulikuwa tunayafanyia uhakiki ili tutengeneze *programme* ya kuanza kulipa. Ushauri huu ni mzuri na ni wa haki na uhakiki huo utakapomalizika tutaanza kuyalipa madeni haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ni la msingi ni kwamba, tuhakikishe *Executive Agencies* yaani mashirika

yale ambayo yako chini ya Wizara ya Fedha yanalipa mchango unaostahili kwa mujibu wa Sheria kwenye Mfuko Mkuu. Hili tunalifanyia kazi kwa maana ya kubadilisha Sheria yenyewe ya *TR* na Sheria hiyo itakapokuwa imebadilishwa na tutaileta mbele yenu na mtaipitisha ili iwe na nguvu ya kisheria kubadilisha Sheria za zamani. kwa kutumia Sheria hiyo mpya, tuna uhakika usimamizi utakuwa mzuri katika haya Mashirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo tumeshauliwa na Kamati ya Fedha na Uchumi ni kwamba, ni namna ya kulishughulikia suala la *Skills Development Levy* na kwamba tutazame namna ya ku- *broaden* wachangiaji wawe wengi na vile vile tupunguze kutoka 6% mpaka 4%.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tutazame namna gani akina nani watanufaika kulingana na uasili wa Sheria ya *Skills Development Levy* hilo tunakubaliana wote na tumeshaahidi kuwa tutateua Kamati ya kulifanyia kazi. Itakapofika Januari tutakuwa tumeshapata matokeo ya Kamati hii kwamba imekuja na nini ili tuwashirikishe na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, Kamati imetushauri kuwa Wizara ya Fedha ikishirikiana na Wizara zingine pamoja na wadau wengine tutazame ni namna gani ya ku-*broaden tax pays,* tusitarajie au tusitegemee vyanzo vya mapato vya kodi vya zamani, ndiyo maana mtakumbuka kuwa, Spika ameunda timu ya kutazama ni namna gani tunaweza kupata mawazo mapya ya kutazama vyanzo vipya na Waziri Mkuu vile vile nafahamu ameunda timu nyingine ya kusaidia kufikiri na kuja na mapendekezo ya

namna gani tunaweza tukatazama *opportunities* ya vyanzo vipya vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala haya tunayafanyia kazi na pindi tutakapo matokeo ya tafiti hizo au matokeo ya Kamati hizo tutayafanyia kazi na kuyaingiza katika *broad base* ya *tax source.*

Mheshimiwa Spika, tumepata mawazo mazuri sana kutoka Kambi ya Upinzani na suala lingine ambalo wamependa kulifahamu ni kwamba, wanafahamu Wizara ya Fedha inatumia karibu asilimia 28 ya mapato ya Serikali. Ni kweli kitakwimu ukipiga hesabu inakuja karibu asilimia 28, lakini utaona Wizara ya Fedha inasimamia nyenzo nyingi katika kusimamia mambo mengi ya Serikali kwa ujumla, kwa hivi ile inawasilisha katika utekelezaji wa mambo muhimu ambayo ni misingi ya utekelezaji wa jumla katika mambo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Kambi ya Upinzani vile vile imehoji au imeshauri kwamba, wakati tunatengeneza asilimia au tunafanya tathmini ya deni tulilonalo la Taifa tumekuwa tukisahau dhamana za Serikali, ni kweli Deni la Taifa haliundwi na kukopa ile *cash* taslimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile *contingent liability* ni sehemu ambayo ni dhamana kwa Kiswahili, ni lazima tunapotengeneza deni la Taifa baadaye tuseme katika *broad term, contingent liability* ikiongezwa inafanya Deni la Taifa liwe na ukubwa wa kiwango gani. Kwa sababu baadaye ikiwa wale uliowadhamini watashindwa kulipa, basi ujue kwamba wewe una deni la kulikabili kwa niaba yao kwa sababu uliwawekea dhamana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri ni mzuri, ni jambo la kawaida katika utaratibu wa *financial services*, hili tunakubali kulitazama kama sehemu ya pili ya kutazama *size* ya *National debt* (*debt stock*) wakati tuna *estimate* kwa sababu ni lazima tu-*include* vile vile dhamana ambazo tunawekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda naomba nichukue nafasi hii niseme, mawazo mengi mazuri kutoka Kambi ya Upinzani tutayafanyia kazi ili baadaye waweze kupata majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine limetoka kwa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi ambaye amependa kuuliza mambo kadhaa, moja utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Tume ya pamoja. Ni kweli majukumu ya msingi ya Tume ya Pamoja ya Fedha kwa mujibu wa Katiba na amesema katika maelezo yangu wakati nawasilisha hotuba ya Wizara sikufafanua vizuri kwa mujibu wa Ibara ya 133 na Ibara ya 134 ya Katiba, ni namna gani na majukumu yale yakoje.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed amesema kweli. Ni kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatunza akaunti maalum itakayoitwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja na ambayo itakuwa ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambamo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge kwa

madhumuni ya shughuli ya Jamhuri ya Muungano kwa mambo ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara hiyo aliyopenda niifahamu ya 134 ambayo ipo katika kifungu kidogo cha (2), inasema majukumu ya Tume yatakuwa ni:-

Kwanza kuchambua mapato na matumizi yatokanayo na au yanayohusu utekelezaji wa mambo ya Muungano, na kutoa mapendekezo kwa Serikali mbili kuhusu mchango na mgawo wa kila mojawapo ya Serikali hizo. Ni kweli kabisa.

Pili, inasema kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha za Jamhuri ya Muungano na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili tumekuwa tukilifanyia kazi na ndiyo maana toka niingie katika nafasi hii tumeshakutana na mwenzangu Waziri wa Fedha kutoka Zanzibar karibu mara nne kwa sababu ya kuheshimu kipengele hiki cha 134(2)(b). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la tatu ni kwamba Ibara hiyo vile vile inasema kutekeleza majukumu mengine ambayo Rais ataipatia Tume au kama Rais atakavyoagiza na kwa mujibu wa sheria itakayotungwa na Bunge. Haya yote tunayatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine alilotaka kujua Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed ni kwamba, deni la Taifa linaendelea kukua, hata hivyo, Serikali imekuwa inakopa kwa miradi bila utafiti wa kutosha kuhusu gharama

za miradi hiyo. Akatoa mfano wa mkopo wa ujenzi wa kiwanja cha ndege Zanzibar ambao unasuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi ni kwamba dhamira yetu muda wote tunapokopa, hatukopi kwa sababu tunataka kula pesa, ikifika Serikali inakopa kwa sababu ya kula pesa tutakuwa tumekosea. Tunakopa kwa sababu tunataka kuwekeza katika miradi ya maendeleo. Tunakopa ili tuwekeze pale ambapo pesa italeta ufanisi wa kiuchumi, pale ambapo mradi utazaa mradi mwingine na pale ambapo matokeo ya uwekezaji yataleta ahueni katika maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kweli Serikali tunapokopa nje na ndani ya nchi kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo tunazingatia kwanza andiko la mradi (*feasibility study*) na siku zote *feasibility study* inaonesha kwamba *investment* itakuwa *viable or not viable* kulingana na *criteria* ambazo sisi tunataka tukiri. Sasa ile *technical analysis* inapotuambia mradi huu haufai, basi tunaishia hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa kwamba Serikali ya Zanzibar inafaidika vipi na faida inayopatikana kutokana na Benki Kuu. Serikali ya Zanzibar imekuwa ikipata mgawo wake wa Fedha kwa asilimia 4.4 ya gawio la benki Kuu. Kwa mfano, kiasi kilichopelekwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutokana na gawio la Benki Kuu kwa mwaka 2010 mpaka 2011 ni shilingi bilioni 7.7. Kwa hivyo tumekuwa tukitoa kulingana na *formula* ambayo tumekubaliana mpaka hapo *formula* itakapobadilika, lakini hivyo ndiyo tumekuwa tunatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la viwango vya mgawo linashughulikiwa na pande mbili, pindi Serikali ya Muungano ya Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kama mojawapo ya Muungano katika sekta ya fedha zilizobakia kupatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hoja nyingine kubwa ambayo ni changamoto ni kwamba, imefika wakati mkopo kufikia muda mrefu, hadi miezi tisa kwa mteja kupatiwa fedha. Naomba niseme wazi kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwamba, si makusudi, kwamba siku zote mtu akienda katika chombo cha pesa akae muda wote huo, kabla ya kupata majibu, kwa sababu unapokwenda kuhitaji hela unakuwa na shida na mradi ule unasubiri kupata fedha ili u-*take off* au mradi uendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utoaji wa mikopo hutegemea aina ya mikopo ambayo mteja amekuwa anaomba. Aidha, muda ambao mteja anatumia katika kukidhi matakwa ya mkopo ya biashara huwa ni pamoja na kwamba uandikishwaji wa thamani kwa mamlaka zinazohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la pili, ni baadhi ya wakopaji wanakuwa wana taarifa chache kuhusu namna ya utunzaji wa mahesabu ya miradi yao. Kwa hali hiyo, wakati vyombo vya fedha vinahitaji takwimu au zinahitaji taarifa za fedha, basi jambo hili huwa linakuwa ndiyo pengine ni chanzo cha kuanza kuchelewesha. Lakini wote tunakubaliana kwa vyovyote vile vyombo vya fedha vinatarajiwa kuchukua muda mfupi sana, vitoe jibu badala ya mwombaji kukaa muda mrefu akisubiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine iliyojitokeza ni kwamba, Serikali iondoe kodi kwenye zana za kilimo na vipuli vya zana za kilimo. Kwa ufupi ni kwamba, tumeshafanya uchambuzi na katika *Finance Bill* ambayo tutaiwasilisha kesho, vifaa vingi vya kilimo vimepata *exemption* ili kusaidia na kuona kwamba tunasaidia Kilimo Kwanza na ukulima kwa ujumla ili uweze kuwa wa manufaa hasa vifaa vya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa vingi vya umwagiliaji pamoja na vifaa vya matrekta vimepata *exemption* na katika hali hiyo kodi kwa wakulima wanaotumia vyombo vya ukulima watapata unafuu kwa kupitia *exemption* hiyo ya *Finance Bill.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine mtaniwia radhi Wabunge nimeziweka kulingana na mtiririko badala ya kusema hii hoja imetoka kwa nani kwa sababu ya muda mfupi ambao nimepewa. Naomba mniwie radhi kama hutasikia hoja yako ikijibiwa ni kwa sababu ya muda, lakini nimeyaweka kwa pamoja kulingana na unyeti wa mambo yalivyojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kwamba, Serikali haijali mali zake hususani magari, majengo na viwanja havina hati. Kiujumla si dhamira ya Serikali kuona kwamba Serikali inakuwa na mali isiyo na mwenyewe, hapana! Sasa hivi tumeshaanzisha mchakato au daftari na kufanya *valuation* kwa ajili ya mali zote za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye mali hizo zote zinawekwa katika *register* ambayo Serikali itakuwa inafahamu mali zake pamoja na thamani. Kwa hiyo ni kweli,

ukipita huku na huko unaweza ukakuta mali hata viwanja kama wanavyosema, lakini tupo katika utekelezaji wa kukusanya takwimu hizo zote na kufungua *register* ya Serikali ili vyote viingie katika *asset* za Serikali. Ni jambo ambao halipendezi, Serikali kuwa na mali ambazo zimezagaa bila kuwa na rekodi maalum. Nakubalina na wazo la Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii iwekeze pia kwenye viwanda na kilimo na siyo kwenye majengo tu. Mifuko ya Hifadhi ya Jamii tayari imeshawekeza kwenye sekta ya viwanda kupitia umiliki wa hisa kwenye makampuni kama vile Tanzania *Breweries Limited*, Tanzania *Cigarette*, Tanzania *Portland* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Mifuko imewekeza kwenye sekta ya kilimo kupitia mikopo iliyokopeshwa, kwa mfano, Kiwanda cha Sukari cha Kagera (Kagera *Sugar Limited*) na *21Century Textile Mill* cha Morogoro. Hii ni mifano tu ya uwekezaji katika viwanda kutokana na hizo *social services.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, miongozi ya uwekezaji iliyotolewa na Benki Kuu kwa *Social Security Investments Guidelines* ya mwaka 2012, imeainisha maeneo ya uwekezaji ikiwemo sekta ya viwanda na kilimo. Ikumbukwe pia kwamba uwekezaji unaofanywa na mifuko unazingatia vigezo muhimu kama hivi vifuatavyo:-

Kwanza, usalama wa fedha za wanachama *safety*. Tunahamasisha Mifuko iwekeze, lakini hapo hapo tutambue Mifuko ile wakati wote ni lazima iwe na hela ambayo wale wastaafu waendelee kulipwa kila wakati inapohitajika.

Pili, angalizo lingine, faida itokanayo na uwekezaji husika, yaani wawekeze lakini waangalie kule wanakowekeza je, faida inayopatikana inakidhi kuwekeza pale na kuendelea kuwa katika biashara.

Tatu, waangalie uwezo wa Mfuko katika kulipa mafao kwa wakati kama nilivyosema *(the liquidity principle).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna mambo ya msingi wakati tunahamasisha vyombo vya *Social Security Funds* viwekeze katika maeneo muhimu ambayo yatasaidia upanuzi wa uchumi na huduma zingine. Lakini hapo hapo tunasema tuangalie usalama wa Mifuko yenyewe isije ikahamasisha kiwango cha kupitiliza ikakosa fedha za kuendelea kuwalipa wale wastaafu waliokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni mtaji wa *NBC*. Napenda kusema kwamba Benki Kuu ipo tayari kutoa maelezo juu ya hali ya mtaji wa *NBC* kama Msemaji wa Upinzani alivyotaka, tutaongozwa na Mwenyekiti wa Kamati. Lakini tungependa kutoa taarifa kuwa *NBC* kwa sasa inakidhi kiwango cha mtaji yaani *(co-capital) as of now. Co-capital* kiwango kinachohitajika kuhimili mahitaji ya kibiashara kulingana na *prudential guidelines* ya *best practice in banking.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kiwango cha uwiano kinachohitajika ni asilimia kumi kisheria na *NBC* wanayo asilimia 10.59 mpaka dakika hii ninayozungumza. Tumewataka *NBC* kuongeza kiwango hiki kama tahadhari katika kipindi cha miezi mitatu na wapo kwenye mchakato

wa kufanya hivyo. Kwa hiyo, kuhusu hoja ya *NBC* naomba kuliweka hili kama nilivyoeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo nimeona inahitaji maelezo inasema utitiri wa uanzishwaji wa Mashirika au Taasisi. Katika uanzishwaji wa mashirika au taasisi, Serikali inazingatia uhitaji wa umuhimu wa kuanzishwa kwenyewe. Aidha, Serikali itaendelea kuzingatia kuwa Mashirika na Taasisi ambazo zinaanzishwa ni zile tu zenye manufaa Kitaifa kwa kukidhi mahitaji muhimu na kwa kukidhi vigezo vilivyowekwa na bila kuumiza upande wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kwamba, kunahitajika taarifa kwenye urekebishaji wa Sheria ya Msajili wa Hazina, Ni kweli. Utaratibu wa kutunga upya sheria ya Msajili wa Hazina umeanza kwa kukusanya maoni ya wadau mbalimbali. Wiki moja na nusu imepita tulikuwa na Mkutano Mkuu wa wadau maalum Dar es Salaam, tukishughulikia suala hili la Sheria ya Msajili wa Hazina. Itakapokuwa imekamilika tutaileta hapa Bungeni ili muipitishe kuwa sheria kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa mikutano mitatu ya kukusanya maoni imeshafanyika kuhusiana na mchakato wa sheria. Mkutano wa kwanza ulijumuisha wadau wa ndani wa Wizara ya Fedha yenyewe, lakini Mkutano wa pili ulihusisha Wakuu wa Mashirika, Wenyeviti wa Bodi, baadhi ya Makatibu Wakuu ambao Wizara zao zina Mashirika na Taasisi nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mkutano wa tatu ulikuwa ni mkutano wa wadau maalum kutoka kwa

watalaam na wanataaluma mbalimbali ambao tulikutana Dar es Salaam wasiopungua watu mia tatu. Mkutano huo ulikuja na mchango mkubwa na mawazo mazuri ambayo yatatusaidia kuboresha rasimu ya sheria hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, utaratibu wa kuimarisha ofisi ya Msajili wa Hazina ni pamoja na hatua zinazochukuliwa za kuandaa Sheria Mpya ya Msajili wa Hazina ambapo sasa maoni ya wadau kama nilivyosema tunaendelea kuyakusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo likiwa ni kuimarisha ofisi hiyo kama Wabunge wanavyopendekeza, kuipa nguvu zaidi ya kisheria na kuijengea uwezo (*capacity building)* na iwe na mamlaka ambayo itakidhi mahitaji ya sasa na mahitaji ya kuona mashirika yetu yanafanya vile ambavyo wote tunatarajia mashirika hayo yafanye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kwamba, Shirika la *TIPPER* linaendeshwa kwa ubia wa asilimia hamsini kwa hamsini na mbia mwenza ndiye amepewa kuendesha kwa makubaliano yaliyopo. Aidha, sababu iliyopelekea kumpa kuendesha ni uzoefu wa kutunza na biashara nyingine. Hoja hii iliyoletwa kwamba tuifanyie kazi au tuitazame, nipende tu kusema hapa ushauri unachukuliwa na tutauangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilisema Sera ya Ubinafsishaji, iangaliwe upya ili mashirika kama *TTCL, ATCL na TRL* yaendeshwe na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na Waheshimiwa Wabunge wote, tunachukua mawazo yenu *with serious concern*,

tunasema Serikali iko tayari, imeshachukua hisa kwa asilimia mia moja katika *ATCL, TRL, KADCO* na inayaendesha yenyewe. Aidha, inajiandaa kuchukua hisa za *Battle* katika *TTCL* na tunaendelea kufanya uchambuzi na mashirika yote ambayo yanaonesha yana athari au yanaonesha yana mtikisiko wa kuweza kuhitaji uchambuzi na kuchukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ambayo Waheshimiwa Wabunge wameonesha wasiwasi wa kuchelewa kwa malipo ya mirathi. Katika hotuba yangu nimeeleza kwamba tumeweka utaratibu wa mafunzo na nimeeleza tumefanya nini katika kipindi cha mwaka huu uliopita na mbele ya safari tunalenga kufanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mambo mengine ambayo nimesema, tunataka kujenga nguvu ya ufahamu, nguvu ya uelewa, taarifa. Wadau wote wawe na taarifa za kutosha kitu gani katika mambo ya mirathi kinahitajika kama taarifa, wadau maana yake ni wananchi kwa ujumla, wadau maana yake vyombo vya fedha, wadau maana yake watumishi wa Mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka wote tuwe na upeo unaofanana katika shughuli hizi za Sheria ya Mirathi. Tunapokuwa tuna taarifa za kutosha, tunajua kabisa tutakuwa tumelifanyia kazi inayostahili na hii tumefanya na tunaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini licha kwa kuwepo na kumbukumbu za watumishi, malipo ya mirathi yanaweza kuchelewa kutokana na sababu zifuatazo:-

Ya kwanza kulingana na tathmini tulizozifanya, kutokamilika kwa utaratibu wa kifamilia wa mirathi ambako familia ya wafiwa hutakiwa kuwa na kikao cha familia ambacho kitamteua msimamizi wa mirathi. Imetokea maeneo mengine vikao vile vinakuwa havina muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa kama kikao kile kinachotakiwa kukaa na kukubaliana na wakateua nani awe msimazi wao, wao wenyewe wakachukua muda mrefu zaidi wa kukubaliana, kwa hivi ni sehemu ya kuchangia katika ucheleweshaji. Nimeona nilichukulie hili kiumakini zaidi kwa sababu linagusa Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sababu ya pili ya matatizo ya mirathi, familia huchelewa kufungua shauri la mirathi katika Mahakama zinazohusika kumthibitisha msimamizi wa mirathi ambaye wamemteua wao. Utaratibu wa Mahakama unahitaji kutoka tangazo ambalo litadumu kwa siku tisini katika magazeti yanayosomwa sana nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi, kuna utaratibu wa kuteua msimamizi, kuna utaratibu wa Mahakama, lakini wananchi wenyewe, wahusika wenyewe, wafiwa wanapoanza kuchukua muda mrefu kuchukua hii hatua ya kwanza, wanakuwa tayari wameshachangia katika tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, lakini la tatu, iwapo Marehemu alikuwa mtumishi wa Serikali, mwajiri wake anatakiwa awasilishe Hazina nyaraka zilizokamilika kwa maana ya taarifa muafaka za zile zinazotokana na familia ambazo hatimaye hupelekwa kwa

Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa ukaguzi wa mwisho kabla ya malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wote huu ambao naueleza, huchukua muda. Hata hivyo, iwapo nyaraka au kumbukumbu zote zimekamilika, malipo ya mirathi hayatakiwi kuchelewa. Lakini kitu kikubwa tunachelewa kuchukua hatua moja baada ya nyingine.

*(Hapa kengele ya kwanza ililia kuashiria kukaribia kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, najua hiyo ni kengele ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine au swali lingine lilikuwa ni je, ni lini basi Kanuni za Ununuzi wa Umma zitaletwa mbele ya Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi? Niseme tu kiufupi, ni kweli kwamba Wizara ya Fedha iliahidi kuziwasilisha mbele ya Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi Kanuni za Ununuzi wa Umma mara zitakapokuwa zimekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, basi nichukue nafasi hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kuwa tayari Wizara imekamilisha Kanuni hizo. Hizo Kanuni tumeshazitayarisha na ziko tayari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kabla ya kuziwasilisha mbele ya Kamati yetu ya Fedha na Uchumi, Kanuni hizo zinapaswa kupitiwa na Mwanasheria wetu Mkuu wa Serikali kwa lengo ya kuzihakiki ambayo ni kazi yetu ya ndani. Zoezi hilo la kuzihakiki linaendelea na mara

zitakapokuwa zimekamilika, zitawasilishwa mbele ya Kamati, ndipo zitangazwe kwa mujibu wa utaratibu tulionao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengine wengi katika wale 12 na wale wengine 34, masuala mengi yanafanana, lakini yaliyo mengi yamekaa katika hali ambayo nimeyajibu sasa hivi. Lakini kuna suala la kilio kikubwa la kuanzisha *micro-finance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili Waheshimiwa Wabunge, tafiti nyingi duniani zinaonesha kwamba, nchi yoyote iliyoboresha huduma za fedha na kuziteremsha mpaka kule chini waliko wananchi, ilithibitisha maendeleo ya kiuchumi. Kwa hali hiyo, kadiri unavyoboresha *outreach* yaani unateremka chini kupeleka huduma za fedha mpaka kule waliko wananchi wa chini, huduma za fedha zinasaidia katika mwenendo wa kuboresha uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kulitambua hilo, sisi Wizara ya Fedha, ndiyo maana tumeamua tuwe na kitengo ambacho kitashughulikia *microfinance* na tujenge uwezo wa namna gani sasa tutazame namna ya kupanua huduma hizi na kuzirasimisha kama nilivyosema kwenye hotuba yangu, huduma ambazo zisizo rasmi, tutazame namna ya hata kuzitungia Sheria na namna ya kuzipanua na ziwe za usalama kisheria mpaka kule chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma kama za *VICOBA* na zingine ambazo tunaweza tukazitaja, tuzirasimishe, tuziwekee Sheria, tuziwekee Kitengo na tuziwekee mkazo zifike mpaka kwa watu walio chini ili zisaidie upanuzi wa huduma za uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, naomba kwa sababu ya muda umepita, nihitimishe tu kwa kusema mimi na Waheshimiwa Manaibu Waziri wenzangu, tumefarijika kwa namna ya pekee mlivyotushauri, mlivyotuelekeza na tunatarajia kwamba mtaendelea kufanya hivyo. Tunachowaahidi ni kitu kimoja, tutajitahidi kuwa waaminifu kwa sababu Wizara ya Fedha ni lazima ioneshe uaminifu. Tutajitahidi kuwa *accountable*, tutajitahidi kuhakikisha kwamba yale yanayotarajiwa tunayatekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba nitoe shukurani na kusema ahsanteni sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mgimwa, tunakushukuru sana kwa majibu uliyoweza kuyatoa mambo ni mengi usingeweza kuya-*cover* yote. Sasa Katibu hatua inayofuata?

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 50- Wizara ya Fedha

Kif. 1001 - *Admin. and HR Management... ... ... ... ...*Sh. 6,611,210,000/=

**NAIBU SPIKA:** Pale pale kwenye mshahara pale Waheshimiwa.

**MHE. ENG. HAMAD Y. MASAUNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, afadhali kwa kuniona. Wakati nikichangia kwa maandishi nilieleza kwamba, mwaka 1994, Mshauri Mwelekezi ambae alipendekeza asilimia 4.5 kama ni mgao kwa Zanzibar, ilileta mashaka kidogo kutokana na vigezo ambavyo vilitumika, lakini wako ambao wanahofu kwamba pengine *data* ambazo zilitumika zilitarajia kuleta majibu hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakati tunaokwenda nao ni mrefu toka mwaka 1994, lakini pia Zanzibar iliwekeza asilimia 11.4 kama mchango wake kwenye *BOT*, sasa je, Mheshimiwa Waziri haoni ni wakati muafaka wa kuachana na hii asilimia 4.5 na badala yake mgao uwe asilimia 11.4?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli vigezo hivyo viliwekwa mwaka 1994 na ni kweli viliainisha aina ya mgao na kwa *percentage*, 4.5%. Muuliza swali Mheshimiwa Masauni anataka kujua kama je, huu sio wakati wa kutazama upya na kuvibadilisha. Nasema hivi, tunayo Tume ya Pamoja na kazi ya Tume ya Pamoja ni kupokea mapendekezo na yakiwasilishwa mapendekezo yatafanyiwa kazi kwa mujibu wa taratibu za Tume. Ahsante.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilipenda kujua juu ya suala la kuanzishwa kwa benki eneo la Mugandu. Kwa muda mrefu benki ya *CRDB* na benki ya *NMB* zimekuwa zikisuasua kupeleka benki eneo hilo ambalo lina wakulima hodari sana wa tumbaku na wananchi wake wana uchumi mzuri, wana fedha za

kutosha, lakini wamekuwa wakikosa huduma ya benki mpaka wasafiri masafa marefu kuja kuweka fedha zao Manyoni au Itigi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa umeme ndiyo sababu walikuwa wanaitoa, wanasema umeme hakuna, sasa kwa kuwa umeme umeshafika Mugandu iko hatua ya mwisho tu kuwasha huo umeme, je, Serikali au Wizara hii iko tayari kuzielekeza hizo benki kujiandaa kupeleka benki eneo katika hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge swali lake la uanzishwaji wa benki katika hiyo sehemu ambayo ameitaja, lakini *in general* uanzishwaji wa benki kunategemewa na *feasibility study*. Kwa hivyo, benki zikienda sio lazima *NMB, NBC, CRDB,* benki yoyote ikiona pana *potential* ya kuanzishwa kwa benki pale, tutaweza kujilipa basi itaanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo asitie mashaka na wameshakusikia wenye mabenki wote wataendelea kufuatilia hilo suala waone kama kweli kuna *potential* ya kuanzishwa benki sehemu hiyo ambayo ameitaja. *(Makofi)*

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu, nilichangia kuhusu Benki ya Wanawake; Benki hii ipo tu Dar-es-Salaam, lakini Mikoani haipo Benki na imekuwa inanufaisha wanawake wa Dar-es-Salaam na hata kule Zanzibar – Pemba, Unguja, hakuna Benki hii. Sasa Wizara, mna mkakati gani wa kuhakikisha Benki hii nayo inawezeshwa ifike kwenye Mikoa mbalimbali, iwafikie wanawake?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge Maryam Msabaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwahi kuelezea kuhusiana na hii Benki ya Wanawake kuwa, Zanzibar, nafikiri itakuwa ndio sehemu ya pili itakayokwenda Benki hii kwa sasa hivi. Lakini vilevile mchakato wa kupeleka hii Benki katika matawi mengi zaidi au mikoa mingi zaidi, unaendana na ule mpango wa Serikali wa kutoa pesa kila mwaka kwa ajili ya kuiwezesha hii Benki kuanza kupanuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi Benki hii bado imekuwa ikifanya mafunzo katika Mikoa mbalimbali, kwa ajili ya kuwatayarisha hawa akinamama kwa ajili ya kutumia Benki hiyo. Lakini hili ni jambo ambalo litafanyiwa kazi; kipindi cha miaka mitano ijayo, hii benki itakuwa imeenea sehemu kubwa zaidi kuliko ilivyo sasa hivi. Asante. (*Makofi)*

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia hoja ya uozo katika Sekta nzima ya ubinafsishaji, katika mchakato mzima wa ubinafsishaji. Nika-*cite* mfano wa ubinafsishwaji wa mgodi wa chumvi uvinza. Nikatoa mfano kwamba, mwekezaji aliuziwa, alibinafsishiwa mgodi kwa milioni 900, akalipa milioni 90, lakini akang'oa *plant* moja ambayo ilijengwa na Waitaliano pale Uvinza akauza nchini Iran, kwa takriban *4.5 billion.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tumekwenda na Naibu Waziri, pale Uvinza, amekuta ile *plant* iliyojengwa kwa msaada wa Waitaliano, kuna matofali matupu, hakuna kitu. Naomba msimamo wa Serikali, kwa sababu, jambo hili nimezungumza muda mrefu. Nimekwenda *CHC,* wanafanya Uswahili na ujanjaujanja, naomba *position* ya Waziri, kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mkataba unaonesha kwamba, malengo ilikuwa ni mtu huyu aendeleze na ameshindwa kuendeleza, kwa nini *plant* ile au mgodi ule usichukuliwe na Serikali, wapewe hata JKT kwa sababu, teknolojia inayofanyika pale ni ya chini mno, hata Magereza wanaweza kuendesha?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza inasikitisha kama Mwekezaji kwa mujibu wa masharti ya uwekezaji anakwenda kufanya kitu kilicho tofauti na Mkataba wa Uwekezaji, kwanza anakuwa amevunja Mkataba. La pili, kama kweli, Mkataba ilibidi anunue kwa milioni 900, akatoa *advance* ya milioni 90, lakini kama kulikuwa na *bad intention* itakayokuwa *established* kwamba, kutokana na alichokilipa *immediately* aka-*dispose for 4.5 billion,* kwa hivi Mkataba uangaliwe. Nasema kwa niaba ya Serikali, tutalifanyia kazi tuone ni nini kilitokea, ni nini uhalali kwa mujibu wa Sheria kwa sababu, *on the face of it, it's unfair.*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilijaribu kuzungumzia suala la noti mbili ambazo Serikali yetu imekuwa nazo; kwa mfano, kuna noti mbili za 10,000/=, 5,000/=, 2,000/=, 1,000/=

na 500/=. Noti hizi, hususan mpya, zimekuwa ni noti ambazo zinachakaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka kupata ufafanuzi kwamba, hali ya kuendelea kutumia noti hizi mbili, itaendelea mpaka lini? Na sasa hivi ni takribani mwaka wa pili, tunatumia noti mbili katika nchi moja? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Noti mbili ndio nini, Mheshimiwa Silinde?

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, noti za aina mbili zenye thamani moja. Kama kuna 10,000/= ya zamani na 10,000/= mpya, kuna 5,000/= ya zamani na 5,000/= mpya. Kwa hiyo, sasa tunataka jibu katika hilo, tutaendelea mpaka lini kuwa na noti mbili? Tuamue moja, kama ni ya zamani au ya sasa?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Sera ya ubadilishaji wa Fedha, iliruhusu noti ya zamani iendelee kutumika sambamba na noti mpya, mpaka itakapobadilishwa yenyewe, ikaisha huko inakotoka. Kwa sababu, tunajua noti inaendelea kuzeeka, kwa hivi inapoendelea kuzeeka inarudishwa Benki, baadaye zitarudishwa zote. Lakini haikuwa na maana kwamba, itaendelea *infinitely.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama kuna mawazo ambayo Mheshimiwa Mbunge, anafikiri, sasa sio nzuri. Lakini Benki, inaruhusu, unaweza ukaibadilisha ukapata noti mpya, lakini haikuwa na maana kwamba, hiyo itaendelea kwa kudumu. Ilikuwa nafasi kwa wananchi, ili wasiwe na wasiwasi, wachukue muda ambao watakwenda kubadilisha. Tofauti na miaka iliyopita

ambapo tuliwawekea kipimo cha miezi miwili au miezi sita au mwezi mmoja, kwa hivi kwa uzoefu tu, ilionekana kwamba, wananchi wetu walisumbuka, hasa wale waliokuwa wanakaa Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, kwa kuwa noti zimeonekana kwamba, bado zilikuwa zinatumika, ziko nzuri, lakini tunaendelea kupokea maoni ya wananchi. Ikiwa wananchi wanakuwa na maoni ambayo yanasaidia kubadilisha utaratibu, basi Serikali, itafanya utaratibu wa kuziondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, hoja ni nzuri kwamba, kama kuna sababu sasa ya kuziondoa ambazo wananchi wanaona kwamba, ni wakati tuziondoe, tutafanya hivyo. Lakini haikuwa na maana kwamba, itaendelea *infinitely,* baadaye zitakwisha huko, halafu baada ya kwisha, hakutakuwa tena na noti ya zamani.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Waziri, Akaunti ya Pamoja ni hitaji la Kikatiba. Hitaji ambalo…

**MWENYEKITI:** Sio kwamba, lilishaulizwa na Mheshimiwa Massauni, hilo?

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda katika *angle* nyingine, ni hitaji ambalo linataka kila Serikali au katika Serikali zetu mbili hizi, kila mmoja achangie. Sasa Mheshimiwa Waziri, tunapozungumzia Tume ya Kuondoa Kero za Muungano kwamba, haiko Kikatiba. Ninachotaka kujua, hii Katiba

umeilia Kiapo, ni lini Wizara yako itaheshimu kipengele hiki cha Katiba na kuanzisha akaunti ya pamoja? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naona Mheshimiwa aliongea kwa jazba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufunguaji wa Akaunti ya Pamoja, ni jukumu la Serikali zote mbili. Hata hivyo, maoni ya *GFC,* ambayo yatasababisha *operational* ya ile Tume ya Pamoja, kwa upande wa Zanzibar, tayari wameshakamilisha. Bado tunasubiri mchakato ukamilike hapa, hasa Baraza la Mawaziri kwa upande wa Tanzania Bara, *so that* watakaa pamoja na kuangalia hayo maoni yanasemaje. Kwa hiyo, Akaunti ya Fedha ya Pamoja, itafunguliwa na *formula* hasa ya hayo mapato, itakuwa *operationed.*

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nilipochangia kwa maandishi, nilizungumzia kuhusu tatizo la mishahara hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa sasa hivi tuna teknolojia ya mitandao, lakini hili tatizo bado limekuwa kubwa sana na ni aibu sana kwa nchi yetu. Naomba Mheshimiwa Waziri, labda atueleze ni lini sasa litakwisha kabisa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi wa swali la wananchi wa Iringa Mjini? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, hakuna anayefurahi na tatizo la mishahara hewa. Ndio

maana kwa kudhamiria kabisa, tumelileta Bungeni, Waheshimiwa Wabunge, mpate taarifa na tukaeleza, watu wangapi tumegundua na tumesimamisha malipo hayo. Sasa tunakwenda hatua ya pili, kubaini kama kuna watu waliobaki. Lakini Ofisi za Nidhamu, zimeelekezwa kuchukua hatua kwa wale wote waliosababisha tatizo la kulipa mishahara hewa.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikopa kwa ajili ya kununua Rada. Kama Naibu Spika, asubuhi alivyofafanua, tumerejeshewa fedha. Lakini mkopo ule, tulichukua pamoja na riba. Niliuliza katika mchango wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, mkopo ule kwanza tumeumaliza kulipa? Kama tumeumaliza, tumelipa kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, tukilinganisha na fedha ambazo zimerejeshwa, yaani kwa maana ya tumelipa kiasi gani *principle* na riba na fedha ambazo zimerejeshwa kutokana na manunuzi hayo ya Rada, je, Serikali, inakuwa imepata hasara au inakuwa imepata faida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba swali hili Mheshimiwa Waziri wa Fedha, aweze kulijibu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza swali zuri, lina sehemu tatu. Lakini kwa mujibu wa maadili ya Kibunge, tunatakiwa kuja na jibu lililo sahihi kwa asilimia mia moja. Atupe tukalifanyie kazi, mpaka dakika hii, maana ukisema riba maana yake ni mpaka dakika hii, ni *percent* ngapi? Kwa hiyo, ile hatutaki kudanganya Bunge, tumekatazwa. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi zaidi kuhusiana na mkakati ulioletwa kwenye bajeti hii na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, magari yatakayoingizwa nchini kwetu, yawe ni yenye umri wa kutumika usiozidi miaka nane, badala ya ile kumi iliyokuwepo. Nina mashaka Watanzania wengi, hususan waajiriwa wapya ambao nao wangependa kununua na kumiliki magari, watashindwa kukidhi gharama za kununua gari ambalo lina umri usiozidi miaka nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa anachosema Mheshimiwa Dokta Kigwangala, ni kweli, tulileta ombi hilo na ni kweli, tutaliona kwenye *Finance Bill.* Tulipendekeza kupunguza ruksa ya magari yanayoingizwa kutoka miaka kumi mpaka miaka nane, tulikuwa na sababu tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kwanza; magari ya zamani kwa utafiti uliofanyika duniani kote, yanatumia mafuta mengi kuliko magari yaliyo mazima. La pili; wakati unafanya *service,* unagharimu pesa nyingi. Tatu; yanakupa gharama kubwa kununulia *spare parts,* ukilinganisha na magari mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho la nne, tuko katika *East Africa Region,* ambayo tunakwenda kwenye *Convergence,* Kenya, imesha-*ban* magari ambayo yana umri wa miaka nane. Uganda, wanaelekea watakuja kuwa na Sera ya sisi ya umri wa miaka nane. Mauritius, ninapozungumza hivi, wamesha-*ban* magari yote zaidi ya

miaka sita; kwa hivi, katika Sera ya kuelekea kwa pamoja, tunaelekea kugota katika magari ya miaka nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na magari ya miaka nane, si kwamba, tuna gari mpya, lakini bado tunasema Watanzania wetu ni masikini; lakini katika kuwasaidia waweze kupata, tusiwaruhusu wanunue kitu ambacho kwanza, kitawaletea gharama zaidi, halafu kitafanya *pollution.*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, nakushukuru sana.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts* … ...Sh. 1,036,177,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning* … … Sh. 35,862,822,000/=
Kif. 1004 – *Legal Services* … … … … … Sh. 799,309,000/=
Kif. 1005 – *Government Communication Unit* … … … . Sh. 771,017,000/=
Kif. 1006 – *Internal Audit Unit* … … … …Sh. 377,483,000/=
Kif. 1007 – *MCC Tanzania* … … … … … Sh. 450,000,000/=
Kif. 1008 – *Procurement Management Unit* … … … …Sh. 572,470,000/=
Kif. 1009 – *Public Procurement Policy Unit (PPU)* … … … … …Sh. 939,544,000/=
Kif. 2003 – *Treasury Registrar* … … … …Sh. 38,573,103,000/=
Kif. 3001 – *Internal Auditor General* … … Sh. 4,806,273,000/=
Kif. 5001 – *Govt Asset Manag. Division* … … … … … … … Sh. 4,121,630,000/=
Kif. 6001 – *Financial Mgt. Inform. Systems Div.* … … … … … Sh. 2,012,604,000/=

Kif. 6002 – *Tax Revenue Appeals Board* … Sh. 808,580,000/=
Kif. 6003 – *Technical Audit Unit* … … … … … Sh. 0/=
Kif. 6004 – *Tax Revenue Appeals Tribunal* …Sh. 670,690,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 45 – Ofisi ya Ukaguzi ya Taifa**

Kif. 1001 – *Admin. and HR Management*… … … … …Sh. 22,415,042,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit* … … … … … … … … Sh. 2,278,346,000/=
Kif. 1003 – *Internal Audit Unit* … … … …Sh. 1,016,395,000/=
Kif. 1004 – *Ministrerial Audit Division* … … Sh. 7,912,772,000/=
Kif. 1005 – *Regional & Local Gov't Audit Div.* ... … … … ...Sh. 11,552,955,000/=
Kif. 1006 – *Value for Money Audit Division* … … … … … … … Sh. 2,055,909,000/=
Kif. 1007 – *Treasury Audit Division* … … ... Sh. 2,691,587,000/=
Kif. 1008 – *Techn. Support, Research and Consultancy* … … … … ... ...Sh. 5,095,100,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 23 – Idara ya Mkaguzi Mkuu**

Kif. 3001 – *Public Debt Management* … …Sh. 350,000,000/=
Kif. 3002 – *Expenditure Management* … Sh.25,400,000,000/=
Kif. 3003 – *Financial Management* … ... Sh. 40,501,754,700/=
Kif. 3004 – *Systems and Internal Audit* … Sh. 4,781,779,000/=
Kif. 3005 – *Sub Treasury Arusha* … … … Sh. 159,000,000/=

Kif. 3006 – *Sub Treasury Coast* … … … … Sh. 138,000,000/=
Kif. 3007 – *Sub Treasury Dodoma* … … … Sh. 256,000,000/=
Kif. 3008 – *Sub Treasury Iringa* … … … … Sh. 149,880,000/=
Kif. 3009 – *Sub Treasury Kagera* … … … …Sh. 140,000,000/=
Kif. 3010 – *Sub Treasury Kigoma* … … … ..Sh. 149,000,000/=
Kif. 3011 – *Sub Treasury Kilimanjaro* … … ..Sh. 156,000,000/=
Kif. 3012 – *Sub Treasury Lindi* … … … … ...Sh. 145,000,000/=
Kif. 3013 – *Sub Treasury Mara* … … … … ..Sh. 141,000,000/=
Kif. 3014 – *Sub Treasury Mbeya* … … … …Sh. 143,000,000/=
Kif. 3015 – *Sub Treasury Morogoro* … … …Sh. 168,000,000/=
Kif. 3016 – *Sub Treasury Mtwara* … … … ...Sh. 166,101,300/=
Kif. 3017 – *Sub Treasury Mwanza* … … … ..Sh. 149,000,000/=
Kif. 3018 – *Sub Treasury Rukwa* … … … … Sh. 148,000,000/=
Kif. 3019 – *Sub Treasury Ruvuma* … … … Sh. 139,000,000/=
Kif. 3020 – *Sub Treasury Shinyanga* … … …Sh. 138,000,000/=
Kif. 3021 – *Sub Treasury Singida* … … … …Sh. 139,000,000/=
Kif. 3022 – *Sub Treasury Tabora* … … … …Sh. 142,000,000/=
Kif. 3023 – *Sub Treasury Tanga* … … … … Sh. 140,000,000/=
Kif. 3024 – *Sub Treasury Manyara* … … … Sh. 140,000,000/=
Kif. 4001 – *Local Government Finances* … Sh. 420,000,000/=
Kif. 7001 – *Pension and Gratuity* … … … ..Sh. 629,250,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 22 - Public Debt and General Services**

Kif. 1001 – *Admin. and HR Management*… … …Sh. 2,735,909,673,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

## Fungu 21- Hazina

Kif. 2001 – *Government Budget Division* … … … … … … Sh. 517,718,507,000/=
Kif. 2002 – *Policy Analysis Division*… … Sh. 198,046,851,000/=
Kif. 4001 – *External Finance Division*… … Sh. 6,171,398,000/=
Kif. 4002 – *Public Private Partnership Unit*… … … … … Sh. 1,098,498,000/=
Kif. 7001 – *Poverty Eradication and Empowerment*… … … ... ... Sh. 2,539,394,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 13 - Financial Intelligence Unit

Kif. 1001 – *Admin and HR Management* … … … …Sh. 1,714,264,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*… … Sh. 56,863,000/=
Kif. 1003 – *Internal Audit Unit* … … … … Sh. 29,030,000/=
Kif. 1004 – *Monitoring Unit*… … … … … Sh. 95,870,000/=
Kif. 1005 – *Inspection Unit*… … … … … Sh. 52,820,000/=
Kif. 1006 – *Procurement Management Unit*… … … … … Sh. 39,240,000/=
Kif. 1007 – *Legal Services Unit*… … … …Sh. 34,120,000/=
Kif. 1008 – *Manag. Information System Unit*… … … … … … Sh. 141,600,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 10 - Joint Finance Commission

Kif. 1001 – *Admin. and HR Management… … … … …* Sh. 1,654,643,260/=
Kif. 1002 – *Internal Audit Unit… … … …* Sh. 40,754,000/=
Kif. 2001 – *Technical Department… …* Sh. 212,176,000/=
Kif. 2002 – *Zanzibar Office… … … … …* Sh. 90,672,740/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

## Fungu 50 – Wizara ya Fedha

Kif. 1001 – *Admin. and HR Management … … … … …* Sh. 3,280,500,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts … … … …* Sh. 0/=
Kif. 1003 – *Policy and Planning … … …*Sh. 4,129,688,000/=
Kif. 1005 – *Government Communication Unit … … …* Sh. 476,000,000/=
Kif. 1007 – *MCC Tanzania … … … …* Sh. 533,366,003,000/=
Kif. 1009 – *Public Procurement Policy Unit (PPU) … … … … …* Sh. 544,500,000/=
Kif. 2003 – *Treasury Registrar … … … … …* Sh. 672,800,000/=
Kif. 3001 – *Internal Auditor General … …* Sh. 1,623,050,000/=
Kif. 5001 – *Government Asset Management Division … ... …* Sh. 1,578,572,000/=
Kif. 6001 – *Financial Mgt. Inform. Systems Division … … … …* Sh. 843,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 45 – Ofisi ya Ukaguzi ya Taifa**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management* … … … … …Sh. 7,500,000,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit* … Sh. 2,123,927,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 23 – Idara ya Mkaguzi Mkuu**

Kif. 3003 – *Financial Management* … … Sh. 6,020,320,000/=
Kif. 3004 – *Systems and Internal Audit* … …Sh. 102,520,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 21- Hazina**

Kif. 2001 – *Government Budget Division*… … … … Sh. 20,758,039,000/=
Kif. 2002 – *Policy Analysis Division* … … Sh. 94,942,543,000/=
Kif. 4001 – *External Finance Division* … …Sh. 1,465,000,000/=
Kif. 7001 – *Poverty Eradication and Empowerment* … … ... ... ... Sh. 1,790,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 13 - Financial Intelligence Unit

Kif. 1001 – *Administration and HR Management* … … ... ... ... ...Sh. 267,800,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*
*(Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mheshimiwa Waziri, Taarifa!

**TAARIFA**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi, imeyapitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali, kwa Mwaka 2012/2013 kwa Mafungu bila marekebisho na kuyapitisha. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu, liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka 2012/2013 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawakumbusha kwamba, ile futari ya *Basement* bado ipo, inayoandaliwa na Mheshimiwa Hawa Ghasia. Vile vile niwakumbushe wale ambao walipewa kadi kwa ajili ya kwenda *Dodoma Hotel,* kwa mwaliko wa Mheshimiwa Stephen Wassira, waelekee huko. Kwa maana hiyo, ule mwaliko wa *St. Gasper,* umefutwa ni *Dodoma Hotel.*

Waheshimiwa Wabunge, muda hauko upande wetu na kwa sababu kesho tunamaliza shughuli zetu, kwa hiyo, hapa atakuwepo Mheshimiwa Spika. Hivyo, naomba nichukue fursa hii kuwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge, kwa muda wote ambao tumekuwa hapa Dodoma, kwa ushirikiano mkubwa ambao tumepeana, kwa kazi nzuri ambayo tumefanya kwa niaba ya Watanzania.

Naomba niwashukuruni sana Wabunge wote kwa ushirikiano mkubwa sana sana sana ambao mmetuonesha. Niwashukuru pia wapiga kura wangu wa Kongwa, kwa imani ambayo wanaendelea kuwa nayo kwangu. Niwahakikishie baada ya Bunge hili, nitaanza kwenda kuwatembelea sasa Vijijini. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya Bunge hili kwisha kesho, nawatakia kila la heri katika safari ya kurudi nyumbani. Wengine husema Mwenyezi Mungu awatangulie, lakini nina wasiwasi, akiwatangulia hamuwezi kumkuta; naomba Mwenyezi Mungu, aende pamoja nanyi sambamba, kila mmoja wenu afike salama. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa maneno hayo, naomba niahirishe sasa shughuli za Bunge, hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.00 jioni, Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 16 Agosti, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*